# KISWAHILI

## Kwa Vyuo Vya Ualimu (TTC)

## Mwongozo wa Mkufunzi

## 1

**Mchepuo wa Elimu ya Lugha (LE)**

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya  Bodi ya Elimu Rwanda.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# VIFUPISHO

***n.k***: *na kadhalika*

***k.v***: *kama vile*

***tnbh***: *tanbihi*

***m.f***: *mfano*

***agh***: *aghalabu*

***Bi.*** *: Bibi*

***Bw.*** *: Bwana*

***k.m*** *: Kwa mfano*

# DIBAJI

Mkufunzi mpendwa,

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mkufunzi kwa mwaka wa kwanza, mchepuo wa Elimu ya Lugha katika vyuo vya ualimu.

Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo,ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi , kwa msaada wa wakufunzi, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao bali hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mkufunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako litakuwa:

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano kwa wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu,
- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya Mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi,
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano,
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani,
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti,
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa mwanafunzi ,
- Kwa kukusaidia katika kazi yako ya kufundisha, yaliyomo katika mwongozo huu wa mkufunzi yanayeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu tatu (3).

Sehemu ya 1: Inayeleza muundo wa kitabu hiki na kukupa mbinu na maelekezo ya ufundishaji.

Sehemu ya 2: Inakupa sampuli ya andalio la somo kama marejeleo ya mchakato wa kuandaa somo.

Sehemu ya 3: Inatoa mwongozo au maelekezo ya ufundishaji kwa kila dhana iliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi .

Ingawa mwongozo huu wa mkufunzi una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi , unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mkufunzi, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda ( REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa.

Pongezi maalum ziwaendee walimu kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. Irénée NDAYAMBAJE**

**Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Elimu Rwanda**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi. Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati .

Shukrani zangu za kwanza ziwaendee wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu katika kukiandaa na kukiandika kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

# YALIYOMO

**VIFUPISHO**..........iii
**DIBAJI**..........iv
**SHUKRANI**..........vii
**SEHEMU YA I: UTANGULIZI WA JUMLA**..........1
1.1. Muundo wa mwongozo wa mkufunzi..........1
1.2. Mwelekeo wa ufundishaji..........1
1.2.1. Mwelekeo wa kuendeleza uwezo..........1
1.2.2. Kuingizwa kwa masuala mtambuka..........3
1.2.3. Uangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum..........5
1.2.4. Mwongozo wa tathmini..........6
1.2.5. Mbinu na mikakati ya kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji..........7
1.2.6. Mbinu za ufundishaji zinazokuza shughuli ya ujifunzaji shirikishi..........7
**SEHEMU YA II: SAMPULI YA ANDALIO LA SOMO**..........9
**SEHEMU YA III: UUNDAJI WA MADA**..........14
**MADA YA 1: MATUMIZI YA KISWAHILI SHULENI**..........15
1.1. Uwezo mahususi wa mada..........15
1.2. Ujuzi wa awali..........15
1.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada..........15
1.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada..........15
1.5: Orodha ya masomo..........16
SOMO LA 1: TARATIBU ZA SHULENI..........17
SOMO LA 2: USAFI SHULENI..........22
SOMO LA 3 : VIONGOZI WETU SHULENI..........27
SOMO LA 4: RATIBA YA WIKI YA MWANAFUNZI..........32
1.6. Muhtasari wa mada ya kwanza..........35
1.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi..........36
1.8. Tathmini ya mada ya kwanza..........36
1.9. Kazi za ziada..........38
1.9.1. Kazi za urekebishaji..........38

1.9.2. Kazi jumuishi ........................................................................38
1.9.3. Kazi za nyongeza ........................................................................38
**MADA YA 2: MSAMIATI KUHUSU MAZINGIRA YA NYUMBANI ..39**
2.1. Uwezo mahususi wa mada ........................................................39
2.2. Ujuzi wa awali ........................................................................39
2.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ......................39
2.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada........................................39
2.5. Orodha ya masomo ........................................................................40
SOMO LA 5: MAZINGIRA YA NYUMBANI ..........................................41
SOMO LA 6: MSAMIATI KUHUSU WATU WANAOPATIKANA NYUMBANI...48
SOMO LA 7: UHUSIANO WA FAMILIA..............................................54
SOMO LA 8: VIFAA VYA NYUMBANI NA USAFI WAKE..............58
SOMO LA 9: MSAMIATI KUHUSU MIFUGO ....................................64
2.6. Muhtasari wa mada........................................................................68
2.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ................................................69
2.8. Tathmini ya mada ........................................................................69
2.9. Kazi za ziada ........................................................................71
2.9.1. Kazi za urekebishaji ........................................................................71
2.9.2. Kazi jumuishi ........................................................................71
2.9.3. Kazi za nyongeza........................................................................72
**MADA YA 3: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALI ...73**
3.1. Uwezo mahususi katika mada ........................................................73
3.2. Ujuzi wa awali........................................................................73
3.3. Masuala mtambuka ........................................................................73
3.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada........................................73
3.5. Orodha ya masomo ........................................................................74
SOMO LA 10: SEHEMU ZA HOSPITALI..........................................75
SOMO LA 11: VIFAA VYA HOSPITALINI........................................81
SOMO LA 12: WAFANYAKAZI WA HOSPITALINI.........................87
SOMO LA 13: USAFI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALINI...92
SOMO LA 14: ADABU HOSPITALINI ..............................................96

3.6. Muhtasari wa mada ........................................................ 102
3.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ........................................ 102
3.8. Tathmini ya mada ya tatu ................................................ 103
3. 9. Kazi za ziada ............................................................... 104
3.9.1. Kazi za urekebishaji .................................................... 104
3.9.2. Kazi jumuishi .............................................................. 104
3.9.3. Kazi za nyongeza .......................................................... 105
**MADA YA 4: MSAMIATI KUHUSU MAENEO YA UTAWALA...106**
4.1. Uwezo mahususi wa mada ............................................. 106
4.2. Ujuzi wa awali ................................................................. 106
4.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ............ 106
4.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada .......................... 106
4.5. Orodha ya masomo .......................................................... 107
SOMO LA 15: WILAYA YETU .................................................. 108
SOMO LA 16: MAKAZI YA WATU ........................................... 115
SOMO LA 17: SIKUKUU ZA KITAIFA ...................................... 119
SOMO LA 18: AINA MBALIMBALI ZA VITAMBULISHO .......... 124
4.6. Mhutasari wa mada: ......................................................... 129
4.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ...................................... 129
4.8. Tathmini ya mada ya nne ................................................ 129
4.9. Kazi za ziada ................................................................... 130
4.9.1. Kazi za urekebishaji ..................................................... 130
4.9.2. Kazi jumuishi ............................................................... 130
4.9.3. Kazi za nyongeza .......................................................... 131
**MADA YA 5: MSAMIATI KUHUSU MAZINGIRA YA KIBIASHARA ........................................................ 132**
5.1. Uwezo mahususi wa mada ............................................. 132
5.2. Ujuzi wa awali ................................................................. 132
5.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ............ 132
5.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada .......................... 132
5.5. Orodha ya masomo .......................................................... 133
SOMO LA 19: MAWASILIANO SOKONI ................................ 134

SOMO LA 20: MAJADILIANO DUKANI ........................................ 139
SOMO LA 21: MATUMIZI BORA YA MIZANI ........................................ 143
5.6. Muhtasari wa mada ........................................ 149
5.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ........................................ 150
5.8. Tathmini ya mada ya tano ........................................ 150
5.9. Kazi za ziada ........................................ 152
5.9.1. Kazi za urekebishaji ........................................ 152
5.9.2. Kazi jumuishi ........................................ 152
5.9.3. Kazi za nyongeza ........................................ 153
**MADA YA 6: UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO ........................................ 154**
6.1. Uwezo mahususi katika mada hii ........................................ 154
6.2. Ujuzi wa awali ........................................ 154
6.3. Masuala mtambuka ........................................ 154
6.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada ........................................ 154
6.5. Orodha ya masomo ........................................ 155
SOMO LA 22: KUIGIZA MAZUNGUMZO ........................................ 156
SOMO LA 23: UMUHIMU WA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO .. 162
SOMO LA 24: VIFAA NA SIFA KATIKA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO .. 166
6.6. Muhtasari wa mada ........................................ 171
6.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ........................................ 172
6.8.Tathmini ya mada ya sita ........................................ 172
6.9. Kazi za ziada ........................................ 173
6.9.1. Kazi za urekebishaji ........................................ 173
6.9.2. Kazi jumuishi ........................................ 174
6.9.3. Kazi za nyongeza ........................................ 175
**MADA YA 7: UTUNGAJI WA INSHA ........................................ 176**
7.1. Uwezo mahususi wa mada ........................................ 176
7.2. Ujuzi wa awali ........................................ 176
7.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ........................................ 176
7.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada ........................................ 176
7.5. Orodha ya masomo ........................................ 177

SOMO LA 25: DHANA YA INSHA ........ 178
SOMO LA 26: AINA ZA INSHA........ 183
SOMO LA 27: INSHA YA MASIMULIZI ........ 189
SOMO LA 28: MWONGOZO WA KUTUNGA INSHA ........ 196
7.6. Muhtasari wa mada........ 202
7.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ........ 202
7.8. Tathmini ya mada........ 203
7.9. Kazi za ziada ........ 205
7.9.1. Kazi za urekebishaji ........ 205
7.9.2. Kazi jumuishi ........ 206
7.9.3. Kazi za nyongeza ........ 206
**MADA YA 8: DHIMA YA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA JAMII ...207**
8.1. Uwezo mahususi wa mada ........ 207
8.2. Ujuzi wa awali ........ 207
8.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ........ 207
8.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada........ 207
8.5.Orodha ya masomo:........ 208
SOMO LA 29: TUONGEE KISWAHILI SANIFU........ 209
SOMO LA 30: MAWASILIANO YETU........ 215
SOMO LA 31: UMUHIMU WA LUGHA ........ 220
8.6. Mhutasari wa mada........ 227
8.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi........ 228
8.8. Tathmini kuhusu mada ya nane........ 228
8.9. Kazi za ziada ........ 229
8.9.1. Kazi za urekebishaji ........ 229
8.9.2. Kazi jumuishi........ 229
8.9.3. Kazi za nyongeza........ 230
**MAREJEO........ 231**

# SEHEMU YA I: UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1. Muundo wa mwongozo wa mkufunzi

Kitabu hiki ni mwongozo wa mkufunzi katika mchakato wa ufundishaji wa somo la Kiswahili, mwaka wa kwanza, mchepuo wa elimu ya lugha katika vyuo vya ualimu nchini Rwanda. Kimetayarishwa kwa mwelekeo wa mtaala uegemeao katika uwezo. Mwongozo wa mkufunzi huu unaundwa na sehemu tatu.

Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla ambao unajishughulisha na namna ya kufundisha na kujifunza Kiswahili, kukuza uwezo wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, jinsi ya kushughulikia masuala mtambuka na inatoa mwongozo kuhusu tathmini.

Sehemu ya pili ni sampuli ya andalio la somo ambayo inaonyesha vipengele vya somo na jinsi ya kuandaa somo hilo.

Sehemu ya tatu inahusu uundaji wa mada tofauti. Sehemu hii inatoa taarifa kuhusu uwezo upatikanao katika mada, ujuzi wa awali wa wanafunzi kuhusu mada inayofundishwa, mwongozo kuhusu vidokezo, orodha ya masomo, mwongozo kuhusu namna ya kufanikisha masomo mbalimbali, maelezo ya ziada, tathmini ya mada, kazi za ziada ambazo zinajumuisha: kazi za urekebishaji, kazi jumuishi na kazi za nyongeza.

Majibu ya kazi zote, tathmini ya mada na kazi za nyongeza zilizomo katika kitabu cha mwanafunzi yanapatikana katika sehemu hii.

## 1.2. Mwelekeo wa ufundishaji

### 1.2.1. Mwelekeo wa kuendeleza uwezo

Kwa kusitawisha mafanikio ya elimu, Serikali ya Rwanda ilianzisha mtaala uegemeao katika uwezo katika shule za elimu ya jumla (CBC). Aina hii ya mtaala ilizinduliwa mwezi wa Aprili 2015 na kutekelezwa kuanzia mwaka wa 2016. Mtaala huu ulibuniwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi , jamii na soko la ajira.

Pamoja na mbinu ya ujifunzaji wa jumla inayomchukua mwanafunzi kama kiini cha ufundishaji, mtaala huu unalazimisha mabadiliko makubwa katika mbinu za ufundishaji na matumizi ya mbinu nyingi za tathmini kwa kuzingatia tathmini endelezi.

Hii ina maana kubwa kwa mkufunzi na utoaji wa msaada na mwongozo kwa shule ili kuhakikisha utekelezaji bora wa mtaala huu.

Mwalimu ana wajibu mkubwa katika kuboresha elimu na ndiye jambo la msingi katika kuamua mafanikio ya wanafunzi wa shule za chekechea na shule za msingi.

Ndiyo maana ni muhimu kuwapa wanafunzi uwezo ambao utawawezesha kutekeleza kwa ufanisi mtaala uegemeao katika uwezo kama inavyotarajiwa.

**Jinsi ya kuendeleza uwezo**

Uwezo hupatikana kwa muda mrefu kupitia mkusanyiko wa athari zitokanazo na mbinu za ujifunzaji unaotilia maanani uwezo. Ikumbukwe kwamba uwezo wa mwanafunzi hauendelezwi katika ombwe bali umeunganishwa wakati huo huo.

Kuhusisha wanafunzi katika ujifunzaji ni muhimu kwa mafanikio ya mtaala uegemeao katika uwezo.

Mwanafunzi anahitaji kuingizwa katika hali za kujifunza zilizo tofauti na katika hali ya vitendo ambapo ujifunzaji unayendelea mara kwa mara.

Kupitia mbinu shirikishi, wanafunzi wanapashwa kufikiria sana, kufanya utafiti, kutatua matatizo, kuwa wabunifu na wagunduzi, kuwasiliana na kushirikiana.

Miongoni mwa mbinu shirikishi, kuna hizi zifuatazo: maigizo, kazi za makundi, maswali na majibu, mbinu za ziara, kazi mradi,tukio,bungua bongo, majadiliano, kazi ya utafiti, michezo na mbinu nyingine nyingi.

Mfano unaofuata unaonyesha namna ambavyo wakufunzi wanaweza kusaidia wanafunzi kuendeleza uwezo wao.

**Mfano**:

a. Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kuwapatia zoezi linalowasaidia kuendeleza uwezo wao katika mada fulani inayofundishwa katika lugha ya Kiswahili.

**Kwa mfano**: Jadili umuhimu wa kutunza mazingira ya shuleni kwa wanafunzi .

b. Kundi limchague kiongozi na katibu wa kuandika maoni yanayotolewa katika majadiliano.

c. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kumalizika, majadiliano yasimamishwe na katibu kutoka makundi tofauti awasilishe

matokeo yao.

d. Uwezo unaoendelezwa ni: Ushirikiano, mawasiliano, tafakuri tunduizi, uongozi na usimamizi, utafiti na usuluhishaji wa matatizo, na ujifunzaji wa kudumu.

Zaidi ya uwezo upatikanao katika masomo mahususi, wanafunzi wanayendeleza pia uwezo wa kijumla unaopatikana kupitia hali mbalimbali.

### 1.2.2. Kuingizwa kwa masuala mtambuka

Katika kitabu hiki, mkufunzi awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

| **Masuala mtambuka** | **Mifano inayoonyesha namna ya kuingiza masuala mtambuka katika somo** |
|---|---|
| Elimu jumuishi | Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi analazimishwa kubainisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kuwaandalia mazoezi kufuatana na mahitaji yao. Shirikisha wanafunzi wote katika kazi walizoandaliwa bila upendeleo.<br><br>Mfano: Mpatie mwanafunzi aliye na ulemavu wa mwili (asiyeona) jukumu la kuongoza mjadala.<br><br>Mtafutie mahali pa kukaa na vifaa vya kutumia kufuatana na mahitaji yake. |
| Usawa wa kijinsia | Katika mchakato wa ufundishaji, mkufunzi analazimishwa kuandaa mazoezi ambayo yanashirikisha wavulana na wasichana na kuwasaidia kutumia uwezo waoipasavyo.<br><br>Hakuna kazi ambayo inatarajiwa kuwa ya msichana au mvulana.<br><br>Wakufunzi wangehakikisha kwamba wasichana na wavulana wanachukua nafasi sawa wakishiriki katika kazi za makundi, Mijadala na midahalo. |
| Elimu kuhusu amani na maadili | Katika mchakato wa ufundishaji, mkufunzi analazimishwa kuwahimiza wanafunzi kuwa na uvumilivu, ushirikiano, kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa pamoja, kusaidiana kwa pande zote, kuheshimu maoni ya wengine, kuheshimu maagizo na kuwepo kwa mazingira mazuri ya kujifunzia. |

| | |
|---|---|
| Mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji | Katika mchakato wa ufundishaji, wanafunzi wanalazimishwa kutunza vizuri vifaa vya shuleni na kutoviharibu kama vile vitabu, madaftari, madawati, n.k. Mkufunzi pia anaweza kuwasaidia kuchagua vitabu vya kusoma vinavyohusiana na masomo yao lakini vinavyokubaliwa katika mfumo wa elimu ya Rwanda. |
| Mazingira na maendeleo endelevu | Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji masuala ya mazingira na maendeleo endelevu yatashughulikiwa kama ifuatavyo:<br><br>-Mkufunzi aeleze wanafunzi umuhimu wa mazingira safi iwe nyumbani, shuleni, hospitalini, n.k.<br><br>-Wanafunzi wasichafue madarasa kwa kutupa karatasi au uchafu wowote katika mazingira ya shule wakati wa kusoma na baada ya maosomo. Washauriwe kutotema mate au kupenga ovyo mahali popote.<br><br>-Mkufunzi aweke maagizo ya kufanya usafi darasani na katika busitani za shule. |
| Mafunzo kuhusu uzalishaji mali / ujasiriamali | Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji mafunzo kuhusu uzalishaji mali/ujasiriamali yatashughulikiwa wakati ambapo: Wanafunzi wanao uwezo wa kutunga mashairi, hadithi na michezo ya kuigiza wakashiriki katika mashindano tofauti na kupewa zawadi au wakaunda klabu za michezo ya kuigiza na ambapo wanawaalika watu kutazama michezo ya kuigiza na kulipa pesa za kuingia. Hii inawasaidia wanafunzi kufahamu kuwa Kiswahili kinaweza kuwa chanzo cha shughuli za uzalishaji mapato na kujipatia ajira. |
| Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia | Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi atoe maagizo na kazi zisizochochea unyanyasaji wa kijinsia. Pia, anaweza kutoa kazi au vifungu vya habari vinavyoshughulikia afya ya uzazi na mpango wa kuboresha uzazi. |
| Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari | Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi atoe kazi na mada za kuzungumzia au kujadili madhara ya mauaji ya kimbari kwa jamii na jinsi ya kutupilia mbali itikadi yake. |

Mkufunzi awasaidie wanafunzi kuingiza masuala mtambuka haya kwa kila somo wanalojifunza na kutafuta suluhisho kuhusu masuala hayo.

### 1.2.3. Uangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum

Malengo ya ujifunzaji na ufundishaji humhusu kila mwanafunzi darasani bila ubaguzi au utengano wowote. Kwa hiyo, inambidi mkufunzi kuyakumbuka na kuyahudumia makundi mbalimbali ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu au ya kipekee katika ujifunzaji wao. Hao ni kama vile wanafunzi wenye tatizo la kutoona, kutosikia, kutoandika, kutosoma, kutozungumza na matatizo mengine ya kiakili.

Kuna watu wanaofikiri kwamba ni kazi ngumu kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji tofauti. Lakini, kwa kushirikiana shuleni, kwa kushirikiana na familia ya wanafunzi hao na jamii kwa ujumla, na kubadilisha mbinu za ufundishaji utakidhi mahitaji ya wanafunzi wote wakiwemo na wale wenye mahitaji maalum kwani baadhi yao huelewa masomo haraka haraka na wengine kidogokidogo.

Wanafunzi wangeweza kujitayarisha kushughulikia mahitaji maalumu ya kielimu kwa kuiga vitendo bora vya wakufunzi wao.

Kwa kuwashirikisha wote, mkufunzi hulazimishwa:

- Kutayarisha mazoezi anuai kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi .
- Kukumbuka kwamba wanafunzi hujifunza kwa njia tofauti. Kwa hiyo, mkufunzi anapaswa kutoa kazi mbalimbali za ujifunzaji kama vile (umithilishaji, muziki na uimbaji, kazi za nje ya darasa na michezo mbalimbali),
- Kushikilia usalama wa darasa na kuondoa usumbufu wowote. Hii itawasaida wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutopotoshwa na mazingira na hivyo watafuata mkufunzi vizuri,
- Kulirahisisha somo kwa kiasi kwamba kila mwanafunzi hulielewa. Wanafunzi wenye mahitaji maalum huwa na vikwazo kuelewa wanapopewa maagizo mengi kwa mfululizo. Bora kutumia sentensi rahisi na zinazoeleweka haraka ili kumsaidia kuelewa kilichoulizwa,
- Kutumia sentensi sahili zinazoeleweka unapoeleza maana au dhana mpya au unapotoa maagizo,
- Kutumia viungo vya mwili na ishara unapofundisha,
- Kuweka mwanafunzi aliye na mahitaji maalumu katika jozi yenye wanafunzi wengine ambao hawana mahitaji yao ya kipekee. Waache wafanye kazi pamoja ili mmoja ajifunze kutoka kwa mwenzake. Hakikisha kwamba wote wanashiriki kufanya kazi iliyotolewa. Wanafunzi wote watanufaika na mbinu hii.

- Kufanya kazi kuwa hai kwani inajulikana kwamba wanafunzi hujifunza kupitia mbinu mbalimbali. Wanafunzi wenye mahitaji maalum huenda wasifaulu katika mbinu moja na kufaulu katika mbinu nyingine. Kwa mfano, tumia picha na sauti kulingana na hali iliyopo,
- Kutumia vifaa halisi anavyoweza kuhisi na kugusa kwa yule aliye na matatizo ya kutoona,
- Kurahisisha kazi katika hatua ndogondogo au malengo ya ujifunzaji. Anzia kwenye kazi rahisi kabla ya kufikia ile ngumu,
- Kusaidia mwanafunzi kidogo kidogo na kumwacha kufanya kazi huku akishirikiana na wengine katika kazi za makundi.

### 1.2.4. Mwongozo wa tathmini

Tathmini ni jambo muhimu sana katika njia hii ya ufundishaji na ujifunzaji. Lengo kuu la tathmini ni kupima maendeleo ya somo ambapo mkufunzi huweza kuchagua aina ya tathmni kulingana na malengo yake.

- **Tathmini endelezi**

  Tathmini hii hulenga kupima jinsi ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea au kama makusudi au malengo ya ufundishaji na ujifunzaji yamefikiwa kwa kiwango fulani ili kuamua kuhusu uboreshaji wa baadaye. Tathmni hii inafanywa wakati masomo yangali yanayendelea na hulenga kuangalia uhusiano uliopo kati ya ufundishaji na ujifunzaji yaani uhusiano kati ya mkufunzi na mwanafunzi . Hujumuisha upimaji wa mwenendo wa somo kabla somo lifikie kikomo. Tathmini endelezi inapaswa kuwa na dhima mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji. Inambidi mkufunzi kuwahamasisha wanafunzi kufanya kazi na majaribio binafsi, mazoezi ya makundi, kwa kutumia mbinu zinazoegemea kwenye uwezo, maadili na mwenendo mwema kulingana na kila somo husika.

- **Tathmini ya jumla**

  Kila tathmini huwa na dhima yake katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, tathmini ya mwishoni mwa mada itafikiriwa na itafanyika mwishoni mwa mada nzima kabla ya kutangulia mada nyingine. Aidha, tathmini inayofanyika mwishoni mwa muhula na mwishoni mwa mwaka zitakuwa mojawapo ya tathmini za jumla na wakati huu hulenga kurekodi ujuzi, uwezo, maadili na mwenendo mwema miongoni mwa wanafunzi kiasi kwamba wakufunzi,

viongozi wa shule na wazazi hupata na kuchunguza matokeo ya tathmini iliyofanywa. Tathmni zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi zitamwelekeza mkufunzi kubashiri matatizo yaliyopo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kiwango cha kuwaelekeza wanafunzi kupata uwezo walionao katika somo hili. Hivyo basi, tathmini zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi ni msingi wa mambo mengine ambayo mwanafunzi atayakuta katika miaka mingine ya masomo yake ya Kiswahili kwa shule za sekondari.

### 1.2.5. Mbinu na mikakati ya kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji

Katika kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi achunguze mambo yafuatayo:

- Upekee wa somo,
- Kielelezo cha somo,
- Malengo maalum ya kutimiza,
- Kuchunguza idadi ya vipindi mahususi kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya somo,
- Maelekezo muhimu kuhusu vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana katika mazingira halisi,
- Jinsi wanafunzi watakavyokaa darasani,
- Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu,
- Uwezo na mtindo wa ujifunzaji.

### 1.2.6. Mbinu za ufundishaji zinazokuza shughuli ya ujifunzaji shirikishi

Ili kufanikisha malengo ya somo lake, mkufunzi azingatie njia zifuatazo:

- **Njia Shirikishi**: Njia shirikishi hutumia makundi ya wanafunzi ambapo mkufunzi huwawezesha wanafunzi kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Kinachopaswa kufanywa hapa ni kuwapatia wanafunzi wote fursa ya kushiriki katika shughuli zinazopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi . Hali hii hutokana na mazingira yanayojengwa na mkufunzi ambapo kila mwanafunzi ndiye ambaye huchukuliwa kama kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mkufunzi kama

vile majadiliano, midahalo na mazungumzo ya aina tofauti kama yalivyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi .

- **Njia ya kibinafsi:** Njia hii inahusu kazi binafsi za kila mwanafunzi ambapo atapewa kazi ama mazoezi yake binafsi ili aweze kufikia kiwango cha umilisi wa lugha kinachotarajiwa. Baada ya kufanya kazi na mazoezi hayo, ni vyema mkufunzi akumbuke kuambatanisha njia aliyoitumia na njia shirikishi kwa kumwomba mwanafunzi achunguze maoni na hoja za wanafunzi wenzake katika makundi yao. Katika njia ya kibinafsi, mkufunzi anaweza kuomba mwanafunzi , kwa mfano, kujisomea kifungu cha habari, kutambua maana za maneno mapya na kuyatumia katika sentensi zake, n.k.
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huchukua mwelekeo wa majadiliano kati ya mkufunzi na wanafunzi . Kuhusiana na mbinu hii, mkufunzi atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaweza kumwuliza mkufunzi wao naye akawajibu. Vilevile, maswali na majibu haya yanaweza kujitokeza kati ya wanafunzi wenyewe. Katika hali hii, mkufunzi atawaelekeza wanafunzi wake kujitafutia majibu kwa maswali wanayouliza huku akiwapa maelekezo muhimu au mwongozo unaofaa kwa kusahihisha makosa wanayoyafanya.
- **Maelezo ya mku funzi**: Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo. Katika njia hii, mkufunzi atakuwa mwelekezi na shughuli yake muhimu itaegemea katika kuwaongoza wanafunzi kupata ufahamu na uelewa unaofaa. Kwa hiyo, mkufunzi atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

# SEHEMU YA II: SAMPULI YA ANDALIO LA SOMO

## 1. ANDALIO LA SOMO

**Jina la shule: ..........................   Jina la Mkufunzi: ..................................**

| Muhula | Tarehe | Somo | Mwaka | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wa kwanza | 13.02.2020 | Kiswahili | Mwaka wa kwanza | Ya pili lugha | 5/5 | Dakika 40 | 45 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo kulingana na mahitaji yao** | Matatizo ya kutosikia vizuri: 1 |
| **Mada kuu** | Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali |
| **Mada ndogo** | Matumizi ya Kiswahili Nyumbani |
| **Uwezo mahususi wa mada ndogo** | Kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha na kuandika matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya nyumbani |
| **Kichwa cha somo** | Ufugaji ni kazi nzuri |
| **Malengo ya kujifunza** | Kupitia michoro na kifungu cha habari, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kutumia kwa usahihi msamiati wa mifugo katika mawasiliano yao ya kila siku. |
| **Mahali ambapo somo litafundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi , Kamusi ya Kiswahili sanifu, daftari, chaki, kalamu. |
| **Vitabu vya rejea** | Kamusi ya Kiswahili Sanifu,Toleo la pili, Oxford University press, Dar-es-Salaam (2004), Mpangilio wa masomo, Muhtasari wa somo. |

| **Muda na hatua za somo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | | **Uwezo wa jumla na**<br><br>**Masuala mtambuka**<br><br>**Vielezwe+maelezo mafupi** |
|---|---|---|---|
| | Katika makundi, wanafunzi wajadiliane kuhusu michoro na kusoma kifungu cha habari na kuchunguza umuhimu wa mifugo tofauti nyumbani | | |
| | **Wajibu wa mkufunzi** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **1. Utangulizi**<br><br>Dakika 4 | Mkufunzi aanze kwa kuamkia wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki katika somo.<br><br>Mkufunzi aulize wananafunzi, mmoja kwa mmoja maswali kuhusu somo lililopita na kuhakikisha kwamba wanakumbuka maelezo yaliyotolewa.<br><br>Mkufunzi anabandika michoro ya ng'ombe, mbuzi, kuku, kondoo kupitia michoro ya mifugo kwenye flip chati.<br><br>Mkufunzi, kufuatana na idadi ya vitabu, anaunda makundi tofauti darasani. | Wanafunzi wajibu maswali ya mkufunzi kuhusu kifungu cha habari walichosoma katika somo lililotangulia.<br><br>Wanafunzi wanajibu maswali ya mkufunzi.<br><br>Wanafunzi wanatazama michoro kwenye flip chat.<br><br>Wanafunzi wanaunda makundi ya wanafunzi | **Uwezo wa jumla**<br><br>**Mawasiliano katika lugha rasmi.**<br><br>Kupitia njia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mkufunzi katika makundi.<br><br>**Mawasiliano katika lugha.**<br><br>Katika makundi, wanafunzi watumie lugha ya Kiswahili kwa njia ya kujibu maswali ya mkufunzi na kuwasiliana kati yao. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **2. SOMO LENYEWE**<br><br>Dakika 30 | | | |
| **2.1. Zoezi la ugunduzi** | Mkufunzi anawaomba kutaja majina ya mifugo kwenye flip chati.<br><br>Awaombe wanafunzi wafungue vitabu vya Kiswahili kwenye ukurasa husika na kusoma kifungu cha habari wakiandika msamiati mpya wanaouona. | Wanafunzi wanataja michoro ya mifugo kwenye flip chati.<br><br>Wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa kimya, kisha waandike msamiati mpya katika madaftari yao. | **Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.**<br><br>Wanafunzi washirikiane katika makundi yao na kuheshimu haki na maoni ya wenzao.<br><br>**Masuala mtambuka**<br><br>**Usawa wa jinsia**<br><br>Wavulana na wasichana wafanye kazi pamoja katika makundi yao bila ubaguzi wowote.<br><br>**Elimu jumuishi**<br><br>Wanafunzi wenye matatizo mbalimbali washughulikiwe. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **2.2. Uwasilishaji wa wanafunzi** | Mkufunzi awaombe wanafunzi kuandika maneno mapya waliyoona kwenye ubao huku akiwaongoza kusoma maneno hayo kwa usahihi. Jaribu kueleza msamiati huo. | -Katika makundi yao waandike msamiati mpya kwenye ubao na wausome kwa usahihi.<br><br>Kutoa mchango kwa kila kundi kwa kueleza msamiati mpya. | |
| **2.3. Uchambuzi** | Baada ya kuelewa masmiati wote wa kifungu, mkufunzi anawaomba kujibu maswali ya ufahamu katika makundi yao.<br><br>Mkufunzi awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu maneno hayo na wajaribu kuyafafanua katika makundi yao wakitumia kamusi ya Kiswahili Sanifu.<br><br>Mkufunzi asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze wasahihishe kwenye ubao. | Wanafunzi , baada ya kuweza kuelewa msamiati mpya, katika makundi yao wajaribu kujibu maswali ya ufahamu katika madaftari yao. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **2.4. Hitimisho/**<br><br>**Ufupisho** | Mkufunzi aandike ufupisho wa somo ubaoni na aombe wanafunzi kuandika ufupisho huo katika madaftari yao | Wanafunzi waandike ufupisho wa somo katika madaftari yao. | |
| **3. Tathmini**<br><br>Dakika 6 | Mkufunzi aandike majina matano ya mifugo nyumbani kisha aombe wanafunzi , kila mmoja, kutoa umuhimu wa kila mfugo. | Kila mwanafunzi atoe umuhimu wa mifugo katika familia kwenye madaftari yao. | |
| **4. Tathmini ya mkufunzi** | Baada ya somo, mkufunzi ahakikishe ikiwa lengo la ufundishaji limefikiwa au la. | | |

# SEHEMU YA III: UUNDAJI WA MADA

# MADA YA 1:

# MATUMIZI YA KISWAHILI SHULENI

## 1.1. Uwezo mahususi wa mada

Kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha na kuandika matini fupifupi kwa kusisitizia msamiati maalum unaotumiwa katika mazingira ya shuleni.

## 1.2. Ujuzi wa awali

Katika shule za awamu ya kwanza (kidato cha 1) wanafunzi walisoma katika mada ya pili: Somo la kwanza: (kitabu cha mwanafunzi )

- Mazingira ya darasani,
- Msamiati wa mazingira ya shuleni,
- Shughuli za siku za mwanafunzi .

Aidha, masomo mengine ya mada hii yalishughulikia msamiati wa mazingira ya shuleni kwa ujumla.

## 1.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile uhifadhi wa mazingira, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu ujasiriamali, mafunzo kuhusu amani na maadili, desturi ya usanifishaji, na elimu jumuishi. Pia, wanafunzi watapata maarifa kuhusu mauaji ya kimabari ili waweze kutupilia mbali itikadi yake. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika.

## 1.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi, wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 1.5: Orodha ya masomo

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| Taratibu za shuleni | **Maarifa na ufahamu:**<br>**Stadi:** Kutumia msamiati unaofaa katika kuelezea mazingira ya shule na vitu vilivyomo.<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>- Kutunza vifaa na kuhifadhi mazingira ya shule. | 5 |
| Usafi shuleni | **Maarifa na ufahamu:**<br>**Kuelezea** kuhusu shughuli za usafi na uhifadhi wa mazingira shuleni<br>**Stadi:** Kutumia msamiati unaofaa katika kueleza mazingira ya shule na vitu vilivyomo.<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>Kuonyesha mwenendo mwema katika mawasiliano yake na viongozi na watu wengine wanaopatikana shule | 4 |
| Viongozi wetu Shuleni | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja na kuelezea majina ya wafanyakazi na shughuli zao za kila siku.<br>**Stadi:** Kutumia msamiati unaofaa katika kueleza mazingira ya shule na vitu vilivyomo.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuonyesha mwenendo mwema katika mawasiliano yake na viongozi na watu wengine wanaopatikana shuleni. | 5 |

| | | |
|---|---|---|
| **Ratiba ya wiki ya mwanafunzi** | **Maarifa na ufahamu:**<br><br>Kueleza shughuli zote zifanyikazo shuleni kulingana na ratiba wanayoitumia.<br><br>**Stadi:** Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya LI-YA katika umoja na wingi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuonyesha mwenendo mwema katika mawasiliano yake na viongozi na watu wengine. | **5** |
| **Tathmini ya mada** | | **4** |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | **23** |

## SOMO LA 1: TARATIBU ZA SHULENI

i. **Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza sehemu kuu za Shule,
- Kutaja vifaa vinavyotumiwa katika shule,
- Kutumia ngeli ya LI-YA na mabadiliko yanayojitokeza.

ii. **Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi ,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Michoro ya vifaa vinavyotumiwa shuleni .

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji.

iii. **Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hii ni mbinu ambapo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi :** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv. Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi . Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo:** ***Mkufunzi awaombe wanafunzi kutazama mchoro ulio katika kitabu cha mwanafunzi na kueleza wanachokiona kwenye mchoro huo. Kazi hii ifanyike katika jozi au katika makundi.***

**Mapendekezo ya majibu:**

- Kuna wanafunzi wanaokwenda shuleni.
- Kuna majengo ya madarasa ya shule.
- Mbele ya madarasa kuna bendera.

**Kusoma na ufahamu: Shule yetu ya Icyerekezo.**

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu. Kazi hii ifanyike katika makundi. Majibu yaliyopendekezwa ni yafuatayo:***

1. Majina ya watu wote wanaotajwa katika kifungu hiki ni: Mkuu wa shule, naibu mkuu wa shule, mkuu wa taaluma na wanafunzi .
2. Mkuu wa shule alizungumza na wanafunzi kwa lengo la kuwaelezea utaratibu wa shule na hasa zaidi kwa wanafunzi wageni.
3. Wanafunzi hao walikuwa katika kiwango cha elimu ya sekondari.
4. Mkuu wa taaluma ni mwalimu anayehusika na masomo na taarifa za kila siku za wanafunzi .
5. Ndiyo. Wanafunzi walifurahishwa na maelezo yaliyotolewa na mkuu wa shule, kwa sababu walimpigia makofi baada ya kutoa maelezo.
6. Kifungu hiki cha habari kinazungumzia kuhusu:

   b. Utaratibu wa shule ya sekondari ya Icyerekezo

7. Ofisi ya Taaluma hujishughulisha na :

   c. Masomo na kumbukumbu za kila siku za wanafunzi .

8. Maabara ni sehemu ambayo walimu na wanafunzi hufanyia:

   c. mazoezi ya sayansi kwa vitendo.

9. Ofisi ya walimu ni:

   c. Sehemu ya kufanyia kazi na kutayarisha masomo ya wanafunzi .

**Msamiati kuhusu mazingira ya shule**

**Kazi ya 2 :** ***Baada ya kusoma kifungu hiki cha habari, oanisha msamiati ulio katika sehemu A na maelezo yaliyotolewa katika sehemu B. Tumia mbinu ya fikili-jozi-changia. Majibu:***

1 (d), 2 (b), 3 (a), 4 (e), 5 (c), 6 (g), 7 (f), 8(h

**Sarufi: Matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya LI-YA**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi aongoze wanafunzi kutazama sentensi walizopewa na kuzungumzia mabadiliko yanayojitokeza kutoka sehemu A kwenda sehemu B. Kazi hii ifanyike katika makundi au katika jozi. Jibu:***

Majina ya ngeli ya **LI-YA** huchukua kiambishi awali LI- katika umoja, na katika wingi, majina ya ngeli ya LI-YA huchukuwa upatanisho wa kisarufi -YA.

**Kazi ya 4:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa wanafunzi . Mkufunzi achunguze kama wanafunzi wametilia maanani matumizi bora ya ngeli za majina.***

| Umoja | Uwingi |
|---|---|
| a. Jaribio hili linatatanisha. | 1. Majaribio haya yanatatanisha. |
| b. Swali hili ni gumu. | 2. Maswali haya ni magumu. |
| c. Jino hili limeota upya. | 3. Meno haya yameota upya. |
| d. Jembe langu lina makali. | 4. Majembe yetu yana makali. |
| e. Juma hili litamalizika kweli? | 5. Majuma haya yatamalizika kweli? |

**Matumizi ya lugha: Shughuli za wafanyakazi shuleni**

**Kazi ya 5:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kuwaongoza kuzungumzia viongozi wote wa shule na wajibu wao. Kila kundi liandike majibu yao kwenye flip chati na kuibandika kwenye ukuta wa darasa. Baada ya hapo, wanafunzi wote wasimame mbele ya kila flip chati na kulinganisha majibu yaliyotolewa. Majibu sahihi yakubaliwe na yale yasiyo sahihi yaondolewe. Mapendekezo ya majibu:***

- **Hedimasta**: Mwalimu mkuu wa kiume wa shule ya sekondari au ya msingi.

- **Hedimistresi**: Mwalimu mkuu wa kike wa shule ya sekondari au ya msingi.
- **Afisa wa taaluma**: Mwalimu anayeshughulikia masomo ya kila siku shuleni pamoja na utunzaji wa vyeti na alama za wanafunzi .
- **Mratibu wa nidhamu**: Hushughulikia mienendo na nidhamu ya wanafunzi .
- **Mhasibu**: Mtaalamu anayehusika na uwekaji hesabu za pesa.
- **Mkutubi:** Mtu anayefanya kazi ya kuhifadhi vitabu katika maktaba na kuviazima wasomaji.

**Kazi ya 6**: ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kuwaongoza kuhusisha maneno ya sehemu A na maana yake katika sehemu B. Majibu:***

1. e
2. a
3. c
4. d
5. b

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi awamotishe wanafunzi kuitambulisha shule waliyoisomea katika kidato cha tatu na kuisimulia hadharani. Hapa mkufunzi asahihishe matamshi ya wanafunzi na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanatumia msamiati unaofaa.***

**Kuandika**

**Kazi ya 8**: ***Katika makundi ya wanafunzi watatu, mkufunzi awaongoze kubuni mazungumzo kati ya Mkuu wa shule na wanafunzi wawili na kuyaigiza mbele ya darasa. Kila mwanafunzi awe na wajibu wake na kuushughulikia.***

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi na kuwaongoza kupanga ratiba yao kwa kutumia kielelezo cha jedwali kilichopo katika kitabu cha mwanafunzi kuhusu kazi hii. Baadaye, wanafunzi wawasilishe matokeo yao mbele ya darasa.***

# SOMO LA 2: USAFI SHULENI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutumia kwa ufasaha msamiati unaotumiwa katika mazingira ya usafi,
- Kueleza msamiati unaohusiana na vifaa vya shule,
- Kutumia ngeli ya LI-YA na vivumishi vya idadi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Mkufunzi atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufika kwenye malengo ya somo lake. Mkufunzi atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi ,
- Mwongozo wa mkufunzi,
- Vinasa sauti,
- Vitabu vya hadithi fupi, riwaya, shairi na tamthilia,
- Michoro ya kisanii,
- Kompyuta,
- Projekta ya kuonyesha picha kutoka mtandao ikiwa ipo,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Mkufunzi anaweza kutafuta zana nyingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo. Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake na kuwa na vifaa mbalimbali. Mkufunzi kwa ubunifu wake anaweza kuandaa vifaa vingine mwenyewe vya kumsaidia kufanikisha somo.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.

- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha huwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi :** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi . Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi awape wanafunzi muda wa kuchunguza na kujadili mchoro uliopo katika kitabu cha mwanafunzi . Kazi hii ifanyike katika makundi na kila kundi liwasilishe uchunguzi wao mbele ya hadhira. Mapendekezo ya majibu:***

- Kuna majengo matano ya shule,
- Kuna bendela ya taifa,
- Kuna wanafunzi (wasichana na wavulana,) wanaosimama katika mazingira ya shule.
- Kuna busitani nzuri.

**Kusoma na ufahamu: Usafi wa mazingila ya shule**

**Kazi ya 2:** ***Wanafunzi wawekwe katika makundi ya watatu watatu kisha watoe majibu ya maswali ya ufahamu waliyopewa. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Usafi wa shule ni njia ya kuendeleza afya kwa kuzuia mawasiliano ya binadamu na athari za taka.
2. Usafi ni jambo la kutilia maanani ili kujiepusha na magonjwa yanayotokana na uchafu.
3. Usafi shuleni unawahusu watu wote.
4. Wanafikiri kuwa usafi unahusu miili na sare tu wakisahau kuwa usafi huhusu kila kitu.
5. Wanafunzi wanaombwa kuvaa sare kwani zinawafanya waonekane maridadi.
6. Kujiepusha na magonjwa yanayotokana na wadudu wanaoweza kuishi, katika nguo chafu.
7. Kuwafukuza mbu wanaosababisha ugonjwa wa malaria.
8. Kutupia uchafu na takataka.
9. Katika bustani wanatumia jembe kwa kupalilia na panga kwa kukata nyasi.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu kwa kuchunguza maana ya msamiati husika. Mkufunzi awasisitizie kutumia msamiati huo katika sentensi zao sahihi. Majibu:***

1. Usafi= hali ya kutokuwa na uchafu.

2. Uchafu= kutokuwa na usafi.
3. Athari = matokeo au alama inayobakia baada ya mtu au kitu kufikwa na jambo fulani.
4. Maanani= mambo ya kuzingatia.
5. Bweni= chumba cha kulala wanafunzi .
6. Bwalo= chumba cha kulia chakula wanafunzi .
7. Mbu= mdudu anayeambukiza ugonjwa wa malaria.

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kuwaongoza kushirikiana katika kazi hii. Majibu:***

1. **Usafi** ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani shuleni.
2. Watu wachache wa shuleni wanafikiri kuwa usafi ni **kunawa** mikono, kuoga na kuvaa sare safi.
3. Sare humfanya mwanafunzi aonekane **maridadi** na apendeze.
4. Mavazi ni **hifadhi** ya staha ya utu wa mtu.
5. Usafi wa mwili unahusiana na kuoga, **kunyoa** nywele, kupiga pasi na kukata kucha.
6. Taka zote zinazotokana na vitu vyote vilivyotumiwa zinafaa kutupwa mahali panapofaa kama vile pipa la taka au **jalalani**.
7. Wanafunzi wana tabia ya **kunawa** mikono kwa maji na sabuni kabla na baada ya chakula.
8. Maji yote ya kunywa na ya matumizi mengine lazima yatoke kwenye vyanzo salama au **yachemshwe**.

**Sarufi: ngeli ya li – ya na vivumishi vya kumiliki**

**Kazi ya 5:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo na kuwaongoza wanafunzi kuchunguza na kueleza aina za maneno yaliyopigiwa mstari. Jibu lililopendekezwa:***

Maneno **langu**, **letu**, **lako**, **lenu** na **lao** ni vivumishi vya kumiliki katika ngeli ya LI-YA katika umoja.

**Kazi ya 6:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika jozi au makundi na kuwaongoza kuweka sentensi husika katika umoja au wingi.***

***Majibu:***

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **1.** Jiji letu linapata wageni kutoka Kigali. | Majiji yetu yanapata wageni kutoka Kigali. |
| **2.** Ua langu linapamba mazingira. | Maua yetu yanapamba mazingira. |
| **3.** Dirisha lao linafunguliwa ili hewa iingie. | Madirisha yao yanafunguliwa ili hewa iingie. |
| **4.** Sikio langu lina shida la kusikia. | Masikio yetu yana shida ya kusikia. |
| **5.** Gari lenu linatereza siku hii. | Magari yenu yanatereza siku hizi. |
| **6.** Jino langu linaniuma. | Meno yetu yanatuuma. |
| **7.** Gazeti letu lina habari nyingi. | Magazeti yetu yana habari nyingi. |
| **8.** Shamba lako limelimwa vizuri | Mashamba yenu yamelimwa vizuri |
| **9.** Dawati lenu limevunjika. | Madawati yenu yamevunjika. |
| **10.** Soko lao linajaa watu. | Masoko yao yanajaa watu. |

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi darasani na kutumia kona ya ujifunzaji ambayo ni nafasi iliyotengwa darasani kwa namna ya kuvutia ufanisi. Ubao au flip chati ibandikwe kwenye ukuta na kila mwanafunzi aweze kuandika jibu lake, wakishamaliza mkufunzi awasaidie kuweka vizuri majibu yaliyo sawa akiwashirikisha wanafunzi wote.***

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8**: ***Mkufunzi atumie njia ya meza ya majadiliano. Mbinu hii ni ushirikiano katika ujifunzaji ambapo swali linaulizwa na mkufunzi kwa kundi la wanafunzi , kila mwanafunzi katika kundi akaandika jibu lake kwenye karatasi na kupeleka kwenye kundi jingine.Wanafunzi wanashiriki katika kundi hilo***

***na kuchunguza jibu linalofaa kwa kuwasilisha darasani. Kila kundi litachangia na kuwasilisha majibu darasani. Majadiliano yatafanywa baada ya kuwasilisha.***

**Kuandika**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi atumie njia ya utafiti kwa kuwaweka wanafunzi katika makundi. Wao wenyewe wafanye utafiti kwa kuwauliza watu wenye uzoefu hapo shuleni au nyumbani kisha wawasilishe matokeo ya utafiti wao darasani kipindi kijacho. Mkufunzi asahihishe makosa ya kiotografia, kisarufi na kisintaksia.***

## SOMO LA 3 : VIONGOZI WETU SHULENI

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kutumia kwa ufasaha msamiati unaoendana na viongozi wa shule,
- Kuelezea viongozi washule na majukumu yao shuleni,
- Kutunga sentensi kwa kuzingatia matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya li-ya.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Mkufunzi atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufika kwenye malengo ya somo lake. Mkufunzi atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi ,
- Mwongozo wa mkufunzi,
- Vinasa sauti,
- Vitabu vya hadithi fupi, riwaya, shairi na tamthilia,
- Michoro ya kisanii,
- Kompyuta,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Projekta ya kuonyesha picha kutoka mtandao ikiwa ipo,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Mkufunzi anaweza kutafuta zana nyingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo. Vifaa hivi viandaliwe

kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake. Mkufunzi, kwa ubunifu wake, anaweza kuandaa vifaa vingine vya kumsaidia kufanikisha somo.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hii ni mbinu ambayo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv. Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majidiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi aombe wanafunzi kutazama mchoro kitabuni. Kwa kutumia mbinu ya fikiri-jozi-changia, mkufunzi aongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu wanachokiona kwenye mchoro huo. Mapendekezo ya majibu:***

- Kuna wanafunzi katika sare zao,
- Viongozi watatu mbele ya wanafunzi ,
- Madarasa,
- Bustani nzuri.

**Kusoma na ufahamu: Viongozi wa shule na majibu wao**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya vitabu na kuwaongoza kujibu maswali ya ufahamu. Mwanzoni, wanafunzi wasome kimya na kuhakikisha kwamba wanayelewa maudhui ya kifungu cha habari. Mwishowe, wanafunzi wapewe fursa ya kusoma kwa sauti inayosikika ili mkufunzi asahihishe makosa ya tahajia yanayoweza kujitokeza.***

***Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Anasoma katika shule ya sekondari ya Gikondo.
2. Anasoma kidato cha nne.
3. Maktaba humsaidia mwanafunzi katika kufanya utafiti wake, na kujinufaisha na uwezo na ujuzi huo katika maisha yake ya kila siku.
4. Kwizera anayelewa vizuri masomo yake kwa sababu anayelewa Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Historia na mengine. Hiki ni kitu kisicho cha kawaida .
5. Mkuu wa shule, mwalimu wa mitaala, mhasibu wa shule, mwalimu wa nidhamu, mwalimu mshauri wa wasichana, mwalimu mshauri wa wavulana, viranja wa shule.
6. Kazi ya mhasibu ni kukusanya ada za wanafunzi .
7. Mwishoni mwa kila muhula wanafunzi hufanya mtihani.
8. Kiranja huwakilisha wanafunzi wenzake katika mikutano mingi ya shule.
9. Jina la mkuu wa shule halikutajwa katika kifungu cha habari. Kwa ujumla ana majukumu ya kuongoza shule yaani utekelezaji wa kazi yote ya uongozi wa shule.
10. Walimu wa zamu huingia bwaloni kuchunga nidhamu ya wanafunzi .

**Msamiati kuhusu mazingira ya shule**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi atumie flip chati inayobandikwa kwenye ukuta darasani na kuandika maneno au msamiati ambao wanafunzi watatafutia maelezo. Wanafunzi waandike maelezo ya msamiati huo kwenye karatasi na baada ya muda uliotolewa, mkufunzi awaongoze kuhusisha maelezo yao na msamiati ulioandikwa kwenye flip chati. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. d
2. a
3. b
4. c
5. e

**SARUFI: Matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya li-ya**

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi awaongoze kuzungumzia mabadiliko yanayojitokeza kutoka sehemu A kwenda sehemu B. Majibu yaliyopendekezwa:***

Kinachoonekana katika sentensi hizi ni kwamba kuna mabadiliko ya upatanisho wa kisarufi katika umoja na wingi wa majina ya ngeli hiyo. Mabadiliko haya pia yanajitokeza kwenye vivumishi vya kuonyesha vinavyofuata majina ya ngeli hiyo.

**Kazi ya 5:** ***Wanafunzi wafanye kazi hii katika jozi na mkufunzi awaongoze kusahihisha maswali haya ubaoni wakiyaweka katika umoja au wingi. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Mazoezi haya hayaeleweki.

b. Mashamba ya mjomba ni mapya.

c. Mayai yaliyoharibika hayafai kwa afya ya mwanadamu.

d. Magari yaliyoharibika hayapendezi.

e. Tope limechafua nguo yangu.

f. Majeshi yamewashinda maadui.

g. Majuma ya kazi yamemalizika.

h. Gurudumu la gari linaviringika kasi.

i. Mahekalu yamejengwa vizuri.

j. Jamvi lililiwa na panya.

**Kazi 6:** ***Mkufunzi abandike flip chati mbili kwenye ukuta wa darasa. Kwenye flip chati ya kwanza kuandikwe maneno na ya pili kuandikwe maelezo yake na kila mwanafunzi aunganishe maneno hayo na maelezo yake. Majibu yaliyopendekezwa:***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mhasibu wa shule | e) hukagua kama wanafunzi wamelipa ada ya shule. |
| 2. Shule yetu ina | c) wavulana na wasichana. |
| 3. Mwishoni mwa kila muhula sisi | b) hufanya mitihani. |
| 4. Karani wa shule | a) Hutunza barua ziingiazo shuleni pamoja na kumbukumbu nyingine zihusuzo shule. |
| 5. Mwalimu mshauri wa wavulana | d) huchunguza nidhamu ya wavulana. |

**Matumizi ya lugha: Vyeo vya viongozi shuleni**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi abandike flip chati mbili kwenye ukuta wa darasa. Kwenye flip chati ya kwanza kuandikwe maneno na ya pili kuandikwe maelezo yake na kila mwanafunzi aunganishe maneno hayo na maelezo yake. Majibu:***

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| 1. Kiongozi wa darasa | c) Kiongozi wa wanafunzi darasani. |
| 2. Naibu mkuu wa shule | a) Makamu wa mkuu wa shule. |
| 3. Mwalimu wa darasa | b) Mwalimu anayehusika na shughuli za kila siku kuhusu darasa alilopewa. |
| 4. Mwalimu wa chakula | e) Mwalimu anayehusika na lishe ya wanafunzi shuleni. |
| 5. Mhasibu | d) Mtaalamu wa hesabu za fedha. |

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8**: ***Kinacholengwa hapa ni kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaambia wabuni mazungumzo yao binafsi. Katika jozi kila mwanafunzi azungumzie mwenzake kuhusu shule alikosomea kidato cha tatu; kisha kila kundi lipewe fursa ya kuzumgumza mbele ya darasa lote.***

***Hapa mkufunzi ahakikishe ikiwa wanafunzi wana matamshi bora na kufuatilia kanuni za kisarufi.***

**Kuandika**

**Kazi ya 9 :** ***Katika kujibu swali hili, mkufunzi atumie mbinu ya fikiri- jozi- changia. Kila mwanafunzi apewe fursa ya kuandika kuhusu umuhimu wa viongozi baadaye ajadili na mwenzake kuhusu swali na hatimaye watoe jibu linalotakiwa kwa kuliandika ubaoni. Kwa kuhitimisha kazi hii, mkufunzi atoe msisitizo kuhusu kazi ya wanafunzi akisisitizia kuwa ni muhimu sana kuwa na viongozi.***

## SOMO LA 4: RATIBA YA WIKI YA MWANAFUNZI

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kutumia kwa ufasaha msamiati unaotumiwa katika shughuli za kila siku za mwanafunzi,
- Kuelezea msamiati unaohusiana na vifaa vya shule,
- Kutumia vivumishi vya kuonyesha vya ngeli ya li-ya.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Mkufunzi atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufika kwenye malengo ya somo lake. Mkufunzi atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi ,
- Mwongozo wa mkufunzi,
- Vinasa sauti,
- Vitabu vya hadithi fupi, riwaya, shairi na tamthilia,
- Michoro ya kisanii,
- Kompyuta,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Projekta ya kuonyesha picha kutoka mtandao ikiwa ipo,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Mkufunzi anaweza kutafuta zana nyingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo. Vifaa hivi viandaliwe

kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake ili wawe na vifaa mbalimbali. Mkufunzi, kwa ubunifu wake, anaweza kuandaa vifaa vingine vya kumsaidia kufanikisha somo hilo.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hii ni mbinu ambayo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga, kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala ya darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv. Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi . Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Majibu yanayotarajiwa kwa kazi zinazofanywa na wahusika wapatikanao katika mchoro huu ni hizi zifuatazo:***

- Ninaona wanafunzi wanaokaa kwenye madawati yao na kujifunza masomo ya mwalimu. (Kazi hii ina umuhimu kwa kupata uwezo, ujuzi, maarifa, maadili na mwenendo mwema na kusaidia kujenga utu na kumfanya mtu kamili katika jamii.)
- Ninaona pia wanafunzi ambao wanafanya usafi wa choo. Hii husaidia watu kutoambukizana magonjwa yatokanayo na uchafu.
- Ninaona tena wanafunzi wanaocheza mpira. Hawa wanafanya mazoezi ya kimwili ambayo husaidia mtu kuwa na afya nzuri.

**Kusoma na ufahamu: Ratiba ya shughuli za kila siku katika shule ya Gasozi**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awape wanafunzi fursa ya kusoma kifungu cha habari. Kazi hii ifanyike katika makundi darasani na baadaye mkufunzi awaongoze kutoa majibu sahihi. Majibu:***

1. Gasimba anasoma katika shule ya Gasozi.
2. Gasimba yupo katika kidato cha kwanza.
3. Hupiga meno yake mswaki, huchana nywele zake na kuvaa sare yake.
4. Mamake Gasimba huamka mapema zaidi.
5. Gasimba hufika shuleni saa kumi na mbili na nusu akaingia darasani na kuanza kusoma.
6. Siku ya Alhamisi jioni, Gasimba hufanya mazoezi ya kuogelea katika bwawa la kuogelea nyumbani kwao na Ijumaa jioni, wanafunzi hushiriki katika mjadala kuhusu mada ambazo walimu wao huwa wamewachagulia.
7. Jumamosi, Gasimba humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani.
8. Jumapili, Gasimba huendelea na mapumziko kama kawaida.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi, kisha awaongoze katika sentensi fasaha wakitumia maneno waliyopewa. Majibu:***

**Ratiba**: Ratiba huwaongoza wanafunzi kutumia muda wao vizuri wakiwa shuleni.

**Kuogelea**: Kagina huenda kuogelea katika ziwa la Kivu kila Jumapili.

**Mjadala**: Kazi ya mjadala husaidia wanafunzi kukuza stadi zao za kuzungumza.

**Huchana nywele**: Murorunkwere huchana nywele zake kabla ya kuenda shuleni.

**Mapumziko**: Wakati wa mapumziko wanafunzi hupata fursa ya kuwasiliana na kujuliana hali.

**Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya kuonyesha vya ngeli ya li-ya**

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kusoma kazi husika na kuzungumzia mabadiliko yanayojitokeza kutoka sehemu A kwenda sehemu B. Kazi hii ifanyike katika makundi.*** **Jibu lililopendekezwa:**

Kinachoonekana katika sentensi hizi ni kwamba, majina ya ngeli ya LI-YA huchukua kiambishi awali LI- katika sentensi za umoja na kiambishi YA- katika wingi. Pia, vivumishi navyo hubadilika vile vile.

**Matumizi ya lugha: Shughuli za kila siku za mwanafunzi**

**Kazi ya 5:** ***Husisha sentensi kutoka sehemu A kwenda sehemu B na kuunda sentensi kamili. Kazi hii ifanyike katika jozi. Majibu yaliyopendekezwa:*** 1(b) 2 (a) 3 (e) 4 (d) 5 (d)

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 6**: ***Mkufunzi aombe wanafunzi kufikiria kuhusu shughuli wanazozifanya shuleni kisha wapewe nafasi ya kuzisimulia hadharani. Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kumjengea kila mwanafunzi uwezo wa kujitegemea.***

**Kuandika**

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii iwe ya nyumbani. Mkufunzi aombe wanafunzi kuandika kwa ufupi kuhusu maendeleo ya shule yao na kumkabidhi kazi hizo kipindi kijacho. Mkufunzi asahihishe makosa ya kiotografia, kisarufi na kisintaksia.***

## 1.6. Muhtasari wa mada ya kwanza

‘**Matumizi ya Kiswahili shuleni’** ni mada ya kwanza katika kitabu cha mwanafunzi . Imejigawa katika masomo manne ambayo ni yafuatayo:

1. **Taratibu za shuleni**: Sehemu hii inazungumzia kuhusu msimiati wa mazingira ya shule na kazi zinazofanyika huko.

2. **Usafi shuleni**: Somo hili limejikita katika kueleza namna ya kuhifadhi mazingira ya shule na kutunza usafi wake.
3. **Viongozi wetu shuleni**: Wafanyakazi katika mazingira ya shule na majukumu yao yameelezwa kinagaubaga.
4. **Ratiba ya wiki ya mwanafunzi** : Somo hili linayelezea shughuli zote zifanyikazo shuleni kulingana na ratiba wanayoitumia.

Ikumbukwe kuwa kila somo limezingatia sehemu kuu sita ambazo ni:

i. Kusoma na ufahamu

ii. Matumizi ya msamiati maalum

iii. Sarufi

iv. Matumizi ya lugha

v. Kusikiliza na Kuzungumza

vi. Kuandika

## 1.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana haki au idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao kwa ajili ya kuimarisha shauku yao ya kuitumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

## 1.8. Tathmini ya mada ya kwanza

***Wanafunzi wajibu maswali haya kibinafsi. Mkufunzi aongoze wanafunzi kujibu maswali haya na kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anatoa majibu sahihi kwa kila swali. Mkufunzi asahihishe kazi ya kila mwanafunzi kisha wanafunzi wote washirikiane kwa kujibu maswali hayo ubaoni. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. a) Viti na meza

   b) Madarasa na vyumba vyake

   c) Ofisi za shule

   d) Maabara za shule

e) viwanja vya michezo

2. a) Shughuli za masomo ya kila siku na michezo mbalimbali.

   b) Shughuli za kufanya utafiti katika maabara na maktabani.

   c) Kufanya usafi shuleni.

3. a) Mkuu wa shule = Kiongozi wa shule anayeshughulika na utawala wa kila siku shuleni na mawasiliano ya nje ya shule.

   b) Naibu mkuu wa shule = Humwakilisha mkuu wa shule kama hayupo pamoja na kutunza kumbukumbuza kila siku za wanafunzi .

   c) Mwalimu wa nidhamu = Hushughulika na maadili na mwenendo mwema wa wanafunzi shuleni.

   d) Mhasibu: Hukusanya karo za wanafunzi .

4. Tunga sentensi nne kwa kutumia ngeli ya li-ya katika umoja na uwingi

Hizi ni baadhi ya sentensi zilizotungwa kwa kutumia ngeli ya LI-YA katika umoja na wingi. Mwalimu aongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi kufuatana na mifano ya hapa chini.

**Majibu**

| **Umoja** | **Wingi** |
| --- | --- |
| a) Bega hili linabeba nyota ya kijeshi. | Mabega haya yanabeba nyota za kijeshi. |
| b) Gari hili ni jipya. | Magari haya ni mapya. |
| c) Jengo hili ni la hospitali. | Majengo haya niya hospitali |
| d ) Pazia hili ni Safi | Mapazia haya ni safi. |

5. Eleza nafasi ya kila mwanafunzi katika harakati za kuzuia ueneaji wa magonjwa shuleni. Mkufunzi awaelekeze wanafunzi kujadili nafasi zao katika harakati za kuzuia ueneaji wa magonjwa shuleni. Kazi hii ifanywe kwa mjadala.

## 1.9. Kazi za ziada

### 1.9.1. Kazi za urekebishaji

a. Taja jina la mbu anayeambukiza malaria.

b. Orodhesha angalau vifaa vitano unavyotumia kwa kusafisha mazingira ya shule.

c. Eleza jinsi ya kusafisha maji ya kunywa.

**Majibu:**

a. Mbu huyu huitwa anofelisi.

b. Sabuni, deki, ndoo, beseni, ufagio.

c. Kuchemsha maji na kunyunyizia dawa ya kuua vijidudu.

### 1.9.2. Kazi jumuishi

Tunga sentensi sahihi tano kwa kutumia ngeli ya LI-YA inayohusu maneno yasiyoweza kuwa katika umoja.

**Majibu:**

a. Maziwa yaliyoganda yamenywewa.

b. Mate yalimdondoka alipoona chakula kitamu.

c. Mazishi ya babu yake yalimhuzunisha.

d. Manukato haya yananukia vizuri sana.

e. Maji yakimwagika hayazoleki.

### 1.9.3. Kazi za nyongeza

Shauri wajasiriamali wa viwanda nchini Rwanda jinsi wanavyoweza kuhifadhi mazingira.

Kazi hii ifanyike katika makundi na mkufunzi awaongoze wanafunzi kufanya utafiti kuhusu namna ya kuhifadhi mazingira. Kila kundi limkabidhi mkufunzi matokeo yake ayasahihishe kwa kuzingatia makosa ya kisarufi, kiotografia na kisintaksia.

# MADA YA 2:

## MSAMIATI KUHUSU MAZINGIRA YA NYUMBANI

### 2. 1. Uwezo mahususi wa mada

Kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha na kuandika matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya nyumbani.

### 2.2. Ujuzi wa awali

Kupitia masomo waliyofundishwa katika kidato cha kwanza, mada kuu ya tatu ilizungumzia masomo tofauti kama vile: msamiati kuhusu vifaa vya nyumbani, sehemu kuu za nyumba, uhusiano wa kifamilia, na mifugo wanaopatikana nyumbani. Wanafunzi hawa wana ujuzi wa jumla kuhusu mazingira ya nyumbani.

### 2.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, kuandika, kuzungumza, sarufi, katika mazoezi mbalimbali; mkufunzi anawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kuingiza masuala mtambuka yafuatayo: elimu kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu uzalishaji mali, mafunzo kuhusu amani na maendeleo, elimu jumuishi, mazingira na maendeleo endelevu na mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari.

### 2.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 2.5. Orodha ya masomo

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| Mazingira ya nyumbani | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja sehemu za nyumba.<br>**Stadi:** Kuchagua msamiati unaofaa katika kuelezea mazingira ya nyumbani .<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kushirikiana katika kazi za nyumbani. | 4 |
| Msamiati kuhusu watu wanaopatikana nyumbani | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja watu wanaopatikana katika familia na uhusiano kati yao.<br>**Stadi**: Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya watu wanawopatikana nyumbani.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuwaheshimu watu wanaopatikana nyumbani kufuatana na marika yao. | 4 |
| Uhusiano wa familia | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja majina ya uhusiano wa familia.<br>**Stadi**: Kutunga sentensi kuhusu uhusiano wa familia.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuwaheshimu watu kufuatana na marika yao. | 4 |
| Vifaa vya nyumbani na usafi wake | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja majina ya vifaa vya nyumbani na vifaa vya usafi nyumbani.<br>**Stadi:** Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya vifaa vya nyumbani na vifaa vya usafi.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuimarisha usafi katika mazingira ya nyumbani na kutumia vizuri vifaa vya nyumbani. | 4 |
| Msamiati kuhusu mifugo | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja majina ya mifugo wanaopatikana nyumbani.<br>**Stadi**: Kutunga sentensi kwa kuzingatia matumizi sahihi ya ngeli ya LI -YA.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kushirikiana nyumbani katika ufugaji. | 4 |
| **Tathmini ya mada** | | **2** |
| **Vipindi vyote vya mada ya pili** | | **22** |

## SOMO LA 5: MAZINGIRA YA NYUMBANI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza sehemu kuu za nyumba.
- Kutaja vifaa vinavyotumiwa katika ujenzi wa nyumba.
- Kutumia ngeli ya LI-YA na mabadiliko yanayojitokeza.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya vifaa vinavyotumiwa katika ujenzi wa nyumba.

Mukufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hii ni mbinu ambayo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa

kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv. Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo :**

1. Watu wanaopatikana nyumbani ni wazazi (baba na mama) pamoja na watoto.
2. Sehemu hizi ni sebule, vyumba vya kulala, chumba cha wageni, n.k.
3. Vifaa ni k. v. kabati, redio, meza, kikombe, stuli, n.k. Mifugo ni k.v. ng’ombe, mbuzi, kuku, kondoo, n. k.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi awape wanafunzi fursa ya kueleza kinachoonekana kwenye mchoro na kuwaongoza kujibu maswali yote yaliyoulizwa kuhusu mchoro huo kupitia mbinu ya bunguabongo. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Ninaona nyumba nzuri ya kisasa iliyojengwa kwa matofali, nyuma yake kuna mifugo kama ng’ombe, mbuzi na kuku. Nyumba hii pia inazungukwa na bustani.
2. Uhusiano upo pale ambapo tunaona nyumba ya kuishi yenye bustani nzuri na mifugo wa nyumbani.

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi watatu watatu kufuatana na idadi ya vitabu vya kusoma vilivyopo. Mkufunzi awaongoze kufanya kazi hii na kuwasaidia wanafunzi wanapokosea. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Majina ya watu wote wanaotajwa katika kifungu hiki ni: Rurangwa, Kalisa, Gakuba, bibi yake na watoto wawili.
2. Familia ya Gakuba ina watu wanne. Gakuba, bibi yake na watoto wawili.
3. Kwa kujenga nyumba yao, walitumia vifaa kama vile: Mchanga, saruji, vyuma, nondo, milango, madirisha, mawe, matofali na mabati. Vifaa vyote vinapatikana nchini Rwanda.
4. Nyumba hii ilijengwa na baba na mama yaani Gakuba na mke wake kwa ushirikiano. Wao walitumia fedha za mkopo kutoka benki.
5. Ndiyo. Mtu mwenye uwezo mdogo wa kiuchumi anaweza kuishi katika nyumba ya kisasa kwa kutumia mkopo wa fedha za benki baada ya makubaliano kama alivyofanya bwana Gakuba.
6. Tunatakiwa kuheshimu mazingira wakati tunapojenga nyumba kwa sababu tunapoyaharibu, tunaharibu maisha yetu binafsi. Bila mazingira hakuna maisha.
7. Kama mwanafunzi wa kidato cha kwanza msaada wangu kwa kuhifadhi mazingira ni:

- Kuelewa umuhimu wa mazingira kwa maisha ya binadamu,
- Kuelezea watu wote sana sana ndugu na marafiki zangu kuhusu ubaya wa kuharibu mazingira,
- Kuhifadhi mazingira ya nyumbani na ya shuleni kama vile: Kupanda miti, kuwa na bustani, kuchimba mifereji ya kuelekeza maji kwa kujilinda mmonyoko wa ardhi, n.k.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Wanafunzi, katika jozi, waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii ya kutumia maneno yaliyotumiwa katika kifungu. Itawabidi kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu.***

1. **Bustani**: Mji wa Kigali una **bustani** ya kupendeza sana.
2. **Bumbuazi**: Mukankusi amepigwa na **bumbuazi** alipopewa tuzo la mwandishi bora wa Kiswahili nchini Rwanda.
3. **Mkopo**: Watu wengi hutajirika kutokana na **mkopo** wa benki.
4. **Kuhifadhi mazingira**: Serikali ya Rwanda inawahimiza

wananchi wote **kuhifadhi mazingira** kama njia moja ya kupata hewa nzuri.

5. **Shirika**: **Shirika** liitwalo “ Mpore kibondo” linatetea haki za Watoto.
6. **Kupumua**: Tukihifadhi mazingira, tutaweza **kupumua** hewa nzuri.
7. **Kutetea**: Shirika “Haguruka” linalenga kuwatetea watu mahakamani.
8. **Klabu / kilabu**: Kila darasa lina **klabu** tofauti kama vile: **klabu** ya lugha, **klabu** ya mazingira, n.k.

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kusoma vizuri kifungu na kuelezeana kati yao maana ya maneno waliyopewa wakitumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu pale inapohitajika. Majibu yaliyopendekezwa:***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1 | d |
| 2 | c |
| 3 | e |
| 4 | a |
| 5 | f |
| 6 | b |

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya LI-YA**

**Kazi ya 5:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kuchunguza sentensi na kuwahimiza kuandika viambishi nafsi vinavyopatikana katika vitenzi hivyo. Majibu yanayopendekezwa:***

- Viambishi nafsi vinavyopatikana katika vitenzi vyote ni **LI-** na **Ya-**. Kiambishi **LI-** kimetumiwa katika umoja na **YA-** katika wingi.
- Maneno haya yote, wingi wake huanza na “**ma-.**”

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 6:** ***Mkufunzi, awaongoze wanafunzi kuandika sentensi katika wingi na kueleza kilichogunduliwa ndani ya sentensi zilizoshughulikiwa. Hapa mkufunzi atumie makundi na kisha wanafunzi wawasilishe majibu ya maswali mbele ya darasa. Majibu yaliyopendekezwa:***

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Kabati limeanguka vibaya. | Makabati yameanguka vibaya. |
| Koti linashonwa na Kalisa. | Makoti yanashonwa na Kalisa. |
| Bega langu limevunjika. | Mabega yetu yamevunjika. |
| Goti lake linamuumiza. | Magoti yao yanawaumiza. |
| Panga linakata nyasi. | Mapanga yanakata nyasi. |
| Janga la njaa lilikumba nchi yetu mwaka 1930. | Majanga ya njaa yalikumba nchi zetu mwaka 1930. |
| Jangwa, barani Afrika, linahamisha watu. | Majangwa, barani Afrika, yanahamisha watu. |
| Jina lake linanifurahisha. | Majina yao yanatufurahisha. |
| Jibu lililotolewa lina makosa. | Majibu yaliyotolewa yana makosa. |
| Jembe linatumiwa kwa kulima. | Majembe yanatumiwa kwa kulima. |

**Tanbihi**: Kutokana na sentensi za hapo juu, kinachoonekana ni kwamba sentensi za umoja, majina huanzwa na kiambishi nafsi "**li**" na majina ya sentensi za wingi huanzwa na **"ma"** ili kuleta upatanisho wa kisarufi katika vitenzi**.**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kuandika sentensi zifuatazo katika umoja au wingi. Mkufunzi atumie makundi, kisha wanafunzi wawasilishe majibu yao mbele ya darasa. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Sisi tuna malengo ya kupambana na majangwa.
2. Ninyi mtaondoa majani makavu hayo.
3. Jani lilikauka.
4. Mashavu yanatuuma.
5. Vijana warefu walibeba makasha kwenye mabega.
6. Madebe hayo yanavuja kwa sababu yametoboka.
7. Mtoto mmoja alilazwa hospitalini kwa sababu ya tatizo la pafu.
8. Daftari linapaswa kuhifadhiwa vizuri.
9. Matarumbeta yalitumiwa wakati wa burudani.
10. Mashirika ya reli yaliagiza magarimoshi makubwa.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8**: ***Mkufunzi amwelekeze kila mwanafunzi kusimulia mbele ya darasa muhtasari wa kifungu "Makao ya Gakuba" kwa maneno yake. Hii lazima iwe kazi ya kibinafsi.***

**Kuandika.**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi aombe kila mwanafunzi kutunga kifungu kuhusu ujenzi wa nyumba ya wazazi wake kwa kuandika misitari 12.***

## SOMO LA 6: MSAMIATI KUHUSU WATU WANAOPATIKANA NYUMBANI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza na kutaja watu wanaopatikana nyumbani,
- Kutumia ngeli ya LI-YA na vivumishi vya idadi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Mkufunzi atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufika kwenye malengo ya somo lake. Mkufunzi atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Magazeti mbalimbali,
- Projekta,
- Kompyuta,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya vifaa tofauti.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa Mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

Mkufunzi anaweza kutafuta zana nyingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo. Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake ili kuwa na vifaa mbalimbali. Mkufunzi kwa ubunifu wake anaweza kuandaa vifaa vingine mwenyewe vya kumsaidia kufanikisha somo hilo.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hii ni mbinu ambayo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv. Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi kulingana na idadi ya vitabu vilivyoko. Mkufunzi awaombe wanafunzi wafungue kwenye ukurasa husika kisha awaulize wanafunzi maswali kuhusu michoro wanayoitazama. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Ninaona michoro minne kitabuni,
- Michoro miwili ya kwanza inaonyesha mwanamume na mwanamke wake,
- Michoro miwili ya mwisho inaonyesha familia ya mwanamke na mwanamume wake pamoja na mtoto mmoja kwa kila familia.

**Kusoma na ufahamu: Watu wa nyumbani**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kusoma kimya kifungu cha habari kuhusu "Watu wa nyumbani" huku wakiandika msamiati mpya wanaouona na kutazama michoro iliyomo.***

***Mkufunzi aandike kichwa cha somo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika.***

***Hatimaye mkufunzi awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichokisoma kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya na kuelewa, mkufunzi awaombe wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa sauti inayosikika kifungu kilichopo. Mkufunzi awaongoze wanafunzi kueleza maana ya maneno mapya yaliyomo kifunguni. Halafu wanafunzi wafanye kazi zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi na mkufunzi atoe msaada panapohitajika. Mkufunzi, pia, asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze kusahihisha ubaoni. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Familia ni jamaa ya watu wanaoishi pamoja yenye baba, mama na watoto.
2. Kwa kawaida familia inajengwa na wazazi pamoja na Watoto.
3. Katika utamaduni wetu kama Wanyarwanda, baba na mama wanashirikiana katika maisha ya kila siku ya familia yao kama vile:

- Wanapendana kati yao,
- Wanasaidiana katika maendeleo ya familia,
- Wanalea watoto wao pamoja,
- Katika kuchukua uamuzi wowote nyumbani, wanashirikiana,

- Wanasaidiana katika kazi za nyumbani.

4. Mchango wa watoto kwa wazazi wao ni kama vile:

   Kuheshimu wazazi wao, kutoa mchango mwafaka kwa maendeleo ya familia yao, kusaidia wazazi wao katika kazi tofauti. Wazazi wanapokuwa wazee, ni majukumu ya watoto kutimiza mahitaji ya wazazi wao.

5. Mila na desturi ambazo wazazi hufundisha watoto wao ni: uzalendo, kuepuka ukatili, kuepuka uongo, kuepuka uovu, kuepuka ulevi, kuepuka uzembe, kupiga marufuku itikadi ya mauaji ya kimbari, kuheshimu watu wote, n.k.

**Msamiati kuhusu watu wa nyumbani**

**Kazi ya 3**: ***Mkufunzi apange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu kwa kila kundi na kuwaomba kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu kwa kueleza maneno hayo na kuyatumia katika sentensi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. **Majukumu**: wajibu na shughuli za mtu.

   **Mfano**: Kila Mnyarwanda ana **majukumu** ya kupiga marufuku itikadi ya mauaji ya kimbari ili yasirudie tena.

2. **Ushirikiano**: Hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli.

   **Mfano:** Wanafunzi wanatumia **ushirikiano** katika kazi zao za makundi.

3. **Usalama:** Hali ya kutokuwepo hatari au fujo.

   **Mfano: Je**shi la serikali ya Rwanda huitwa Afrika kote katika shughuli za kulinda **usalama** wa raia.

4. **Uzalendo:** Hali au fikira ya mtu kuwa tayari kufa kwa ajili ya uhuru na usalama wa nchi yake.

   **Mfano:** Kila mwanchi anatakiwa kuwa na **uzalendo** ili nchi yetu iwe na amani.

5. **Mienendo:** Matendo ya mtu yanayojirudiarudia ama tabia**.**

   **Mfano:** Mwanafunzi anayetakiwa ni yule mwenye **mienendo** mizuri popote alipo.

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aombe kila mwanafunzi kuoanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B baada ya kusoma kifungu cha habari. Kazi hii ifanyike katika jozi au katika makundi ya wanafunzi zaidi ya jozi.***

| A | B |
|---|---|
| 1 | b |
| 2 | a |
| 3 | e |
| 4 | c |
| 5 | d |

**Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya idadi katika ngeli ya LI-YA**

**Kazi ya 5:** ***Hapa mkufunzi atumie mbinu ya " fikiri- jozi-changia" kuhusu sentensi hizi tano. Yeye achunguze na kueleza muundo wa vivumishi vilivyotumiwa.***

1. Jibu moja limepatikana.
2. Mawe sita yameanguka chini.
3. Matunda saba yameiva.
4. Madarasa tisa yanasafishwa.
5. Makoti kumi yatashonwa.

Muundo wa vivumishi vilivyotumiwa ni huu: Vivumishi vya idadi tulivyoviona hapo juu, tarakimu **moja**, **sita**, **saba**, **tisa** na **kumi** havichukui kiambishi **ma**- katika wingi. Vivumishi hivi hubaki vile vilivyo yaani **moja**, **sita**, **saba**, **tisa** na **kumi**.

**Kazi ya 6:** ***Kuandika sentensi kwa kutumia vuvumishi vilivyomo ndani ya mabano. Mkufunzi hapa atatumia makundi ya wanafunzi.***

1. Mawe **matatu** yamewekwa kando ya barabara.
2. Madirisha **matano** yamefunguliwa.
3. Meno **mawili** yameng'oka.
4. Matunda **manane** yameiva.
5. Makundi **manne** ya wanafunzi yameshiriki vilivyo.
6. Madarasa **matatu** yamejengwa.
7. Taja mambo **matatu** yanayozingatiwa katika kazi ya fasihi.
8. Makoti **matano** yameuzwa na mfanyabiashara huyu.

**Kazi ya 7**: ***Katika makundi yale chunguza mifano mingine ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri ya ngeli ya "li-ya", kisha utunge sentensi zenye vivumshi hivyo. Majibu yaliyopendekezwa ni haya yafuatayo:***

1. Macho **machache** yanatazama majigambo ya watoto.
2. Katika kongamano la Kiswahili mambo **mengi** ya kuendeleza lugha hiyo yaligusiwa.
3. Makundi **kadhaa** ya wanafunzi yanawatembelea wagonjwa hospitalini.
4. Gari langu linateleza sana kwa sababu ya maji **tele** yanayojaa barabarani.
5. Mawese **kidogo** yananunuliwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 8.** ***Kila mwanafunzi afanye kazi hii kwa kukamilisha tungo zifuatazo akitumia vivumishi vya idadi toka moja hadi arubaini (tarakimu ziandikwe kwa maneno).***

1. Kanuni za Mungu ni kumi.
2. Mwaka una miezi kumi na miwili.
3. Ni rahisi kujua kwamba wiki moja ina siku saba.
4. Watu wa zamani walipika kwa kuweka chungu juu ya mafiga matatu.
5. Wanyarwanda huwapa majina watoto wao kwenye siku ya nane.
6. Nchi ya Rwanda ina majimbo/mikoa minne na mji wa Kigali.
7. Nchi yetu inapakana na nchi nne.
8. Dunia ina mabara matano.
9. Rwanda ina milima ya volkano mitano.
10. Katika mchezo wa soka, timu moja huwa na wachezaji kumi na wawili uwanjani.
11. Siku moja ina saa ishirini na nne.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika jozi, kisha awaambie kusoma kifungu cha habari husika, baadaye watoe muhtasari. Hapa, mkufunzi ahakikishe ikiwa wanafunzi wana matamshi bora na kusahihisha pale panapohitajika.***

**Kazi ya 10:** ***Kila mwanafunzi, kwa njia ya mazungumzo , aeleze mwenzake ushirikiano uliopo nyumbani kwao kati ya baba, mama na watoto.***

**Mfano:** Nyumbani kwetu, kazi ya mama na baba ya kila siku ni uchoraji. Wanafanyia kazi hiyo mjini Rubavu. Mama anachora na baba humsaidia kupaka rangi michoro hiyo nasi watoto kwa upande wetu tunafanya kazi ya kuiuza michoro hiyo dukani na kushughulikia kazi za nyumbani pindi tunapotoka shuleni.

**Kuandika:**

**Kazi ya 11:** ***Mkufunzi aombe wanafunzi kubuni mazungumzo ya watu nyumbani wakishirikiana katika kazi fulani. Kazi hii iwe ya nyumbani na wanafunzi wamkabidhi mkufunzi majibu kipindi kijacho.***

## SOMO LA 7: UHUSIANO WA FAMILIA

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza na kutaja ukoo wa watu,
- Kutumia ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kuuliza.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki.

Mukufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa Mkufunzi awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hii ni mbinu ambayo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.

- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga, kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi awapatie wanafunzi nafasi ya kutazama mchoro kisha awaongoze kueleza walichoona kwenye mchoro huo. Mapendekezo ya majibu:***

- Nimeona watu wengi ambao mmoja kati yao anawapiga picha.
- Huenda hii ikawa ni familia pana yenye babu na nyanya, watoto wao yaani familia mbili za mume na mke, na wajukuu wao pamoja na mpiga picha.

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kujibu maswali ya ufahamu kimakundi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Uhusiano uliopo kati ya Butera na Mukabutera ni kwamba wote ni ndugu. Yaani Butera ni kaka ya Mukabutera na Mukabutera ni dadake Butera.
2. Ni binti yake.
3. Ni bin yake.
4. Kujaza mapengo:
   a. Bw. Rutebuka ni **mume** wa Bi. Nyiranzage.
   b. Mukabutera ni d**ada yake** Butera.
   c. Rutabagisha ni **baba** yao Butera na Mukabutera.
5. Nyiramavugo atamwita mke wa Butera **mkaza mwana.**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi abandike flip chati moja inayobeba maswali kwenye ukuta na katika jozi wanafunzi waandike kwenye karatasi majibu ya maswali hayo kisha wayahusishe na maswali yaliyoulizwa kwenye flip chati. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Mama ya mama yangu anaitwa **nyanya.**
2. Ndugu wa kike wa baba yangu anaitwa **shangazi.**
3. Baba ya mume wangu anaitwa **babamkwe**.
4. Mtoto wa mtoto wangu anaitwa **mjukuu.**
5. Baba ya baba yangu anaitwa **babu.**
6. Mtoto wa mjukuu wako anaitwa **kitukuu.**
7. Mama ya mke wako anaitwa **mamamkwe.**
8. Mwanamke aliyeolewa na babako, na ambaye si mama yako wa damu anaitwa **mama wa kambo.**
9. Mtoto wa kwanza kuzaliwa anaitwa **kifunguamimba.**
10. Mtoto wa mwisho kuzaliwa anaitwa **kitindamimba.**

**Msamiati kuhusu uhusiano wa kifamilia.**

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aunde jozi tofauti darasani na kutumia mbinu ya fikiri- jozi- changia ili wanafunzi waweze kuchangia maoni kuhusu maana za maneno waliyopewa katika jozi zao.***

***Majibu yaliyopendekezwa:***

1. **Mzazi**: baba au mama wa mtu. Mtu mwenye watoto aliowazaa yeye mwenyewe.

2. **Nyanya**: Mzazi wa kike aliyemzaa baba au mama huitwa pia bibi.
3. **Kifunguamimba**: mtoto wa kwanza katika familia.
4. **Baba wa kambo**: Baba ambaye hana uhusiano wa damu na mtoto anayeishi naye.
5. **Binamu:** Mtoto wa shangazi au mjomba.

**Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya kuuliza katika ngeli ya LI-YA**

**Kazi ya 5:** ***Wanafunzi katika jozi, wasome sentensi walizopewa na kuchunguza upatanisho wa kisarufi unaojitokeza kwa kuongozwa na mkufunzi.***

Katika sentensi hizi, inaonekana kwamba vivumishi vya kuuliza vimechukua upatanisho wa kisarufi kufuatana na majina ya ngeli ya LI-YA. Katika umoja, kivumishi huchukua kiambishi ngeli LI- na katika wingi kivumishi hiki huchukua Ya-.

**Kazi ya 6:** ***Katika jozi, wanafunzi watumie vivumishi viulizi ambavyo wanapewa ndani ya mabano ili kujaza sentensi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Jibu **lipi** limeishapatikana?
2. Mawe **mangapi** yamewekwa kando ya barabara?
3. Madirisha **gani** yamefunguliwa?
4. Meno **yapi** yameng'oka?
5. Tunda **gani** limeiva?

**Kazi ya 7:** ***Mwanafunzi mmoja mmoja aandike sentensi hizi katika umoja au wingi, mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi anafanya zoezi hili. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Majengo yapi ni makubwa?
2. Papai lipi limeiva?
3. Nikupe gunia lipi/gani?
4. Shirika gani linasaidia wakulima?
5. Sasa ninyi mnataka niwape majembe yapi?

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 8:** ***Kila mwanafunzi asome maelezo hapo juu kuhusu uhusiano wa kifamilia kisha awaambie wenzake hali halisi ya kila mtu katika familia yake binafsi. Mkufunzi awaongoze katika mchakato huu.***

**Mfano:**

- Mimi ni mtoto wa Gakire na Nyiramafaranga,
- Shangazi yangu ni Mukundwa,
- Mjomba wangu ni Kwizera, n.k.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi atoe kazi ya nyumbani kwa wanafunzi ili waulize wazazi na majirani au wenzao muundo wa kifamilia wa ukoo wao. Baadaye kila mwanafunzi asimame mbele ya darasa na kuwazungumzia ukoo wake.***

**Mfano**: Mimi ni Umutoni, Umutoni wa Kabanda, Kabanda wa Gahigi, Gahigi wa Rutare, Rutare wa…, **n.k.**

**Kuandika**

**Kazi ya 10:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga mazungumzo kuhusu " uhusiano wa kifamilia"(Angalau misitari kumi na mitano).***

**Mwongozo :**

Hapa, mkufunzi awaongoze katika kuunda makundi darasani ya washiriki wawili, watatu au wanne kulingana na idadi ya wanafunzi wake. Mkufunzi awasisitizie kuwa ni lazima kifungu kiwe kinazingatia uhusiano waliojifunza katika mada hii.

## SOMO LA 8: VIFAA VYA NYUMBANI NA USAFI WAKE

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kueleza na kutaja vifaa vya nyumbani,
- Kutaja umuhimu wa usafi nyumbani,
- Kutumia ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,

- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya vifaa vinavyotumiwa katika kufanya usafi.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa, Mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majidiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi awaombe wanafunzi kuorodhesha vifaa vya nyumbani vinavyotumiwa kufanya usafi. Mwanafunzi mmoja baada ya mwingine ataje vifaa vyake kwa kuviandika kwenye flip chati iliyobandikwa kwenye ukuta darasani. Pendekezo la majibu:***

- Ndoo,deki, ufagio, beseni, sabuni, n.k

**Kusoma na ufahamu: Vifaa vya nyumbani na usafi wake**

**Kazi ya 2:** ***Kusoma kwa kimya kifungu cha habari kuhusu "Vifaa vya nyumbani" huku wakiandika msamiati mpya wanaouona na kutazama michoro. Mkufunzi aandike kichwa cha somo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika. Hatimaye mkufunzi awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma ili kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya na kuelewa, mkufunzi awaombe wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa sauti inayosikika kifungu kilichopo. Mkufunzi awaongoze wanafunzi kueleza maana ya maneno mapya yaliyomo kifunguni. Halafu mkufunzi awaongoze wanafunzi katika makundi yao, wafanye kazi zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi na yeye atoe msaada panapohitajika. Mkufunzi asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze kusahihisha ubaoni. Majibu yaliyopendekezwa katika maswali ya ufahamu:***

1. Ni sehemu zote za nyumba kama vile vyumba vya kulala, sebule, jikoni, chooni, na bila kusahau bustani, n.k.
2. Ni kama vile : Sahani, vikombe, vijiko, sufuria,vijiko, nguo, meza, kabati, runinga, redio, na kadhalika.
3. Watoto wanapaswa kuepukana na uchafu kwa sababu uchafu unasababisha magonjwa mbalimbali ya watoto, k.v. kuharisha, minyoo, upele, n.k. na familia hulipa gharama kubwa ya matibabu. Kwa hiyo, kujilinda uchafu ni kuchangia katika maendeleo ya familia nzima.
4. Katika kufanya usafi wa nyumbani tunatumia maji safi, sabuni, dawa ya kuua vijidudu, fagio, n.k.

5. Kunawa mikono baada ya kutoka msalani, kuchemsha maji kabla ya kuyatumia, kuweka dawa ya kuua vijidudu majini hasa kwenye pahali pachafu, kuosha vyombo, mboga na matunda kwa maji safi.
6. Maji safi humwezesha binadamu kuwa na afya nzuri na kufikia maendeleo yake.
7. Dosari au kasoro zinazotokana na kuwa na uchafu kwa binadamu na mazingira yake ni hizi zifuatazo:

- Kuambukizwa maradhi yatokanayo na uchafu kama: minyoo, kuhara, malaria itokanayo na mbu (kutofyeka nyasi karibu na nyumba, n.k.)
- Kupoteza uchumi wa familia kwa kulipa matibabu.
- Kukwama kimaendeleo kutokana na kupoteza muda na mali wakati mtu ameugua.

**Msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Katika jozi, wanafunzi watumie Kamusi ya Kiswahili Sanifu kwa kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kusaidiwa na mkufunzi.***

1. **Athari**: Wanyarwanda wanapopanda miti wanayepukana na **athari** za ukosefu wa mvua.
2. **Maanani**: Nchini Rwanda, kupiga marufuku itikadi ya mauaji ya kimbari ni jambo la kutiliwa **maanani.**
3. **Kuhara**: Kalisa ameumwa ugonjwa wa **kuhara** kwa sababu amekunywa maji machafu.
4. **Kinga:**Watalaamu wengi siku hizi wanatafuta **kinga** ya UKIMWI.
5. **Takataka:** Tunatupa **takataka** jalalani kama njia moja ya kuhifadhi mazingira.
6. **Kaya**: Nchini kwetu katika **kaya,** mama na baba hushirikiana katika shughuli zote.

**Kazi ya 4 :** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi au jozi na kuwaongoza kukamilisha sentensi walizopewa kwa kutumia maneno, k.v. runinga, redio, kijiko, sufuria, meza, malaria, usafi, tabia, sabuni, linafaa na vifaa.*** **Majibu:**

1. Mama anapika chakula ndani ya **sufuria.**
2. Tunaposoma kiswahili nyumbani, tunaandikia kwenye **meza.**
3. Nyanya yangu anatumia **kijiko** wakati mimi ninatumia uma.

4. Tunasikiliza habari za mpira kwenye **redio.**
5. Wanafunzi hupenda kutazama filamu kwenye **runinga.**
6. Usafi nyumbani ni jambo ambalo **linafaa** kutiliwa maanani.
7. Watu wengi wanafikiri kuwa **usafi** unahusu miili na mavazi tu.
8. Usafi nyumbani huonekana kupitia **vifaa** vinavyotumiwa nyumbani.
9. Kunawa mikono kwa maji na **sabuni** hupunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa.
10. Wazazi na walezi wengine wanapaswa kuwazoeza watoto **tabia** ya kunawa mikono kwa maji safi.
11. Nyasi nazo zinazozunguka nyumba zetu zinafaa kukatwa ili kuwafukuza mbu wanaosababisha ugonjwa wa **malaria.**

**Sarufi: Nomino za ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki**

**Kazi ya 5**: ***Katika jozi, wanafunzi wachunguze mifano ya sentensi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, kisha waeleze aina za maneno yaliyopigiwa mstari. Jibu lililopendekezwa*:**

Maneno yaliyopigiwa mstari ni vivumishi vya kumiliki kwa sababu yanatoa taarif ya kujulisha umiliki wa nomino.

**Kazi ya 6: *Wanafunzi waandike wingi wa sentensi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi na kuweka sentensi hizo katika wingi. Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea. Baadaye, wanafunzi wanaweza kubadilishana majibu ili kuchunguza kama majibu yao yote ni sahihi. Mapendekezo ya jibu:***

1. Majembe yetu yamepotea.
2. Majanga makubwa yamesababisha maafa.
3. Majaribio ya leo yamesahihishwa.
4. Majeshi yao yana askari wengi.
5. Majeraha yao yana uchafu sana.
6. Mambo haya yaliwafurahisha wengi.
7. Macho yao yanaoona mbali sana.
8. Mawe yetu yana thamani kubwa.
9. Meno yenu yameng’oka.
10. Meko yetu yameharibika.

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 7:** ***Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanafunzi wajadili kuhusu "Umuhimu wa usafi na madhara ya kutokuwa na usafi."***

**Tanbihi:** Hapa mkufunzi anatakiwa kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano hayo huku akipima matumizi ya lugha na jinsi kanuni za kisarufi zinavyotumiwa, n.k.

**Kazi ya 8**: ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi katika kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu ili kutambua umuhimu wa vifaa vilivyotolewa. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. **Bafu:** Chumba cha kuogea au beseni kubwa ambamo mtu huingia na kuoga.
2. **Sabuni:** Mchanganyiko wa vitu vinavyotokana na mafuta na kemikali nyingine ambavyo hutumiwa kwa kufulia, kuogea au kusafishia vitu.
3. **Deki:** Ni kifaa kinachotumiwa katika kudeki mahali pachafu kwa kutumia maji na sabuni.
4. **Ufagio:** Ni kifaa ambacho hutumiwa katika kufagia pahali penye uchafu, k.v. taka au vumbi.
5. **Taulo:** Ni kitambaa kinachotumiwa kufutia mwili baada ya kuoga.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya fikiri-jozi-changia kwa kuongoza kila mwanakundi kuelezea mwenzake namna wanavyofanya usafi nyumbani kwao hasa hasa usafi wa vifaa vya nyumbani.***

**Kuandika**

**Kazi ya 10:** ***Kazi hii inaweza kuwa ya nyumbani na ya kibinafsi. Kila mwanafunzi atunge kifungu cha habari kwa kutumia kichwa kilichotolewa ambacho ni "Uchafu ni asili ya maradhi mengi." Kipindi kijacho, wanafunzi wamkabidhi matokeo yao.***

# SOMO LA 9: MSAMIATI KUHUSU MIFUGO

## i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutaja na kueleza umuhimu wa mifugo wa nyumbani,
- Kutumia ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kuonyesha.

## ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya mifugo mbalimbali.

Mukufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa Mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

## iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii ya humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha wanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majidiliano.

**Kazi ya 1:** ***Katika jozi, mkufunzi aombe wanafunzi kukumbushana majina ya mifugo wanayoyajua. Mkufunzi abandike flip chati kwenye ukuta darasani na kila jozi iandike majibu yao kwenye flip chati hiyo. Mapendekezo ya majibu:***

a. Ng'ombe,

b. Nguruwe,

c. Mbuzi,

d. Kondoo,

e. Kuku,

f. Jogoo, n.k

**Kusoma na ufahamu: Kazi nzuri ya ufagaji**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi aongoze wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari huku wakiandika msamiati mpya wanaouona na kutazama michoro.***

***Mkufunzi aandike kichwa cha somo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika.***

***Hatimaye mkufunzi awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichokisoma kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya na kuelewa, mkufunzi awaombe wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa sauti inayosikika kifungu kilichopo. Mkufunzi awaongoze wanafunzi kueleza maana ya maneno mapya yaliyomo kifunguni. Halafu mkufunzi awaongoze wanafunzi katika makundi yao na kufanya kazi zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi. Aidha, mkufunzi atoe msaada panapohitajika. Mkufunzi asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze kusahihisha ubaoni. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Majina yote ya mifugo yaliyotajwa hapo juu ni: nyuki, kondoo, ng'ombe, kuku na farasi.
2. Umuhimu wa asali kwa maisha ya binadamu: asali inauzwa na inatumiwa kama chakula au hutengenezewa dawa.
3. Tunakata sufu ya kondoo kwa sababu sufu hutumiwa kutengenezea nyuzi za kufumia nguo.
4. Kabla ya kukama ng'ombe tunapaswa kuziosha chuchu kwa maji vuguvugu na kuzikausha kwa kitambaa safi.
5. Mifugo tano katika vifungu vya habari hapo juu na umuhimu wao kwa binadamu ni:

   a. **Nyuki** hutupatia asali. Asali ni chakula na dawa.

   b. **Kondoo** hutupatia nyama, fedha, sufu na mbolea.

   c. **Ng'ombe** hutupatia maziwa, nyama, mbolea na fedha.

   d. **Kuku** hutupatia mayai, nyama, mbolea na fedha.

   e. **Farasi** hubeba mizigo na watu na kutupatia fedha.
6. Kwa maoni yangu, ufugaji unaleta manufaa mengi kwa maendeleo ya nchi. Ufugaji ni njia moja miongoni mwa nyingine za kuletea nchi fedha kupitia: nyama, mbolea, n.k. tena ufugaji husaidia sana kilimo kutokana na mbolea.

**Msamiati kuhusu mifugo**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awamotishe wanafunzi kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu ili kutoa maana ya msamiati husika. Kazi hii ifanyiwe katika makundi kulingana na kamusi zilizopo. Majibu yaliyopendekezwa:***

**Kurina**: Kufukuza nyuki kutoka kwenye mzinga na kukata masega ili kupakua asali.

**Kukata sufu**: Kunyoa manyoya ya kondoo kutoka kwenye ngozi yake.

**Kukama**: Kuminya chuchu za mnyama kama vile ng'ombe ili maziwa yatoke.

**Kupandisha madume kwa mtamba**: Kumpa ng'ombe wa kike mbegu za kiume ili kuzalisha ndama.

**Kufuga ng'ombe ndani kwa ndani**: Kufuga ng'ombe ndani ya eneo au jengo fulani na kuwapa mahitaji yote humo bila kuwatoa nje.

**Kuwapeleka ng'ombe katika josho**: Kuwapelekea ng'ombe katika dimbwi maalumu lililotiwa dawa ya kuulia kupe.

**Kuatamisha kuku**: Kumfanya kuku kulalia mayai.

**Kuchunga**: Kuwapeleka wanyama malishoni na kuwalinda wasiibwe.

**Kukata pembe**: Kutoa pembe kwa kutumia kisu au chuma moto.

**Kazi ya 4:** ***Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu, wanafunzi waongozwe kusoma kifungu cha habari husika na kutafuta maana za maneno yaliyotajwa. Majibu:***

| A | B |
|---|---|
| 1 | g |
| 2 | a |
| 3 | c |
| 4 | f |
| 5 | e |
| 6 | d |
| 7 | b |

**Sarufi: Ngeli ya LI –YA na vivumishi vya kuonyesha**

**Kazi ya 5:** ***Katika jozi, mkufunzi aongoze wanafunzi kutazama sentensi husika na kujadili mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza.***

**Jibu:** Mabadiliko yanayojitokeza yanaandamana na matumizi ya ngeli ya LI-YA pamoja na vivumishi vya kuonyensha. Msisitizo umewekwa kwenye upatanisho wa kisarufi ambapo katika umoja kivumishi cha kuonyesha huchukua kiambishi ngeli LI- na katika wingi huchukua kiambishi YA-.

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii inaweza kuwa ya kibinafsi. Hapa mkufunzi ajenge tabia ya ujasiri miongoni mwa wanafunzi na kuwawezesha kujitegemea. Majibu yaliyopendekezwa :***

1. Debe **hili** lilitoboka.
2. Jambazi **lile** liliadhibiwa.
3. Tafadhali kunja majamvi **hayo**.
4. Anakuomba umnunuliye machungwa **hayo**.
5. Jahazi **lile** ni kubwa.

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi kwa kila mwanafunzi na asahihishe sentensi kama ilivyoagizwa. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Kabati **lile** lilivunjwa na wezi.
2. Maji haya **ya**limwagwa ovyo sakafuni.
3. Alipotaka kujenga nyumba alitafuta **mawe** makubwa.
4. Mafuta haya ha**ya**mwagwi ziwani kwa sababu **y**anaweza kuua samaki.
5. Maboga haya yana manufaa **mengi** kwa mwili wako.

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 8:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kuchunguza michoro ya mifugo iliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi na kuihusisha na majina yao. Mifugo hao ni: mbuzi, mbwa, kuku, paka na sungura. Kusikiliza na kuzungumza***

**Kazi ya 9:** ***Katika jozi au makundi, kila mwanafunzi azungumzie wanafunzi wengine jinsi nyumbani kwao au kwa babu yake wanavyofanya ufugaji.***

**Kuandika**

**Kazi ya 10:** ***Katika kundi la wanafunzi watano, mkufunzi awaongoze kutunga kifungu kifupi cha maneno yasiozidi 100 kuhusu " Umuhimu wa ufugaji nchini Rwanda." Baadaye mkufunzi asahihishe kazi hizi akizingatia makosa ya kiotografia na kisintaksia.***

## 2.6. Muhtasari wa mada

Mada hii ya pili "**Matumizi ya Kiswahili nyumbani**" ina masomo matano yanayohusiana na mada husika. **Somo la kwanza** linayeleza mazingira ya nyumbani yaani sehemu za nyumba,vifaa vitumiwavyo kwa

kujenga nyumba na matumizi ya ngeli ya LI-YA katika sentensi. **Somo la pili** linashughulikia watu wanaopatikana nyumbani, majukumu yao, kazi za nyumbani na matumizi ya vivumishi vya idadi katika ngeli ya ya LI-YA. **Somo la tatu** linashughulikia uhusiano wa kifamilia yaani ukoo wa mtu pamoja na matumizi ya vivumishi vya kuuliza katika ngeli ya LI-YA. **Somo la nne** linashughulikia vifaa vya nyubani na usafi wake pamoja na matumizi ya vivumishi vya kumiliki katika ngeli ya LI-YA. **Somo la tano** linashughulikia msamiati kuhusu mifugo na matumizi ya vivumishi vya kuonyesha katika ngeli ya LI-YA. Kila somo linaundwa na vipengele vidogo vidogo sita kama vile maswali ya ufahamu, msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, kusoma na kusikiliza, na kuandika.

## 2.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana haki au idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao kwa ajili ya kuimarisha shauku yao ya kuitumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

## 2.8. Tathmini ya mada

***Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea baina ya wanafunzi. Hii pia itasaidia kupima uwezo wa kila mwanafunzi kwa njia rahisi.***

1. Tumia maneno ya ngeli ya LI-YA yaliyo katika mabano na vivumishi vya kumiliki au vya sifa kwa kutunga sentensi sahihi katika umoja (azimio, ini, jiko,ua, shamba).
   a. Azimio: Mimi nina **azimio** la kufanya kazi kwa bidii na kuondoa umaskini nyumbani mwangu.
   b. Ini: **Ini** lake linaumwa ndiyo maana anadhoofika.
   c. Jiko: **Jiko letu** limejengwa vizuri.
   d. Ua: **Ua hili** linauzwa kwa bei ghali.
   e. Shamba: **Shamba hilo** lina mahindi mazuri.
2. Weka sentensi za hapo juu (angalia swali la kwanza) katika wingi
   a. Sisi tuna maazimio ya kufanya kazi kwa bidii na kuondoa umaskini nyumbani mwetu.

b. Ma**ini yao yana**umwa ndiyo maana wanadhoofika.

**c. Meko yetu** yamejengwa vizuri.

d. Ma**ua haya** yanauzwa kwa bei ghali.

**e. Mashamba hayo** yana mahindi mazuri.

3. Wanafunzi wajaze sentensi walizopewa kwa kutumia maneno: baba, wifi, mama, shangazi, mjomba, mjukuu, binamu, mpwa, mapacha na baba wa kambo.

**Majibu:**

a. Mke wa baba yako ni **mama** yako**.**

b. Mume wa mama yako utamuita **baba** yako.

c. Mtoto wa mjomba au shangazi yako ni **binamu.**

d. Mtoto wa mtoto wako utamuita **mjukuu**.

e. Bwana ya mama yako ambaye si baba yako utamuita **baba wa kambo.**

f. Dada ya baba yako utamuita **shangazi.**

g. Kaka ya mama yako utamuita **mjomba.**

h. Mke wa ndugu yako utamuita **wifi.**

i. Watoto wawili waliozaliwa siku moja na mama mmoja tutawaita **mapacha.**

j. Mtoto wa dada yako utamuita **mpwa.**

4. Umuhimu wa vifaa vya nyumbani vifuatavyo: Sufuria, kikombe, kabati, sabuni na kiti.

**Majibu**

| **Kifaa** | **Umuhimu** |
|---|---|
| a. Sufuria | kupika chakula |
| b. Kikombe | Kunywea maji |
| c. Kabati | Kuwekea vitu |
| d. Sabuni | Kufulia na kuogea |
| e. Kiti | kukalia |

5. Mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga insha ndogo ya maneno yasiyozidi 100 kuhusu “Umuhimu wa kuishi katika nyumba ya kisisa kwa maisha ya binadamu”

Mkufunzi hapa anatoa mwongozo wa kutunga insha.

- Namna ya kutunga insha na sehemu kuu za insha kama vile: kichwa, utangulizi, mwili, na hitimisho.
- Kulinganisha nyumba ya jadi na nyumba ya kisasa, n.k.

## 2.9. Kazi za ziada

### 2.9.1. Kazi za urekebishaji

Haya ni maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye kiwango cha chini.

- Sahihisha sentensi zifuatazo.

a. Majino yake mazuri yameng'oka.

b. Majiko ya makaa analeta uchafu nyumbani.

c. Madawati zinavunjika.

d. Majiwe yanajenga nyumba.

e. Madirisha wanafungwa.

**Majibu:**

a. Meno yake mazuri yameng'oka.

b. Meko ya makaa yanaleta uchafu nyumbani.

c. Madawati yanavunjika.

d. Mawe yanajenga nyumba.

e. Madirisha yanafungwa.

### 2.9.2. Kazi jumuishi

- Andika sentensi zifuatazo katika umoja au wingi

a. Jibu zuri linafurahisha.

b. Mawe mabaya yamewekwa kando ya nyumba.

c. Madirisha mazuri kwenye nyumba yanapendeza.

d. Meno makubwa yameng'oka.

e. Tunda zuri linauzwa kwa bei ghali.

**Majibu**

a. Majibu mazuri yanafurahisha.

b. Jiwe baya limewekwa kando ya nyumba.

c. Dirisha zuri kwenye nyumba linapendeza.

d. Jino kubwa limeng'oka.

e. Matunda mazuri yanauzwa kwa bei ghali.

### 2.9.3. Kazi za nyongeza

Sehemu hii inahusu wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu cha werevu.

Mkufunzi awapatie wanafunzi wa kundi hili kazi kulingana na kiwango cha ujuzi na uwezo wao.

**Mfano wa kazi:**

Tunga kifungu cha habari chenye aya mbili kwa kutumia majina angalau matano ya ngeli ya li – ya.

# MADA YA 3:

# MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALI

## 3.1. Uwezo mahususi katika mada

Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya hospitali

## 3.2. Ujuzi wa awali

Mada hii inazungumzia "Msamiati katika mazingira ya hospitali." Tayari wanafunzi wa mwaka huu wana ujuzi wa awali wa kutosha kuhusu msamiati utumiwao katika sehemu mbalimbali. Ikumbukwe kuwa katika kidato cha tatu, wanafunzi waliyagusia sana mambo ya matumizi ya msamiati katika mazingira mbalimbali kama vile sokoni, nyumbani, shuleni na hata hotelini. Kwa hiyo, mada hii itakuwa chanzo cha kupanua ujuzi wa msamiati walionao kuelekea mazingira ya hospitalini. Isitoshe, msamiati wa mazingira ya hospitali ni mojawapo ya msamiati wa matumizi katika maisha ya kila siku. Kwa hiyo, si kitu kipya kwa wanafunzi kwa sababu wengi baadhi yao huwa wanahitaji huduma katika hospitali mbalimbali.

## 3.3. Masuala mtambuka

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile uhifadhi wa mazingira, usawa wa jinsia pamoja na elimu jumuishi. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika.

## 3.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi, wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 3.5. Orodha ya masomo

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| 1. Sehemu za hospitali | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja sehemu za hospitali na kueleza umuhimu wake.<br><br>**Stadi:** Kutumia kwa usahihi msamiati husika katika mawasiliano ya muktadha unaofaa.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha usafi katika sehemu zote za mazingira unamoishi. | 4 |
| 2. Vifaa vya hospitalini | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha vifaa vitumiwavyo hospitalini na kueleza umuhimu wake.<br><br>**Stadi:** Kutumia kwa usahihi msamiati husika katika mawasiliano ya muktadha unaofaa.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuboresha usafi na usanifishaji wa vifaa vyote vinavyotumiwa mahali mbalimbali. | 4 |
| 3. Wafanyakazi hospitalini | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha wafanyakazi wa hospitalini na kueleza majukumu yao.<br><br>**Stadi:** Kutumia kwa usahihi msamiati husika katika mawasiliano ya muktadha unaofaa.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujivunia huduma bora katika kazi mbalimbali | 4 |
| 4. Usafi hospitalini | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza umuhimu wa usafi hospitalini.<br><br>**Stadi**: Kufanya usafi kwa kuboresha afya.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha usafi katika mazingira mbalimbali. | 4 |
| 5. Adabu hospitalini | **Maarifa na ufahamu:** Kuonyesha mwenendo au maadili mema hospitalini.<br><br>**Stadi**: Kufuata na kutimiza sheria za hospitalini.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kukuza adabu hospitalini. | 4 |

| | | |
|---|---|---|
| Tathmini ya mada | | 2 |
| Vipindi vya mada yote | | 22 |

## SOMO LA 10: SEHEMU ZA HOSPITALI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kubainisha na kueleza sehemu mbalimbali za hospitali,
- Kutumia kwa ufasaha msamiati maalum wa mazingira ya hospitali katika mawasiliano,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia katika sentensi mbalimbali kauli za vitenzi tofauti.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha jengo la hospitali, vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.

- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu**: Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**KIDOKEZO**

***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Mahali penye majengo ambapo wagonjwa huhudumiwa kwa njia moja au nyingine.
2. Roi Faisal, CHUK, KMH( Kanombe Military Hospital).
3. Vifaa vitano vinavyotumiwa hospitalini na umuhimu wake.

- ***Sindano:*** *Kifaa cha kupenyezea dawa mwilini.*
- ***Machela:*** *Kifaa cha kuwabeba wagonjwa hospitalini.*
- ***Makasi:*** *Kifaa cha kukatia vitu mbalimbali.*
- ***Bendeji:*** *Ni kitambaa cha kufungia jeraha au kidonda ili kisichafuliwe.*
- ***Eksrei au uyoka:*** *Ni mashine ya kutazamia viungo vya ndani ya mwili.*

4. Wafanyakazi angalau wanne wapatikanao hospitalini na kazi au majukumu yao:

- Daktari au tabibu huwatibu wagonjwa.
- Muuguzi au nesi humsaidia daktari katika kazi yake.
- Mhazigi huwashughulikia waliovunjika viungo kama vile miguu au mikono.
- Karani hufanya rekodi za wagonjwa.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo kila mwanafunzi anapewa fursa ya kutoa maoni yake. Mapendekezo ya majibu:***

**Ninaona:**

- Mwamume anayevaa bwelasuti na stethoskopu sawa na daktari,
- Majengo yenye milango sawa na ya hospitali,
- Watu wanaokaa kwenye viti kama wagonjwa wanaohitaji kuhudumiwa,
- Mtu anayeendesha baiskeli ya hospitalini.

**Kusoma na ufahamu: Ziara yetu hospitalini**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo na kuwaongoza katika majadiliano yao. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

**A.**

1. Habari hii imetokea katika hospitali iliyoko wilayani Huye, kati ya Daktari mkuu, muuguzi wake na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Maadili.
2. Lengo la wanafunzi kuitembelea hospitali lilikuwa la kuyaelewa vyema mazingira ya hospitali hiyo.

3. Watu wanaozungumza katika kifungu cha habari hiki ni: Daktari mkuu, muuguzi, wanafunzi wageni kama vile Aminata, Pascal, Samilla na Jado.
4. Sehemu za hospitali zilizotajwa ni:
   - Pambajio au sehemu ya kuwapokelea wagonjwa,
   - Chumba cha matibabu ya dharura,
   - Wodi au chumba cha kushughulikia maradhi ambayo si ya kawaida kama vile maradhi ambayo yamezuka ghafla na bado hayaeleweki vizuri,
   - Maabara ni chumba cha kufanyia uchunguzi wa magonjwa,
   - Chumba cha kuhifadhia dawa,
   - Kungawi, yaani chumba cha kujifungulia kwa kina mama wajawazito.
5. Aminata alikuwa kiranja, yaani kiongozi wa darasa.

**B.**

1. c
2. d
3. b
4. a
5. b

**Matumizi ya msamiati kuhu mazingira ya hospitali**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya Kamusi za Kiswahili Sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. ***Kudunga:*** *kuchoma kwa kitu chenye ncha.*
2. ***Matibabu:*** *dawa na huduma inayotolewa kwa kumtibu mgonjwa.*
3. ***Mgonjwa:*** *mtu aliye na maradhi au maumivu fulani katika mwili wake.*
4. ***Hali mahututi:*** *hali ya mgonjwa kukaribia kufa.*
5. ***Kupenyeza:*** *kulazimisha kitu kiingie mahali penye uwazi mdogo.*
6. ***Kuhifadhi:*** *kuweka mahali pa salama.*
7. ***Uchafu:*** *hali ya kutokuwa safi, taka.*
8. ***Mjamzito:*** *mwanamke mwenye mimba.*

9. ***Kujifungua:*** *kuzaa.*
10. ***Dharura:*** *shughuli au jambo la haraka linalotokea bila ya kupangwa au kutazamiwa.*

Baada ya kutoa maana, mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga sentensi mmoja kwa mmoja na kusahihisha makosa mbalimbali yanayoweza kujitokeza.

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya fikiri-jozi-changia. Jozi inayotoa jibu sahihi ipigiwe makofi. Inayokosa jibu isahihishwe na nyingine.***

1. *c.*
2. *d.*
3. *a.*
4. *e.*
5. *b.*

**Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi**

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Wanafunzi wawili wawili wajadiliane kuhusu nafasi ya viambishi vilivyokolea pamoja na athari yake ndani ya kitenzi. Majibu yaliyopendekezwa:***

Viambishi vilivyokolea ni viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi.

Mnyambuliko wa vitenzi ni jinsi vitenzi vinavyobadilika kulingana na kauli/hali mbalimbali.

Hapo juu kauli za vitenzi zilizotumiwa ni tatu kama ifuatavyo:

i. Kauli ya kutenda

ii. Kauli ya kutendana

iii. Kauli ya kutendea

- Kauli ya Kutenda - kitendo katika hali yake ya kawaida (bila kunyambuliwa).
- Kauli ya Kutendana - unamfanya mtu kitendo, naye anakufanya vivyo hivyo.
- Kauli ya Kutendea - kufanya kitendo kwa niaba (au kwa ajili) ya mtu mwingine

**Kazi ya 6:** ***Unda makundi matano. Kila kundi lipewe kitenzi na kuombwa kukinyambua katika kauli mbili husika. Pendekezo:***

| Kundi | Kitenzi | kutendea | Kutendeana |
|---|---|---|---|
| 1 | jenga | Jengea | Jengeana |
| 2 | lima | Limia | Limiana |
| 3 | kufanya | kufanyia | kufanyiana |
| 4 | kusoma | kusomea | kusomeana |
| 5 | imba | imbia | imbiana |

**Kazi ya 7.** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi ajitegemee kuunda sentensi na baadaye aisome darasani kwa kutoa sauti ili wenzake wakubaliane naye au wasahihishe.***

**Mfano:**

- Wanafunzi **wamefanya** kazi nzuri sana.
- **Walimpelekea** zawadi kwa sababu ya mchango wake katika vitendo vya kupigana dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.
- Inatubidi **tushirikiane** katika kazi zote ili kujenga umoja kati yetu.

**Kazi ya 8:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Tumemwandikia barua kwa ajili ya mwaliko.
2. Wazazi waliwafanyia mema watoto wao.
3. Baba yake amemwekea mtoto wake pesa kwenye akaunti.

**Matumizi ya lugha: Sehemu muhimu za hospitali**

**Kazi ya 9:** ***Chora sehemu muhimu za hospitali kwenye karatasi au kwenye ubao. Washirikishe wanafunzi kwenda mbele. Mmoja atoe jina la sehemu fulani, mwenzake aeleze umuhimu wa sehemu hiyo.***

**Mfano:**

Wodi: Sehemu ya kuwalaza wagonjwa wanapoendelea kupokea matibabu.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 10:** ***Kazi hii itolewe kama kazi ya nyumbani. Wanafunzi wawasilishe kazi yao darasani wakati wa kipindi kijacho.***

**Kazi ya 11:** ***Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika katika mazungumzo husika. Kila mwanafunzi apewe jukumu lake la kuigiza, wakati unaokusudiwa kuwasilisha kazi hii.***

**Kazi ya 12:** ***Kazi hii iwe ya kipekee. Kila mwanafunzi apewe fursa ya kufikiri na kuorodhesha maoni, kisha ashirikishwe kwenda mbele ya darasa na kuwasilisha hoja zake.***

**Kuandika**

**Kazi ya 13:** ***Kazi katika makundi madogomadogo. Washirikishe wanafunzi katika kazi ya kuchora hospitali na kuwasilisha matokeo ya kila kundi.***

## SOMO LA 11: VIFAA VYA HOSPITALINI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kubainisha na kueleza vifaa mbalimbali vitumiwavyo hospitalini,
- Kutumia kwa ufasaha katika mawasiliano msamiati maalum kuhusu vifaa vya hospitali,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia katika sentensi mbalimbali kauli za vitenzi tofauti.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha baadhi ya vifaa vitumiwavyo hospitalini, vifaa halisi kama makasi, bendeji, plasta,vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali, kitabu cha mwanafunzi na kitabu cha mkufunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.

- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii ya humwacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Weka michoro miwili miwili kwenye karatasi kubwa na kuibandika kwenye ubao au ukuta. Washirikishe wanafunzi kwenda mbele. Mmoja atoe jina la kifaa, mwenzake aeleze umuhimu wa kifaa hicho.***

**Mfano:**

1. **Mikroskopu au hadubini:** Inatumiwa kuangalia vijidudu vidogo sana ambavyo haviwezi kuonekana kwa macho.

2. **Sindano**: Zinatumiwa kwa kupenyezea dawa mwilini.
3. **Vitanda**: Umuhimu wake ni kuwasaidia wagonjwa kulala.
4. **Vidonge**: Wagonjwa huvimeza kwa ajili ya matibabu.
5. **Makasi** : Hutumiwa hospitalini kukata vitu mbalimbali.
6. **Kipimajoto :** Hutumiwa kwa kupima kiwango cha joto mgonjwa alichonacho.

**Kusoma na ufahamu: Vifaa vya hospitalini**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo na kuwaongoza katika majadiliano yao. Pendekezo la majibu ya ufahamu:***

**A.**

1. Mazungumzo yametokea hospitalini katika vyumba mbalimbali ambamo vifaa tofauti hupatikana.
2. Kutazama vifaa vya hospitalini na kuelewa umuhimu wake.
3. Daktari mkuu, muuguzi, Aminata pamoja na Bugingo.
4. Sindano kwa sababu watoto hata watu wazima huogopa kudungwa sindano.
5. Ametumia mbinu ya kuonyesha michoro ya vifaa tofauti.

**B.**

1. a
2. d
3. d
4. d
5. c

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Waweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya kamusi za Kiswahili sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Baada ya kutoa maana, waongoze wanafunzi kutunga sentensi mmoja kwa mmoja na kusahihisha makosa mbalimbali yanayoweza kujitokeza.***

i. **Vidudu:** Mdudu mdogo sana.

ii. **Bakteria**: Kiumbe mdogo sana anayeonekana kwa hadubini tu na ambaye wakati mwingine husababisha ugonjwa kwa binadamu na wanyama. Pia kijasumu, kimelea.

iii. **Kuhifadhi**: Kuweka kitu mahali pa usalama kwa matumizi ya baadaye; kutunza.

iv. **Jeraha**: Kidonda au mchubuko ulio kwenye mwili.

v. **Kidonda**: Jeraha kubwa sana.

**Kazi ya 4:** ***Tumia mbinu ya Fikiri-Jozi-Changia. Jozi inayotoa jibu sahihi ipigiwe makofi. Inayokosa jibu isahihishwe na nyingine. Yafuatayo ni majibu yaliyo pendekezwa:***

| Maneno | Maelezo |
|---|---|
| ***Sabuni*** | Mchanganyiko wa vitu vinavyotokana na mafuta na aina mojawapo ya magadi na ambayo hutumiwa kwa kufulia, kuogea au kusafisha vitu. |
| Machela | *Kifaa kitumiwacho hospitalini kuwabeba wagonjwa* |
| ***Makasi*** | Kifaa kinachotengenezwa kwa madini, aghalabu ya chuma, chenye visu viwili vilivyounganishwa kwa msumari mdogo na tundu mbili za kuingizia vidole, kinachotumiwa kukatia kitu k.v. nguo au nywele. |
| ***Plasta*** | Kitu kama gome gumu kilichotengenezwa kwa unga maalumu na kitambaa kinachofungwa sehemu ya mwili iliyovunjika ili kushikanisha mifupa iliyovunjika. |

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Mkufunzi amotishe jozi ambayo imepata jibu na kulitoa. Kama jozi nyingine haikubaliani na jibu hilo ipewe fursa ya kutoa hoja. Mkufunzi ashiriki kama mtatuzi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Kitambaa kigumu sana cha kufungia sehemu iliyovunjika huitwa ***plasta.***
2. Dipfriza ni *kifaa cha* ***kuhifadhia baadhi ya dawa.***
3. ***Sindano*** ni kifaa cha kupenyezea dawa mwilini.
4. ***Eksirei*** ni mashine ya kuonea viungo vya ndani ya mwili.

**Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi**

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Wanafunzi wawili wawili wajadiliane kuhusu nafasi ya viambishi vilivyokolea pamoja na athari yake ndani ya kitenzi. Pendekezo la majibu*****:**

Viambishi vilivyokolea ni viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi.

Mnyambuliko wa vitenzi ni jinsi vitenzi vinavyobadilika kulingana na kauli/hali mbalimbali.

Hapo juu kauli za vitenzi zilizotumiwa ni tatu kama ifuatavyo:

- Kauli ya kutendeka
- Kauli ya kutendesha
- Kauli ya kutendewa

**Kazi ya 7:** ***Unda makundi matano. Kila kundi lipewe kitenzi na kuombwa kukinyambua katika kauli mbili husika. Pendekezo la majibu:***

| Kundi | Kitenzi | kutendeka | Kutendewa |
|---|---|---|---|
| 1 | kunywa | kunyweka | kunywewa |
| 2 | kuzaa | kuzalika | kuzaliwa |
| 3 | kupenda | kupendeka | kupendewa |
| 4 | kutaja | kutajika | kutajiwa |
| 5 | kujenga | kujengeka | kujengewa |

**Kazi ya 8.** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi ajitegemee kuunda sentensi na baadaye aisome darasani kwa kutoa sauti ili wenzake wakubaliane naye au wasahihishe.***

**Mfano:**

- Kazi ya udaktari inapendeka sana.
- Si vizuri kufanyisha watoto kazi ngumu.
- Ametusomea ushahidi wa mtu aliyenusurika mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi..

**Kazi ya 9:** ***Chagua mwanafunzi wa kujitolea na kumwomba asome sentensi moja na mwingine aitolee jibu. Endelea namna hii mpaka sentensi zote zisahihishwe.***

Mtoto alipatiwa na baba yake elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira, uzalishaji mali pamoja na usawa wa kijinsia. Alielezewa pia faida za kupiga marufuku uvivu, ulevi pamoja na ukatili. Alitungiwa hadithi za kumwongoza na kumwelekeza katika njia nzuri za kimaisha. Baadaye alipelekewa wajibu wa kuzitetea haki za binadamu na kuishi kwa amani na watu wote mahali popote atakapokuwepo.

### Matumizi ya lugha: Vifaa vya hospitalini

**Kazi ya 10:** Weka michoro miwili miwili kwenye karatasi kubwa na kuibandika kwenye ubao au ukuta. Washirikishe wanafunzi kwenda mbele. Mmoja atoe jina la kifaa, mwenzake aeleze umuhimu wa kifaa hicho.

**Mfano:**

1. **Mikroskopu au hadubini**: Inatumiwa kuangalia vijidudu vidogo sana ambavyo haviwezi kuonekana kwa macho.
2. **Sindano**: Zinatumiwa kwa kupenyezea dawa mwilini.
3. **Vitanda**: Umuhimu wake ni kuwasaidia wagonjwa kulala.
4. **Vidonge**: Wagonjwa huvimeza kwa ajili ya matibabu.
5. **Makasi**: Hutumiwa hospitalini kukatia vitu mbalimbali.
6. **Kipimajoto**: Hutumiwa kwa kupima kiwango cha joto mgonjwa alichonacho.

**Kazi ya 11:** ***Wagawe wanafunzi katika makundi matano. Kila kundi lipewe idadi ya vifaa vya kushughulikia, kisha kila kundi liwasilishe kazi yake.***

**Kwa mfano:**

**Koleo:** Kifaa cha kushikia vitu vinavyotumiwa na daktari.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 12**: ***Kazi hii itolewe kama kazi ya nyumbani. Wanafunzi wawasilishe kazi yao darasani wakati wa kipindi kijacho. Kinacholengwa ni kumwezesha mwanafunzi kuwa na uwezo wa kuvitambua vyombo vitumiwavyo nyumbani.***

**Kazi ya 13:** ***Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika kisha wapewe muda wa kuwasilisha utafiti wao kuhusu vyombo walivyoviona zahanatini. Kazi hii ifanywe kimazungumzo mbele ya darasa na mkufunzi aliongoze darasa lake katika kumuunga mkono mwenzao au kusahihisha pale anapokosea.***

**Kazi ya 14:** ***Kazi hii iwe ya kipekee. Kila mwanafunzi apewe fursa ya kufikiri na kuorodhesha maoni, kisha ashirikishwe kwenda mbele ya darasa na kuwasilisha hoja zake.***

**Kuandika**

**Kazi ya 15:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Mwanafunzi wa kujitolea atoe jibu kwa kushirikiana na wenzake.***

**Mfano:**

a. Nilipokuwa bado mtoto nilikuwa na woga wa kuenda hospitalini kwa sababu **ya kuogopa kudungwa sindano.**

b. Inasemekana leo kuwa Hospitali ya Roi Faisal ni maarufu sana kwa sababu **inatumia vifaa vya kisasa na wafanyakazi wataalamu.**

c. Hospitali au zahanati nyingi hushindwa kutoa huduma bora kwa sababu **ya ukosefu wa vifaa vya kutosha na wafanyakazi mashuhuri.**

d. Sindano, hospitalini, hutumiwa mara moja kwa mgonjwa kwa ajili ya **kupenyezea dawa**.

## SOMO LA 12: WAFANYAKAZI WA HOSPITALINI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutaja wafanyakazi wanaopatikana hospitalini na majukumu yao,
- Kutumia kwa ufasaha, katika mawasiliano, msamiati maalum kuhusu wafanyakazi wa hospitalini,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia katika sentensi mbalimbali kauli za vitenzi tofauti.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha baadhi ya wafanyakazi wa hospitalini,vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.

- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa.

**Kazi ya 1:** ***Tumia mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Wamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao.***

**Mwelekeo** :

**Ninaona:**

- Daktari ambaye amevaa bwelasuti nyeupe, kofia, glovu pamoja na stethoskopu shingoni,
- Muuguzi,
- Dobi ambaye ni mwanamke,
- Mwanamume anayepiga deki.

**Kusoma na ufahamu: Kazi nzuri ya udaktari**

**Kazi ya 2:** ***Tumia mbinu ya kazi ya mzunguko darasani ambapo karatasi nne zenye kuonyesha maswali manne zimebandikwa kwenye kuta tofauti. Waweke wanafunzi katika makundi. Kundi la kwanza kwenye karatasi ya kwanza na kuandika kitu, kundi la pili likafuata, n.k. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Wafanyakazi wa hospitali wanane ambao ni muuguzi, mkunga, mhazigi, msaidizi, karani, mfamasia, daktari wa meno, daktari mkuu pamoja na wanafunzi wawili ambao ni Aminata pamoja na Mireille.
2. Kuelezewa kuhusu wafanyakazi wa hospitalini na majukumu yao.
3. Faida: wanafunzi wameelezewa mengi kuhusu hospitali na wameridhika nayo. Hasara: Ziara hii imewafanya wafanyakazi karibu wote kusimamisha kidogo kazi zao kwa ajili ya kuwasiliana na wanafunzi wageni. Labda, kuna huduma mbalimbali ambazo hazikufanyika kama ilivyopangwa.
4. Ndiyo. Wanafunzi wameridhika na ziara yao kwa sababu wamefurahia habari zote walizopata na mwishowe, wameahidi kuwaunga mkono wafanyakazi wa hospitali kwa kuchagua mchepuo wa udaktari.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya kamusi za Kiswahili sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Baada ya kutoa maana, mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga sentensi mmoja kwa mmoja na kusahihisha makosa mbalimbali yanayoweza kujitokeza. Majibu:***

a. **Kutibu:** Kumpa mtu dawa au matibabu ya kuponyesha ugonjwa wake.

**M.f:** Daktari ni fundi wa **kutibu** magonjwa mbalimbali.

b. Jukumu: Wajibu na shughuli za mtu.

**M.f:** Mwanafunzi hodari ana **wajibu** mkubwa wa kushinda masomo yake yote.

c. Kwa mujibu: Kwa kuzingatia, kulingana na.

**M.f:** Kwa **mujibu** wa wandishi wa vitabu, uandishi si kazi rahisi.

d. Wahenga: mjuzi wa mambo ya kale mwenye kutegemewa kutoa ushauri katika masuala ya kijamii.

**M.f:** Nchi ya Rwanda inababahatika kuwa na **wahenga** wengi katika ngazi za serikali zote.

e. Kuahidi: kutoa ahadi

**M.f:** wanafunzi wa mwaka wa kwanza walisoma kwa bidii baada ya **kumwahidi** mkufunzi wao kutomuaibisha katika matokeo ya mitihani ya taifa.

**Kazi ya 4:** ***Tumia mbinu ya fikiri-jozi-changia. Jozi inayotoa jibu sahihi ipigiwe makofi, nyingine ambayo imekosa jibu isidharauliwe bali isaidiwe. Majibu yaliyopendekezwa:***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. | h |
| 2. | a |
| 3. | b |
| 4. | f |
| 5. | c |
| 6. | g |
| 7. | e |
| 8. | i |
| 9. | j |
| 10. | d |

**Kazi ya 5:** ***Kazi katika jozi. Chunguza kila jozi kwa ajili ya kuhakikisha kuwa majibu sahihi yamepatikana. Majibu yaliyopendekezwa:***

| | |
|---|---|
| 1. | c |
| 2. | d |
| 3. | b |
| 4. | e |
| 5. | a |

## Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi

**Kazi ya 6 :** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Wanafunzi wawili wawili wajadilane kuhusu nafasi ya viambishi vilivyokolea pamoja na athari yake ndani ya kitenzi. Jibu lililopendekezwa:***

Viambishi vilivyokolea vinaonyesha kauli ya kutendwa ambayo huathirika moja kwa moja na kitendo.

**Kazi ya 7:** ***Kazi katika jozi. Mkufunzi achunguze ikiwa kila mwanafunzi anashiriki ipasavyo na kutoa mchango wake katika jozi. Mapendekezo ya majibu:***

1. Pesa zangu zimeibiwa na wezi.
2. Mtoto wa kike wetu alizaliwa miaka sita iliyopita.
3. Nzi wenye kutoka chooni wameuliwa na dawa.
4. Meneja alifikishwa mahakamani na kampuni yake kwa sababu ya uporaji mali.
5. Chakula kitamu kimeliwa kwa wingi.
6. Samaki wengi walivuliwa kutoka ziwa Kivu.
7. Si vizuri pombe kuywewa hospitalini.
8. Barabara za lami nyingi zitatengenezwa na wilaya.
9. Nguo za aina mbalimbali zimefuliwa na dobi.

**Matumizi ya lugha: Aina za kazi**

**Kazi ya 8:** ***Tumia mbinu ya bunguabongo. Mkufunzi ahakikishe kuwa mwanafunzi anayetaja mfanyakazi fulani anataja pia kazi anayoifanya. Wanafunzi huweza kutoa baadhi ya majibu haya:***

**Mfano**: Askari jeshi : Hulinda usalama wa nchi.

**Polisi:** Huchunguza ikiwa sheria na usalama wa nchi hauvunjwi.

**Dereva:** Huendesha vyombo vya nchi kavu k.v. gari au treni.

**Daktari:** Huwatibu wagonjwa.

**Hakimu:** Mtaalamu wa sheria anayeajiriwa kusikiliza mashtaka kortini na kutoa uamuzi.

**Mkunga:** Husaidia wajawazito kujifungua.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii iwe ya nyumbani. Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na majukumu ya wahusika wanaojitokeza katika mazungumzo.***

**Kazi ya 10:** ***Kazi ya utafiti au ziara ambayo ni ya kibinafsi. Watolee wanafunzi tarehe ya mwisho ya kuwasilisha kazi hii.***

**Kazi ya 11**: ***Kazi hii ni aina ya mdahalo. Ifanyike kwenye meza duara au sehemu mbili tofauti za wanafunzi lakini wanaotazamana. Kila sehemu itetee hoja zake. Ongoza majadiliano yao kwa kusisitizia adabu ya kuheshimiana kwa kutomkata kauli anayetoa hoja kabla hajamaliza.***

**Kuandika**

**Kazi ya 12**: ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Mwanafunzi wa kujitolea atoe jibu kwa kushirikiana na wenzake. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Ili uwe na cheti cha daktari unapaswa kuwa na weledi katika mchepuo wa **udaktari.**

b. Baada ya kuhitimu masomo ya **anga** mtu huweza kupatiwa cheti cha urubani.

c. Hakimu ni mfanyakazi ambaye alihitimu masomo ya **sheria**.

d. Kasisi huwa ameyazingatia masomo ya **teolojia.**

e. Keshia huteuliwa baada ya masomo ya **uhasibu.**

f. Katibu ni lazima awe na stadi katika elimu ya **uhazili.**

## SOMO LA 13: USAFI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALINI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutumia kwa ufasaha msamiati maalum kuhusu usafi wa mazingira katika mawasiliano,
- Kueleza aina mbalimbali za ugonjwa unaosababishwa na ukosefu wa usafi na jinsi ya kujilinda ugonjwa huo,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya U-ZI.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha kazi za usafi hospitalini, vifaa vinavyotumiwa katika usafi, vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Wafanyakazi wa kike na kiume ambao wamejishughulisha na usafi hospitalini,
- Vifaa vinavyotumiwa katika usafi kama vile bwelasuti, glovu, viatu maalum, fagio, deki, beseni, n.k.

**Kusoma na ufahamu: Usafi ni ufunguo wa afya nzuri**

**Kazi ya 2:** ***Tumia mbinu ya Fikiri-Jozi-Changia. Jozi inayotoa jibu sahihi ipigiwe makofi. Inayokosa jibu isahihishwe na nyingine.***

1. c

2. b

3. c

4. d

5. b

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Waweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya kamusi za Kiswahili sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Halafu, wakimaliza kueleza msamiati huu wautungie sentensi sahihi kulingana na werevu wao wa msamiati. Hapa mkufunzi atachunguza sentensi zilizotungwa ikiwa ni sahihi na kuzingatia istilahi iliyoagizwa. Mapendekezo ya maelezo:***

1. **Madimbwi:** Mahali ambapo maji yametuama; bwawa dogo.
2. **Kupiga deki:** Kupitisha kitambaa chenye majimaji kwenye sakafu ili kuondoa uchafu.
3. **Huduma**: Shughuli ambayo hufanywa kwa manufaa ya mtu au watu wengine; msaada

4. **Kuambukiz**a: Kumpa au kumletea mtu ugonjwa au kitu kibaya.
5. **Kipindupindu**: Maradhi ya kuharisha na kutapika ambayo husababishwa na uchafu.
6. **Kichaka**: Mahali penye miti mifumifupi iliyoshonana na nyasi, miba, n.k; kituka.
7. **Minyoo:** Mchango mweupe mrefu unaokaa katika tumbo la mnyama au mtu.
8. **Bwelasuti**: Vazi linalovaliwa juu ya jingine hasa kukinga uchafu wakati wa kazi; ovaroli, surupwete.

**Kazi ya 4:** ***Tumia mbinu ya fikiri-jozi-changia. Mapendekezo ya majibu ni yafuatayo:***

1. **Deki** ni kifaa chenye majimaji kinachotumiwa kuosha sakafu ili kuondoa uchafu.
2. Baada ya kujisaidia ni lazima umwage maji katika **choo.**
3. Matumizi ya maji machafu yanaweza kuwa chanzo cha kuambukizwa ugonjwa wa **kipindupindu.**
4. Kila jamii inalazimishwa kuwa na jalala la kutupia **taka.**
5. Usafi ni jambo la **kutiliwa maanani** mahali popote.

**Sarufi: Matumizi ya kauli ya kutendeshana**

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Pendekezo la jibu:***

Kiambishi –**shana** kilichoongezwa kwenye shina la kitenzi kinaleta dhana ya kauli ya **kutendeshana,** yaani mtu anakufanya utende jambo fulani, nawe unamfanya atende jambo lilo hilo.

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa mwanafunzi. Majibu:***

a. Wamepikishana chakula kitamu.

b. Tumefanyishana mambo mema ya kuieleza jamii yetu.

c. Wamelimishana shamba la maharage.

d. Mmechoreshana michoro inayoeleza wazi usawa wa kijinsia.

**Matumizi ya lugha: Msamiati kuhusu aina za magonjwa**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi ya wawili wawili kisha awaombe wajadiliane kati yao kuhusu magonjwa yanayoweza kuhatarisha maisha yao.***

**Kwa mfano:** Mafua: Maradhi ya kuambukiza yanayosababisha mgonjwa kuumwa na koo na kicwa.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8:** ***Hii ni mbinu ya mchezo wa umithilishaji. Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika katika mazungumzo husika. Kila mwanafunzi apewe jukumu lake la kuiga wakati unaokusudiwa kuwasilisha kazi hii.***

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii ni aina ya mdahalo. Ifanyike kwenye meza duara au sehemu mbili tofauti za wanafunzi lakini wanaotazamana. Kila upande utetee hoja zake. Ongoza majadiliano yao kwa kusisitizia adabu ya kuheshimiana kwa kutomkata kauli anayetoa hoja kabla hajamaliza.***

**Kuandika**

**Kazi ya 10:** ***Tumia mbinu ya fikiri-jozi-changia na kuongoza wanafunzi kujadili na kutoa maoni yao.***

**Mfano:**

- Inatubidi kuondoa vichaka karibu na nyumba kwa ajili ya kuwazuia mbu ambao husambaza ugonjwa wa malaria.
- Tumia ufagio kwa kusafisha chumba au darasa dhidi ya uchafu au vumbi.
- Kila asubuhi tunanawa usoni kabla ya kupata kifunguakinywa.
- Safisha choo baada ya haja kubwa ili nzi wasipewe fursa ya kuambukiza ugonjwa wa kipindupindu.

## SOMO LA 14: ADABU HOSPITALINI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutumia kwa ufasaha msamiati maalum kuhusu mwenendo unao takiwa katika mazingira ya hospitalini,
- Kueleza aina mbalimbali za ugonjwa unaosababishwa na ukosefu wa usafi na jinsi ya kujilinda ugonjwa huo,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia kwa usahihi kauliza vitenzi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha kazi za usafi hospitalini, vifaa vinavyotumiwa katika usafi, vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

**Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.

**Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.

**Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

**Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea katika kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.

**Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.

**Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.

**Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka karatasi kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo Mijadala.

**Kazi ya 1:** ***Mbinu ya bunguabongo itumiwe pale ambapo wanafunzi wanashirikishwa kufikiri sana na kutoa maoni tofauti. Pendekezo la majibu:***

- Kutopiga kelele hospitalini,
- Kutotema mate popote,
- Kutotupa makamasi hapa na pale.

**Kusoma na ufahamu: Utaratibu hospitalini**

**Kazi ya 2:** ***Katika makundi wanafunzi washirikishwe na kujibu maswali husika. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Darasani kati ya mwalimu na kundi la wanafunzi ambao walikuwa wanawasilisha kazi kutoka ziara yao.
2. Mbinu ya utafiti ambapo matokeo yake yaliwasilishwa darasani.
3. Kwa ajili ya kuhifadhi mazingira na kuboresha afya ya binadamu.
4. Wahusika kumi na wawili (mwalimu na wanafunzi kumi na mmoja).
5. Inawezekana kuwa ni:

- Uongozi wa hospitali,
- Daktari mkuu,
- Wizara ya Afya.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Tumia mbinu ya fikiri-jozi-changia. Jozi inayotoa jibu sahihi ipigiwe makofi, nyingine ambayo imekosa jibu isidharauliwe bali isaidiwe.***

1. D
2. H
3. A
4. I
5. E
6. J
7. C
8. F
9. B
10. G

**Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi**

**Kazi ya 4:** ***Kazi hii ifanyike katika makundi ya wanafinzi watatu watatu. Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ili kuhamasisha wanafunzi kugundua kauli ya vitenzi vilivyotumiwa. Pendekezo la jibu ni lifuatalo:***

Viambishi vilivyopigiwa mstari vinaonyesha hali ya kutendeana katika vitenzi.

**Matumizi ya lugha: Muhtasari kuhusu kauli za vitenzi**

**Kazi ya 5:** ***Unda makundi manane na kila kundi lipewe vitenzi vya kunyambua kama ifuatavyo:***

Kundi la 1: Kitenzi kufanya

Kundi la 2: Kulima

Kundi la 3: Kupiga

Kundi la 4: Kucheza

Kundi la 5: Kulipa

Kundi la 6: Kupenda

Kundi la 7: Kuomba

Kundi la 8: Kudunga

Chora jedwali ambalo limezingatia kauli zote za vitenzi na kuwaongoza wanafunzi kulijaza.

1. Kauli ya Kutenda - kitendo katika hali yake ya kawaida (bila kunyambuliwa).
2. Kauli ya Kutendea - kufanya kitendo kwa niaba (au kwa ajili) ya mtu mwingine.
3. Kauli ya Kutendana - unamfanya mtu kitendo, naye anakufanya vivyo hivyo.
4. Kauli ya Kutendeana - unafanya kitendo kwa niaba ya mtu, naye anafanya kitendo hicho kwa niaba yako.
5. Kauli ya Kutendwa - kuathirika moja kwa moja na kitendo.
6. Kauli ya Kutendewa - kitendo kufanywa kwa niaba yako au kwa ajili yako.
7. Kauli ya Kutendeka - kitendo kukamilika au kuwa katika hali timilifu.
8. Kauli ya Kutendesha- kumfanya mtu atende jambo fulani.
9. Kauli ya Kutendeshana - mtu anakufanya utende jambo fulani, nawe unamfanya atende jambo lilo hilo.

Pendekezo la majibu ni lifuatalo:

| TENDA | TENDEA | TENDANA | TENDEANA | TENDWA | TENDEWA | TENDEKA | TENDESHA | TENDESHANA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| fanya | fanyia | fanyana | fanyiana | fanywa | fanyiwa | fanyika | fanyisha | fanyishana |
| Lima | Limia | Limana | Limiana | Limwa | Limiwa | Limika | Limisha | Limishana |
| Piga | Pigia | pigana | Pigiana | Pigwa | Pigiwa | Pigika | Pigisha | Pigishana |
| cheza | chezea | chezana | chezeana | chezwa | chezewa | chezeka | chezesha | chezeshana |
| *lipa* | lipia | lipana | lipiana | lipwa | lipiwa | lipika | lipisha | Lipishana |
| penda | pendea | pendana | pendeana | pendwa | pendewa | pendeka | pendeza | pendezana |
| omba | ombea | ombana | ombeana | ombwa | ombewa | ombeka | ombeza | ombezana |
| dunga | dungia | dungana | dungiana | dungwa | dungiwa | dungika | dungisha | dungishana |

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 6: *Kazi iwe ya kibinafsi. Mwanafunzi wa kujitolea au aliyechaguliwa na mkufunzi asimame mbele ya darasa na kutoa muhtasari wa mazungumzo baina ya mwalimu na wanafunzi.***

**Mfano:**

Haya ni mazungumzo ya kundi la wanafunzi ambao walikuwa wameitembelea hospitali iitwayo Girubuzima. Ziara yao ilikuwa na lengo la kuchunguza mienendo hospitalini. Baada ya ziara yao walipewa na mwalimu fursa ya kuwasilisha matokeo ya kazi yao. Wameeleza jinsi walivyoiona miiko hospitalini ambayo ilikuwa imeandikwa kwenye ukuta wa hospitali ikiwemo kuvuta sigara, Kuchafua majengo ya hospitali na mazingira yake, kujisaidia pasipofaa, kutema mate hadharani, kupiga kelele, n.k.

**Kazi ya 7: *Hii ni mbinu ya mchezo wa umithilishaji. Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika katika mazungumzo husika. Kila mwanafunzi apewe jukumu lake la kuigiza wakati unaokusudiwa kuwasilisha kazi hii.***

**Kuandika**

**Kazi ya 8:** ***Kazi hii iwe ya nyumbani ambapo kila mwanafunzi atajitegemea au wanafunzi wawili au zaidi wanaweza kushirikiana katika kazi hii.***

## 3.6. Muhtasari wa mada

'Matumizi ya msamiati katika mazingira ya hospitali' ni mada ya tatu katika kitabu cha mwanafunzi. Imejigawa katika masomo manne ambayo ni yafuatayo:

a. Sehemu za hospitali: Msamiati kuhusu sehemu za hospitali umesisitiziwa.

b. Vifaa vya hospitalini: Somo hili limejishughulisha na matumizi ya msamiati maalum kuhusu vifaa vinavyotumiwa hospitalini.

c. Wafanyakazi wa hospitalini: Msamiati kuhusu ajira hospitalini umegusiwa.

d. Usafi katika mazingira ya hospitali: Kumetiliwa maanani msamiati kuhusu vifaa vya usafi pamoja na magonjwa yanayoweza kuambukiza.

e. Adabu katika mazingira ya hospitali: Msamiati kuhusu mwenendo mwema hospitalini umeshughulikiwa.

Ikumbukwe kuwa kila somo limezingatia sehemu kuu sita ambazo ni:

1. Kusoma na ufahamu
2. Matumizi ya msamiati maalum
3. Sarufi
4. Matumizi ya lugha
5. Kusikiliza na kuzungumza
6. Kuandika

## 3.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana haki au idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao kwa ajili ya kuimarisha shauku yao ya kuitumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

## 3.8. Tathmini ya mada ya tatu

Kazi hii iwe ya kibinafsi au ifanyiwe katika makundi madogo madogo kulingana na idadi ya wanafunzi darasani. Hakikisha kuwa vitabu pamoja na madaftari ya wanafunzi tayari yamewekwa mbali kwa ajili ya kuepuka tabia ya kuibia jaribio.

1. Vifaa angalau vinne vya hospitalini na umuhimu wake ni:
   - Sindano: kifaa cha kupenyezea dawa mwilini.
   - Machela: kifaa cha kuwabebea wagonjwa hospitalini.
   - Makasi: kifaa cha kukatia vitu mbalimbali.
   - Eksrei au uyoka ambayo ni mashine ya kutazamia viungo vya ndani ya mwili.
2. Baadhi ya sehemu muhimu za hospitali tatu na umuhimu wake ni:
   - Pambajio au sehemu ya kuwapokelea wagonjwa.
   - Chumba cha matibabu ya dharura wanamopokelea wagonjwa mahututi au wenye majeraha.
   - Wodi ya matibabu maalumu au chumba cha kushughulikia maradhi ambayo si ya kawaida kama vile maradhi ambayo yamezuka ghafla na bado hayaeleweki vizuri.
3. Kukamilisha sentensi:

i. Kazi ya muuguzi ni **kumsaidia daktari katika kazi yake.**

ii. Karani hospitalini hushughulikia **kufanya rekodi za wagonjwa.**

iii. Tabibu ni mfanyakazi wa hospitalini **anayewatibu wagonjwa.**

iv. Mfanyakazi wa hospitalini anayeshughulikia waliovunjika viungo vya mwili huitwa **mhazigi**.

v. Anayetoa huduma kwa wajawazito wakati wa kujifungua huitwa **mkunga.**

4. Hasara zinazoweza kujitokeza kwa sababu ya ukosefu wa usafi.

   a. Nzi kutoka choo huweza kuambukiza magonjwa ya aina mbalimbali kama vile kipindupindu na kuhara.

   b. Mbu huweza kujificha vichakani au madumbwini na kusababisha ugonjwa wa malaria.

5. Kasoro angalau tano ambazo zinachukuliwa kama mwiko hospitalini.

   a. Kupiga kelele katika mazingira ya wagonjwa.

b. Kuvuta sigara.

c. Kutupa taka ovyoovyo.

d. Kutema mate hadharani.

e. Kujisaidia pasipofaa.

6. Weka vitenzi vinavyopatikana katika sentensi zifuatazo katika hali ya kutendwa.

   a. Vyumba, vyoo pamoja na jikoni vimesafishwa kwa ajili ya kujilinda uchafu.

   b. Jana chakula kililiwa na wageni kwa wingi.

   c. Si vizuri kelele zipigiwe hospitalini.

   d. Maji hunywewa baada ya kuchemka.

   e. Tai huvaliwa shingoni.

## 3. 9. Kazi za ziada

### 3.9.1. Kazi za urekebishaji

Eleza maana ya wafanyakazi hawa:

Mhasibu
Bawabu
Topasi
Hamali/mpagazi

**Majibu yaliyopendekezwa:**

Mhasibu: Mtaalamu wa kuweka hesabu ya fedha.

Bawabu: Alindaye mlangoni.

Topasi: Asafishaye choo.

Hamali/mpagazi: Abebaye mizigo kwa malipo.

### 3.9.2. Kazi jumuishi

a. Jaza sentensi zifuatazo kimazungumzo:

i. Si vizuri kupiga..................hospitalini.

ii. Inakatazwa kuvuta................hospitalini.

iii. Hairuhusiwi kutupa..............mahali pasipofaa.

b. Jaza sentensi hizi kimaandishi:

i. Tunavaa glovu kwa ajili ya............................

ii. Sehemu ya hospitali ambapo wagonjwa hukaribishwa huitwa...................

iii. Usafi ni ..........................wa maisha mazuri kwa kila mtu.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

a. Kujibu sentensi kimazungumzo:

i. Si vizuri kupiga **kelele** hospitalini.

ii. Inakatazwa kuvuta **sigara** hospitalini.

iii. Hairuhusiwi kutupa **taka** mahali pasipofaa.

b. Kujaza sentensi hizi kimaandishi:

**Majibu yaliyopendekezwa:**

i. Tunavaa glovu kwa ajili ya **kujilinda uchafu.**

ii. Sehemu ya hospitali ambapo wagonjwa hukaribishwa huitwa **pambajio.**

iii. Usafi ni **msingi** wa maisha mazuri kwa kila mtu.

### 3.9.3. Kazi za nyongeza

Weka sentensi zifuatazo katika umoja au wingi:

i. Uele ule umeniogofya sana.

ii. Uso wako unametameta.

iii. Nyimbo ndizo zinaburudisha mno.

iv. Kuta ambazo zitajengwa zitafurahisha.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

i. Ndwele zile zimeniogofya sana.

ii. Nyuso zenu zinametameta.

iii. Wimbo ndio unaburudisha mno.

iv. Ukuta ambao utajengwa utafurahisha.

# MADA YA 4:

# MSAMIATI KUHUSU MAENEO YA UTAWALA

## 4. 1. Uwezo mahususi wa mada

Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika maeneo ya utawala.

## 4.2. Ujuzi wa awali

Hii ni mada ya nne katika mwaka wa kwanza, mchepuo wa lugha. Mada hii inazungumzia msamiati kuhusu maeneo ya utawala. Wanafunzi wa mwaka wa kwanza wana ujuzi wa awali kwa sababu katika shule za awamu ya kwanza (kidato cha1) walisoma katika mada ya nne «msamiati kuhusu mazingira ya utawala.»

## 4.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile uhifadhi wa mazingira, usawa wa jinsia pamoja na elimu jumuishi. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika.

## 4.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi, wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 4.5. Orodha ya masomo

| | Kicwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | WILAYA YETU | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja ngazi za utawala na viongozi wakuu wa serikali.<br>- Kuonyesha msamiati unaofaa katika maeneo ya utawala.<br>**Stadi:** Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya viongozi na ngazi za utawala.<br>- Kuchora kielelezo cha ngazi ya utawala nchini Rwanda.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu viongozi na watu wengine wanaopatikana katika maeneo ya utawala. | 5 |
| 2 | **MAKAZI YA WATU** | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja aina mbalimbali za makazi.<br>**Stadi**: Kutunga sentensi kwa kutumia aina za makazi ya watu mbalimbali.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu mipango ya serikali ya kuwajengea raia katika maeneo yasiyo hatari. | 5 |
| 3 | **SIKUKUU ZA KITAIFA** | **Maarifa na ufahamu:** Kuorodhesha sikukuu za kitaifa<br>**Stadi**: Kutumia msamiati sahihi kuhusu sikukuu za kitaifa.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kushiriki katika sikukuu za kitaifa na shughuli nyingine za kimaendeleo. | 5 |
| 4 | **AINA MBALIMBALI ZA VITAMBULISHO** | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja aina mbalimbali za vitambulisho vinavyotumiwa.<br>**Stadi:** Kutunga sentensi kwa kutumia aina mbalimbali za vitambulisho.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kudumisha amani, ushirikiano na maridhiano miongoni mwa wanajamii. | 5 |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya pili** | | | **22** |

## SOMO LA 15: WILAYA YETU

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza ngazi mbalimbali za kiutawala na viongozi wake,
- Kutoa maana ya msamiati wa kiutawala,
- Kutumia umoja na wingi wa majina ya ngeli ya U-ZI.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya ofisi na viongozi,
- Ramani inayoonyesha nchi, mikoa,wilaya, n.k.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lililivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo:**

***Kazi hii ifanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Tumia mbinu ya bunguabongo. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Katika mazingira ninamoishi kuna: Mkuu wa Kijiji, Katibu Mtendaji wa Kata na Katibu Mtendaji wa Tarafa.
- Tarehe ya 1 Februari inanikumbusha sikukuu ya Mashujaa.
- Ninajua cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha utaifa, Kadi ya bima ya afya.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi aulize wanafunzi wanachokikumbuka wanapotazama mchoro uliotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Hii ni ofisi ya wilaya.

b. Watu wanaongoja kupewa huduma kwenye Wilaya.

c. Kuna katibu ofisini.

**Kusoma na ufahamu: Ofisi za kiutawala**

**Kazi ya 2:** ***Kazi hii iwe ya kimakundi: Mkufunzi awahinize kushirikiana ili kupata majibu ya maswali ya ufahamu.***

***A. Majibu ya maswali ya ufahamu:***

1. Wahusika wanaozungumza ni **Abayo, Anezerwe na Gloriose**
2. Abayo aliamua kwenda nyumbani kwa Gloriose na Anezerwe ili kuwajulisha ziara ya rais wa jamhuri kwao ili wasikose kuhudhuria.
3. Sherehe zinatarajiwa kufanyika kijiji cha Kinini, kata ya Gitabi, tarafa ya Bwiza, wilaya Bikombe, Mkoa wa Mashariki.
4. Raia wamealikwa kuwapokea viongozi mbalimbali wakiwemo: rais wa jamhuri, mawaziri, wabunge, maseneta, gavana wa mkoa wa Mashariki, wakuu wa wilaya mbalimbali, viongozi wa tarafa, wakuu wa jeshi na polisi kwenye ngazi mbalimbali.
5. Miundombinu zilizotajwa katika kifungu cha habari ni kuanzisha mradi wa umwagiliaji, kuzindua mradi wa ukarabati wa nyumba kwa familia zilizokumbwa na mvua kali na ukarabati wa barabara ya lami.
6. Baadhi ya mienendo bora iliyotajwa katika mazungumzo ni kujiendeleza, uzalendo na ushikamano.

***B. Jaza sentensi zifuatazo kwa kutegemea mazungumzo hapo juu:***

**i.** **Abayo** ndiye alikwenda kuwaarifu **Anezerwe na Gloriose** ziara ya **rais wa jamhuri.**

ii. Ziara hii inatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi kadhaa kama vile **waziri wa elimu,wabunge, maseneta**, n.k.

iii. Lengo kuu la ziara hii ni kuanzisha miradi ya kimaendeleo kama vile **umwagiliaji**, **ukarabati wa nyumba**, n.k.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3**: ***Ambia wanafunzi katika makundi yao ya wanne wanne,watoe maana ya msamiati na kuutumia katika sentensi fupifupi. Itabidi watumie Kamusi ya Kiswahili Sanifu au mtandao. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

**Rais**: Kiongozi mkuu kabisa wa nchi ambayo ni jamhuri.

**Mbunge**: Mtu aliyechaguliwa na watu ili kuwawakilisha bungeni.

**Waziri**: Mtu anayepewa madaraka ya kusimamia na kuongoza wizara.

**Wizara:** Ni idara kuu ya serikali inayosimamia na kushughulika na mambo maalumu kwa taifa au nchi.

**Dhoruba**: Upepo wa nguvu nyingi sana, tufani, kimbunga au halibari.

**Umwagiliaji:** Usambazaji wa maji kwa mifereji au mabomba ili kulowanisha ardhi au kutia mimea maji.

**Miundombinu**: Aina ya mfumo fulani wa kitu, mahali, shirika au asasi unaowezesha shughuli fulani kufanyika kwa ufanisi kwa mfano: Mfumo wa simu au wa usafiri.

**Kazi ya 4:** ***Ambia wanafunzi waoanishe msamiati wa sehemu A na maelezo yake katika sehemu B kwa kutumia mbinu ya fikiri-jozi-changia.***

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Kijiji | Mkuu wa Kijiji |
| 2. Jeshi | Kanali |
| 3. Jamhuri | Rais |
| 4. Kata | Katibu mtendaji wa Kata |
| 5. Mkoa/jimbo | Gavana |
| 6. Bunge | Mbunge |
| 7. Wilaya | Meya |
| 8. Tarafa | Katibu mtendaji wa Tarafa |
| 9. Wizara | Waziri |

**Kazi ya 5**: ***Waambie wanafunzi wajaze akili ramani ifuatayo na kutoa mikoa yote ya nchi ya Rwanda. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Mikoa ya Rwanda: Jimbo la Magharibi, Jimbo la Mashariki, Jimbo la Kusini, Jimbo la Kaskazini na Mji wa Kigali.

b. Mkufunzi aombe wanafunzi kuorodhesha wilaya zote zilizomo katika kila mikoa.

**Mfano:** Jimbo la Mashariki linaundwa na wilaya ya Ngoma, Kirehe, n. k.

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI**

**Kazi ya 6**: ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kueleza mabadiliko ya kisarufi yaliyojitokeza katika sentensi husika.***

**Pendekezo la jibu :**

Sehemu moja inaonyesha majina katika umoja ambayo kiambishi nafsi chake ni “**u-**”. Sehemu ya pili inaonyesha wingi wa majina ya sehemu A ambayo kiambishi nafsi chake ni “**zi-**”. Ndiyo sababu ya ngeli hii kuitwa ngeli ya **U-ZI**.

**Kazi ya 7:** ***Katika jozi, ongoza wanafunzi kujaza jedwali hili kwa kuweka sentensi zilizomo katika umoja au wingi.***

| | Sentensi katika umoja | Sentensi katika wingi |
|---|---|---|
| *1* | Ukurasa huu umeandikwa na Yusufu. | Kurasa hizi zimeandikwa na Yusufu. |
| *2* | Utepe unatumiwa kupima urefu wa vitu au watu. | Tepe zinatumiwa kupima urefu wa vitu au watu. |
| *3* | Waya huu unatumiwa katika kazi ya umeme. | Nyaya hizi zinatumiwa katika kazi za umeme. |
| *4* | Wembe wangu utakata nguo zote. | Nyembe zetu zitakata nguo zote. |
| *5* | Waadhi huu ni wa mnyama gani? | Nyaadhi hizi ni za wanyama gani? |

**Kazi ya 8**: ***Omba wanafunzi wajaze sentensi kwa kutumia jibu sahihi katika mabano kama ilivyoagizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa wanafunzi. Majibu yaliyopendekezwa :***

1. huu
2. hizo
3. ule
4. huo
5. hizi

**Kazi ya 9**: ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari kilichomo katika kitabu chao na kueleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari. Mapendekezo ya jibu:***

Maneno “wenyewe” na “zenyewe” ni vivumishi vya pekee vyenye dhana ya kurejesha katika ngeli ya U-ZI kwa sababu vina uaminifu wa kulirejea jina lile linalowakilishwa. Wenyewe hutumiwa katika umoja na zenyewe hutumiwa katika wingi.

**Matumizi ya lugha: Ngazi za utawala**

**Kazi ya 10**: ***Ambia wanafunzi wajadili maswali yaliyomo katika kitabu cha mwanafunzi. Waambie wajibu katika makundi ya wanafunzi wanne wanne au watano watano kufuatana na idadi ya wanafunzi waliomo darasani. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Jamhuri-Mkoa-Wilaya-Tarafa-Kata-Kijiji.
- Jamhuri→ Rais,
- Mkoa→Gavana,
- Wilaya→ Meya,
- Tarafa→ Katibu mtendaji wa tarafa,
- Kata →Katibu mtendaji wa kata na
- Kijiji→ Mkuu wa kijiji

**Kazi ya 11:** ***Ambia wanafunzi waoanishe sehemu A na sehemu B. Kazi hii waifanye katika jozi.***

| A (Ngazi za utawala) | B (Viongozi) |
|---|---|
| 1. Kijiji | Mkuu wa kijiji |
| 2. Kata | Katibu mtendaji wa kata |
| 3. Tarafa | Katibu mtendaji wa tarafa |
| 4. Wilaya | Meya au Mkuu wa wilaya |
| 5. Mkoa/jimbo | Gavana au Mkuu wa Jimbo/Mkoa |

**Kazi ya 12:** ***Katika jozi, ambia wanafunzi wakamilishe sentensi wanazoziona kitabuni.***

1. Karongi ni mojawapo ya wilaya zinazouunda mkoa wa Magharibi.
2. Rais wa jamhuri ya Rwanda alihutubia raia wote.
3. Nishati, umeme, ukarabati wa barabara ni baadhi ya miundombinu.
4. Gavana ni kiongozi mkuu wa mkoa.
5. a. Idadi fulani ya Kata inaunda tarafa.

   b. Jamhuri ya Rwanda inaongozwa na rais.

   c. Rwanda imegawanyika katika mikoa ifuatayo : Mashariki, Magharibi, Kaskazini, Kusini na Mji wa Kigali.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 13:** ***Saidia wanafunzi kujenga makundi kisha uwaombe kuigiza mazungumzo kuhusu kifungu walichosoma awali "Ofisi za kiutawala" baina ya Abayo, Baba, Gloriose na Anezerwe. Watumie michezo ya umithilishaji. Mkufunzi asisitizie sana kuhusu matamshi bora na matumizi ya ishara katika uigizaji wao wanapokosea wasahihishwe na wenzao wakiongozwa na mkufunzi***

**Kazi ya 14:** ***Kwanza mkufunzi awape wanafunzi muda wa kufanya utafiti kuhusu kazi hii, kisha aombe wanafunzi wasimulie mbele ya darasa walichojifunza katika ziara yao kwenye kituo cha utawala kilichoko karibu nao. Mkufunzi asisitizie sana kuhusu matamshi bora na matumizi ya ishara katika uigizaji wao wanapokosea wasahihishwe na wenzao wakiongozwa na mkufunzi. Kazi hii iwe ya nyumbani.***

**Kazi ya 15:** ***Ambia wanafunzi wajitambulishe kwa wenzao kwa kuzingatia maeneo ya utawala wanamoishi pamoja na viongozi wake. Hapa ni namna ya kumwezesha mwanafunzi kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza, na kuzingatia msamiati kuhusu mada iliyofundishwa.***

**Kuandika**

**Kazi ya 16:** ***Mkufunzi aombe wanafunzi kutunga mazungumzo kati ya raia mmoja na kiongozi wilayani juu ya huduma ya kuomba kitambulisho fulani. Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea baina ya wanafunzi.***

**Kazi ya 17:** ***Ambia wanafunzi watunge kifungu cha habari kifupi kwa kutumia msamiati ulioko katika kitabu chao.***

**Kielelezo:**

Sifa na Solange ni mabinti wawili wakazi wa nchi yetu katika Mkoa wa Kusini. Mwaka jana walishiriki katika kazi za Umuganda kumjengea nyumba Bi. Mukamana aliyenusurika mauaji ya kimbari dhidi ya watutsi mwaka 1994. Kazi hizi za Umuganda zilifanyika katika wilaya yetu, tarafa ya Izuba, kata ya Buhoro na kijiji cya Isimbi. Nyumba hii ilijengwa vizuri na viongozi wengi walikuwepo. Mwishoni, waliokuwa wameshiriki wote walipongezwa na katibu mtendaji wa tarafa akawaomba kujitafutia suluhu wenyewe kwa shida mbalimbali.

## SOMO LA 16: MAKAZI YA WATU

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutaja aina mbalimbali za makazi,
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia aina za makazi ya watu mbalimbali,
- Kutumia kwa ufasaha ngeli ya U-ZI katika sentensi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya ofisi na viongozi,
- Ramani inayoonyesha nchi, mikoa, wilaya, n.k.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, ambapo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili

mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1**: ***Kwa kutumia mbinu ya bunguabongo, ambia wanafunzi wachunguze mchoro uliopo kitabuni na kufafanua kama wanayoyaona yanahusiana na makazi. Jibu lililopendekezwa:***

Mchoro huu unahusiana na makazi ya watu kwani unaonyesha majengo mengi yanayoonekana kama mji.

**Kusoma na ufahamu: Makazi ya watu**

**Kazi ya 2:** ***Ambia wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu baada ya kusoma kifungu cha habari. Haya watayajibu katika makundi darasani. Majibu:***

1. Ni nyumba zilizojengwa kwenye maeneo bora. Yaani yasiyoweza kumletea mtu shida.
2. Maeneo hayo ni yale yanayoweza kuhatarisha maisha ya Mnyarwanda: K.m: vinamasini, mabondeni, milimani, kando ya mito na maziwa, n.k.

3. Serikali iliwahamishia katika maeneo salama na ikawasaidia kujenga nyumba na kuwaletea karibu miundombinu ili kurasisha maisha yao.
4. Umeme, maji safi, viwanda kadhaa, hospitali, barabara za lami, n.k.
5. Mmomonyoko wa ardhi husababishwa na mvua nyingi na kazi mbalimbali za binadamu za kutojali mazingira yake, k.v. kukata miti, kuchoma mapori, uchungaji wa ng'ombe, kuchimba madini, n.k.
6. Makazi ya mjini ni mazuri kwani kuna aina kadhaa za miundombinu inayorahisisha maisha kwa binadamu lakini yale ya kijijini hayana miundombinu ya kutosha.
7. Omba wanafunzi waseme **NDIYO** au **HAPANA** kwa sentensi zilizotolewa katika kitabu cha wanafunzi:
   a. Ndiyo.
   b. Hapana.
   c. Ndiyo
   d. Hapana.

**Msamiati kuhusu makazi**

**Kazi ya 3:** ***Ambia wanafunzi wafafanue maneno waliyo nayo katika kitabu; wawili kwa wawili washirikiane:***

a. **Nyumba:** Jengo ambalo mtu huishi au hifadhi ya mwanadamu.

b. **Bondeni:** Sehemu ya ardhi iliyo kati ya vilima viwili.

c. **Mmomonyoko wa ardhi:** umegukaji wa ardhi unaosababishwa na kutiririka kwa maji.

d. **Kinamasi:** Sehemu ya matope au utelezi.

e. **Mjini:** Makazi ya watu wengi kulikojengwa nyumba nyingi na kunakofanyika shughuli mbalimbali.

**Kazi ya 4:** ***Katika jozi, ambia wanafunzi waoanishe maneno katika kundi A na maana yake katika kundi B.***

| | A: Maneno | B: Maana |
|---|---|---|
| 1 | Umeme | Mtu aliye na haki za kisheria za kuwa mkazi katika nchi fulani. |
| 2 | Ziwa | Sura ya nchi iliyoko baina ya milima. |
| 3 | Raia | Mji mkubwa wenye watu wengi na miundombinu kadhaa. |
| 4 | Mabonde | Eneo kubwa lenye maji lililozungukwa na nchi kavu. |
| 5 | Jiji | Nguvu ya vitu kama betri au jenereta inayopitia katika waya na kutoa moto au mwangaza. |

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI**

**Kazi ya 5** : ***Katika jozi, ambia wanafunzi watazame sentensi vitabuni mwao na kujadili mabadiliko ya kisarufi yaliyojitokeza:Majibu yaliyopendekezwa***:

Maneno **mmoja, mbili, tatu, nne** na **chache**. ni vivumishi vya idadi katika ngeli ya U-ZI, kwa sababu vinaonyesha idadi au hesabu ya vitu.

**Kazi ya 6**: ***Katika jozi, ambia wanafunzi waweke katika umoja au wingi sentensi ambazo wanazisoma katika kitabu chao. Majibu yaliyopendekezwa:***

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ukuta mmoja umejengwa leo. | Kuta mbili zimejengwa leo. |
| Uso mmoja utatibiwa kesho. | Nyuso nyingi zitatibiwa kesho. |
| Ukucha mmoja wa Solange ni mrefu. | Kucha chache za solange ni ndefu. |

**Kazi ya 7**: ***Ambia wananfunzi wajaze nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kivumishi kinachofaa. Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa wanafunzi. Mapendekezo ya majibu:***

a. Upondo <u>mmoja</u> umeweka ndani ya mtumbwi.

b. Petro aliandika kurasa <u>tano</u>.

c. Umutoni na Abayo walipokea fagio <u>nyingi</u> siku ile.

d. Mtoto huyu aliwaandikia wazazi wake nyaraka nyingi katika muhula wa tatu.

e. Wembe mmoja ulimkata kidole.

**Matumizi ya lugha: Makazi ya watu**

**Kazi ya 8:** ***Mkufunzi atumie makundi ya wanafunzi watano watano ili wajadili maswali waliyopewa. Mapendekezo ya majibu:***

a. Makazi ni muhimu sana kwa binadamu:

**Kilelezo:** Makazi hutusaidia kuishi vyema kwa kutulinda mvua, upepo, wadudu na wanyama mbalimbali wanaoweza kuathiri maisha yetu. Bila makazi…….

b. Serikali ya Rwanda iliwakataza raia kujenga na kuishi katika maeneo ya hatari. Serikali ilifanya hivi ili kuwalinda raia wasije wakapoteza maisha yao kutokana na hali ya mazingira isiyo nzuri hapo.

**Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu makazi**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi awaambie wanafunzi wazungumzie wenzao umuhimu wa kuishi katika maeneo yasiyo ya hatari. Kazi hii ifanyike katika jozi.***

**Kazi ya 10:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi katika majadiliano yao yanayohusu picha au video walizoziona zinazohusu makazi nchini Rwanda hasa hasa mji wa Kigali. Mbinu ya fikiri-jozi-changia itumiwe katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.***

**Kuandika: Utungaji wa insha kuhusu makazi**

**Kazi ya 11:** ***Kazi hii iwe ya nyumbani. Ambia wanafunzi watunge insha yenye aya 3 (Maneno yasiyopungua mia moja) wakieleza umuhimu wa kuishi katika maeneo yasiyo ya hatari. Hapa mkufunzi asisitizie namna ya kuepukana na makosa ya kiotografia, ya kisarufi, namna ya kuandika insha (utangulizi, kiini cha ujumbe na hitimisho) na matumizi ya lugha kwa ujumla.***

## SOMO LA 17: SIKUKUU ZA KITAIFA

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kuorodhesha sikukuu za kitaifa,
- Kutumia msamiati sahihi kuhusu sikukuu za kitaifa,
- Kutumia umoja na wingi wa majina ya ngeli ya U-ZI.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya ofisi na viongozi,
- Ramani inayoonyesha nchi, mikoa, wilaya, n.k.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mukufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.

- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo Mijadala.

**Kusoma na ufahamu: Sikukuu za kitaifa**

**Kazi ya 1:** ***Kazi hii ifanyike katika makundi. Majibu ya maswali ya ufahamu:***

1. Krismasi
2. Ni mwalimu ambaye alituuliza sababu ya sherehe tulizokuwa nazo.
3. Ni kwenye tarehe 1 Mei kila mwaka.
4. Idi, Pasaka na Ijumaa takatifu, n.k.
5. Fursa ya kukutana na wananchi, kuwajulisha mipango ya serikali, pia hupata fursa ya kupumzika na kuwatembelea jamii na marafiki.

**Msamiati kuhusu sikukuu za kitaifa**

**Kazi ya 2:** ***Waongoze wanafunzi kueleza maneno yaliyomo katika kitabu chao wakiyahusisha na kifungu walichokisoma. Baadaye, wayatumie maneno hayo katika sentensi kamili. Utumiaji wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu uwasaidie pale panapohitajika. Mapendekezo ya majibu:***

1. **Krismasi:** Sherehe za kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Yesu kristo kama wanavyoamini Wakristo, pia Noeli.
2. **Mashujaa**: Watu wenye ujasiri, watu ambao huweza kukabili mambo ya hatari bila hofu.
3. **Kukomboa:** Kutoa mtu katika hali ya kukandamizwa, kudhulumiwa au kutawaliwa na mtu mwingine au nchi nyingine.
4. **Kimbari:** Enye kutenga mbari za watu k.m. rangi, kabila, dini, taifa, ukoo, n.k.
5. **Fursa**: Nafasi ya kufanya jambo fulani,wasaa.

**Kazi ya 3:** ***Ambia wanafunzi wajaze sentensi kwa kutumia msamiati waliopewa kitabuni: uhuru, Idi, wafanyakazi, mashujaa, kimbari. Kazi hii ifanyike katika jozi au katika makundi.***

1. Katika mwezi wa Februari sisi husherehekea sikukuu ya mashujaa lakini ile ya uhuru/ukombozi wa taifa ni mwezi wa Julai.
2. Mauaji ya kimbari nchini Rwanda yaliacha watu wengi bila makazi.
3. Majeshi ya RPF Inkotanyi yaliwahi kuikomboa nchi ya Rwanda mnamo mwaka wa 1994.
4. Idi huanza kulingana na kalenda ya waislamu.
5. Kwenye sikukuu ya Krismasi, wao walikula chakula kizuri sana.

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI na vivumishi vya sifa**

**Kazi ya 4:** ***Omba wanafunzi watazame sentensi walizo nazo kitabuni na kueleza maneno yaliyopigiwa kistari: Hapa mkufunzi huweza kutumia mbinu ya fikiri-jozi-changia. Jibu lililopendekezwa:***

Maneno yaliyopigiwa kistari ni vivumishi vya sifa katika ngeli ya U-ZI kwani vinataja tabia au namna vitu vilivyo au vinavyoonekana.

**Kwa mfano** : mpya, nzuri, mbaya, mzito, nzito, n.k.

**Kazi ya 5:** ***Ambia wanafunzi wajaze nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kivumishi wanachokitoa mabanoni. Mkufunzi aongoze mchakato wa ujifunzaji na kuchangia pale inapohitajika. Mapendekezo ya majibu:***

a. Ukucha wake **mbaya** umekatwa na Ahirwe.

b. Mbwa huyu ana nyayo **safi.**

c. Kalisa aliandika kurasa **ndefu.**

d. Ufunguo **mdogo** umepotea njiani.

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa wanafunzi. Omba wanafunzi waandike sentensi mbili zenye vivumishi vya sifa vinavyoonyesha tabia na nyingine mbili za vivumishi vya sifa vinavyoonyesha jinsi vitu vilivyo au vinavyoonekana. Majibu yaliyopendekezwa:***

| Vivumishi vya sifa vinavyoonyesha jinsi vitu vilivyo au vinavyoonekana | Vivumishi vya sifa vinavyoonyesha tabia |
|---|---|
| 1. Kurasa ndogo zimeishaandikwa. | 1. Kuta zilizoko ni mbovu. |
| 2. Ukuta mrefu utajengwa kesho. | 2. Nikuze anaonyesha uso mnyamavu kweli. |

**Matumizi ya lugha: Sikukuu za kitaifa**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi abandike flip chati kwenye ubao na kuwaomba wanafunzi kuchagua na kupanga maneno katika kundi A la sikukuu zinazobadili tarehe au kundi B ambalo linahusisha sikukuu zisizobadili tarehe.***

**A**

Sikukuu ya mashujaa

Sikukuu ya ukombozi wa taifa

Sikukuu ya uhuru wa taifa

Sikukuu ya watakatifu wote

Krismasi

Sikukuu ya kazi ulimwenguni

**B**

Idi

Pasaka

**Kusikiliza na kuzungumza: Sikukuu za kitaifa**

**Kazi ya 8:** ***Omba wanafunzi wajadiliane kuhusu sikukuu za kitaifa na kutoa matokeo yao hadharani. Kazi hii ifanyike katika makundi na kila kundi liwasilishe matokeo yao hadharani.***

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kukuza stadi za kuzungumza kwa wanafunzi. Kila mwanafunzi asimulie mbele ya hadhira sikukuu aliyoisherehekea siku moja au zaidi, na kueleza jinsi ilivyokuwa.***

**Kuandika**

**Kazi ya 10:** ***Wanafunzi wapewe kazi ya nyumbani na kutunga kifungu cha habari kuhusu sikukuu fulani aliyoisherehekea siku moja au zaidi na kuonyesha vile alivyoona pale.***

## SOMO LA 18: AINA MBALIMBALI ZA VITAMBULISHO

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutaja aina mbalimbali za vitambulisho,
- Kutunga sentensi kwa kutumia aina mbalimbali za vitambulisho,
- Kutumia kwa ufasaha ngeli ya U-ZI.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyomsaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya ofisi na viongozi,
- Ramani inayoonyesha nchi, mikoa, wilaya, n.k.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa

kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

*iv.* ***Majibu:*** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali majidiliano lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kusoma na ufahamu: Ombi la vitambulisho**

**Kazi ya 1:** ***Hapa, mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi ya watu watatu kisha wawasilishe majibu yao mbele ya darasa. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Kwenye ofisi ya tarafa.
2. Kutafuta vitambulisho mbalimbali.
3. Aliwapokea vizuri ofisini mwake na kuwahudumia.
4. Kwenye mtumishi wa mtandao wa kiteknolojia Irembo.
5. Ni kwa nyanja ya kiteknolojia.

**Msamiati kuhusu aina ya vitambulisho**

**Kazi ya 2:** ***Katika makundi, mkufunzi awaongoze wanafunzi kutoa maana ya msamiati ulio katika kitabu cha mwanafunzi, kisha watunge sentensi sahihi. Kamusi ya Kiswahili Sanifu itumiwe pale inapohitajika. Majibu yaliyopendekezwa:***

**i.** **Cheti:** Karatasi au hati anayopewa mtu kuthibitisha jambo fulani.

**Mfano**: Mugisha alipoteza **cheti** chake cha uraia alipokuwa safarini.

ii. **Ofisi:** Chumba ambacho wafanyakazi hukaa na kuhudumia watu.

**Mfano: Ofisi** ya Rais wa Rwanda iko mjini Kigali.

iii. **Huduma:** Shughuli ambayo hufanywa kwa manufaa ya mtu au watu wengine au mambo ambayo ni muhimu kwa maisha ya binadamu k.m hospitali, maji, usafiri, n.k.

**Mfano**: Utoaji wa **huduma** nzuri huchangia katika maendeleo ya nchi.

iv. **Kibali:** Ruhusa inayotolewa ili kufanyika kwa jambo fulani, idhini.

**Mfano**: Nani kakupa **kibali** cha kuingia hapa?

v. **Kuambatana:** Kuwa pamoja, kufuatana, kushirikiana

**Mfano:** Ni lazima barua ya muombaji kazi **kuambatana** na wasifu-kazi yake.

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kujaza sentensi kwa kutumia msamiati unaofaa: Majibu yaliyopendekezwa:***

i. Nilipoingia kazini ilinibidi nitafute cheti cha kuzaliwa.

ii. Mujawase ataulizwa pasipoti kabla ya kuenda nchini Ujerumani.

iii. Katibu mtendaji wa tarafa anawapa raia huduma nzuri sana.

iv. Ofisi ya wilaya yetu inapatikana mbali na nyumba yangu.

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI na vivumishi vya kumiliki**

**Kazi ya 4:** ***Kwa kutumia makundi, mkufunzi awaongoze wanafunzi kutazama sentensi hizi na kujadili mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza. Majibu yaliyopendekezwa:***

Sentensi hizi zina vivumishi **vya kumiliki** katika ngeli ya U-ZI. Katika umoja U- imetumiwa na kwa wingi zi- imetumiwa kufuatana na upatanisho wa kisarufi. Maneno «wake, zao, wangu na zetu» ni vivumishi vya kumiliki kwani yanajulisha umiliki wa nomino.

**Kazi ya 5:** ***Katika jozi, waelekeze wanafunzi wajaze sentensi kwa kutumia vivumishi vya kumiliki vinavyofaa kulingana na kiambishi cha nafsi ambacho kimeandikwa katika mabano. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Ukucha …wake……umerefuka sana.

2. Uzi ……wetu……..ni mweusi sana.
3. Kazeneza na Mwami waliibiwa funguo …zao….zote.
4. Usikose kupaka rangi ukuta …wako..ule kwani umechafuka sana.

**Kazi ya 6:** ***Ongoza wanafunzi wasome kifungu cha habari na kueleza matumizi ya maneno yaliyopigwa kistari. Mkufunzi atumie mbinu ya fikiri-jozi-changia. Majibu yaliyopendekezwa:***

Maneno yaliyopigiwa kistari ni vivumishi vya kuuliza. Hili ni kundi la maneno yatumiwayo kuulizia maswali.

**Mfano:**

**Umoja**

Ukuta **upi/gani** ulijengwa?

**Wingi**

Kuta **zipi/gani** zilijengwa?

**Kazi ya 7:** ***Ongoza wanafunzi kuuliza maswali matatu wakitumia vivumishi*** *–pi* ***au*** *gani* ***katika ngeli ya U-ZI. Kazi hii iwe ya kibinafsi. Mapendekezo ya majibu:***

a. Ukurasa gani umesomwa?
b. Kumbi zipi zimejengwa?
c. Wembe upi umemkata kidole cha mkono?

**Kazi ya 8:** ***Ongoza wanafunzi kujaza sentensi wakitumia kivumishi cha kuuliza kinachofaa. Mapendekezo ya majibu:***

i. Uwineza alichukua funguo…zipi/gani….?
ii. Mchana huo, Dusabe aliambiwa habari…gani/zipi…..?
iii. Ni wembe…upi/gani ambao binti yangu atauleta?
iv. Tumbili wanapenda kuparamia ukuta…upi…?
v. Karatasi …zipi/gani…..zilitengenezwa katika miti ya kwetu?

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 9:** ***Katika makundi ya wanafunzi watano watano, mkufunzi awaongoze wanafunzi kujibu maswali waliyopewa na kila kundi liwasilishe mbele ya darasa matokeo yao. Mapendekezo ya majibu:***

1. Raia wanaweza kupata Pasipoti, cheti cha kuzaliwa, Cheti cha

ndoa na leseni ya udereva kwenye mtandao wa kiteknolojia IREMBO.

Au kuzifikia ngazi za kiutawala zifuatazo: paspoti, cheti cha kuzaliwa na cheti cha ndoa vyote kwenye ofisi ya tarafa. Lakini kwa pasipoti lazima uendelee mpaka wilayani ndipo utakapomkuta afisa mtendaji wa waingiao na watokao nchini. Na leseni ya udereva utaenda kwenye ofisi ya polisi inayohusika na mambo ya vyeti vya udereva.

2. Atamjulisha kiongozi anayehusika kwenye ngazi ya kijiji, kata, tarafa na hata ngazi za polisi vilevile.
3. Ndiyo. Mtu yeyote anayetumia kitambulisho chochote kinyume na sheria lazima aadhibiwe kwa sababu serikali imeandaa kanuni zote za utumiaji wa vitambulisho ili kulinda madhara yoyote yanayoweza kujitokeza. Kukiuka kanuni za serikali ni kosa kubwa.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 10: *Mkufunzi awaongoze wanafunzi kuzungumzia matumizi ya kitambulisho cha kitaifa kilichotajwa. Hapa mkufunzi atumie mbinu ya mjadala:***

**Umuhimu:**

Kitambulisho cha kitaifa kinasaidia kumtambua mhusika kwa urahisi anapohitaji kuduma katika taasisi mbalimbali.

Kitambulisho cha taifa kinamsaidia mtu kupata stahili zake za jamii k.v. kupata malipo ya pensheni, haki za matibabu, n.k.

**Hasara**

Anaweza kukosa huduma, haki tafauti za kila raia k. v. kupiga kura, kupata pasipoti, n. k.

**Kuandika**

**Kazi ya 11**: ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kuandika umuhimu wa vitambulisho vya kitaifa wakitumia maneno yasiyopungua 100. Kazi hii iwe ya nyumbani na kibinafsi.***

## 4.6. Mhutasari wa mada:

Mada hii ya nne **"Matumizi ya Kiswahili katika maeneo ya utawala"** ina masomo makuu manne yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: Kusoma na ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza pamoja na kuandika. **Somo la kwanza** linaeleza ngazi za utawala na viongozi wakuu wa serikali. **Somo la pili** ni makazi ya watu na linahusu aina mbalimbali za makazi. **Somo la tatu** ni sikukuu za kitaifa na matumizi yake. **Somo la nne** ambalo ni la mwisho linahusu aina ya vitambulisho vinavyotumiwa nchini. Katika kila somo kuna kipengele cha sarufi ambacho kinagusia matumizi ya ngeli ya U-ZI.

## 4.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana haki au idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao kwa ajili ya kuimarisha shauku yao ya kuitumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

## 4.8. Tathmini ya mada ya nne

Patia wanafunzi maswali ya tathmini ya mada ya nne. Kila mwanafunzi ajibu maswali mwenyewe katika daftari lake.

**Majibu ya tathmini ya mada ya 4:**

1. Rais
2. a) Ukuta **mmoja** ulioanguka ulikuwa haukujengwa vizuri.

   b) Habimana hakuvunja ufunguo **mdogo**.

   c) Nyuzi zao ni nyeusi na nyekundu pia.
3. Majina ya kiutawala yanayotumiwa kwa viongozi wa:

   a) wilaya→Meya   b) kijiji→Mkuu wa kijiji

   c) Tarafa→Katibu mtendaji wa tarafa
4. Aina tano za vitambulisho vya kitaifa: pasipoti, cheti cha kuzaliwa, cheti cha kulipa kodi, cheti cha kufariki, leseni ya udereva, n.k.

5. Kupata muda wa kuhutubia raia ili kuwajulisha mipango ya serikali pia ni fursa ya kupumzika.
6. Vitambulisho vya Taifa ni chachu ya maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa.

- Vinasaidia kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.
- Vinasaidia kumtambua mhusika kwa urahisi anapohitaji kupatiwa huduma katika taasisi mbalimbali kama vile benki, taasisi za mikopo na huduma za afya.
- Vitarahisisha kuwatambua wakwepaji wa kurejesha mikopo kutoka kwenye benki na asasi mbalimbali za fedha nchini.
- Vitasaidia kuweka kumbukumbu za matukio ya uhalifu katika daftari la kumbukumbu la kielektroniki.

## 4.9. Kazi za ziada

### 4.9.1. Kazi za urekebishaji

a. Taja angalau ngazi tatu za utawala unazozijua na huduma zinazotolewa hapo.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

- Tarafa: Hutoa vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya ndoa, n.k
- Wilaya: Hutoa pasipoti
- Polisi: Hutoa leseni za udereva

b. Eleza umuhimu wa vitambulisho kwa taifa.

**Pendekezo la majibu:**

Vitambulisho vya taifa ni chachu ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

### 4.9.2. Kazi jumuishi

Weka sentensi zifuatazo katika umoja au wingi.

a. Ukurasa ulioandikwa na Bi. Amina unasomeka vizuri.

b. Waraka ambao umemfurahisha aliutunza vizuri.

c. Uzi uliotumiwa kushonea nguo umemalizika.

d. Unyasi huu umekauka maji.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

a. Kurasa zilizoandikwa na Bi. Amina zinasomeka vizuri.

b. Nyaraka ambazo zimewafurahisha walizitunza vizuri.

c. Nyuzi zilizotumiwa kushonea nguo zimemalizika.

d. Nyasi hizi zimekauka maji.

### 4.9.3. Kazi za nyongeza

Jadili hasara za kutokuwa na vitambulisho vya kitaifa kwa mwananchi.

**Pendekezo la jibu:**

Mwananchi asiyekuwa na vitambulisho vya taifa anaweza kukosa huduma zinazopewa raia k.v. kunyimwa pasipoti, leseni ya udereva ama viza.

# MADA YA 5:

## MSAMIATI KUHUSU MAZINGIRA YA KIBIASHARA

### 5.1. Uwezo mahususi wa mada

Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika shughuli za kibiashara.

### 5.2. Ujuzi wa awali

Katika shule za awamu ya kwanza (kidato cha 1 mada ya tano) wanafunzi walisoma katika mada ya pili « Msamiati kuhusu mazingira ya biashara. »

### 5.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile uhifadhi wa mazingira, usawa wa jinsia pamoja na elimu jumuishi. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzikatika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika.

### 5.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa mkufunzi kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 5.5. Orodha ya masomo

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, Stadi, maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **1. Mawasiliano sokoni** | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza shughuli tofauti za kibiashara zinazofanyika sokoni.<br><br>**Stadi:** Kutumia msamiati wa mazingira ya biashara kwa usahihi katika mawasiliano rahisi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha heshima kati ya wateja na wanunuzi. | 7 |
| 2.**Majadiliano dukani** | **Maarifa na ufahamu:** Kutoa aina za bidhaa zinazouzwa dukani.<br><br>**Stadi**: Kutumia kwa ufasaha msamiati wa kibiashara katika kujadiliana bei.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha heshima kati ya wateja na wanunuzi. | 7 |
| 3. **Matumizi bora ya mizani** | **Maarifa na ufahamu:** Kuonyesha mwenendo au maadili mema ya kutumia mizani bora katika biashara.<br><br>**Stadi**: Kutumia kwa ufanisi mizani katika hesabu za biashara.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu sheria zilizowekwa na nchi kuhusu shughuli za kibiashara. | 6 |
| **Tathmini ya mada** | | **2** |
| **Vipindi vya mada yote** | | 22 |

## SOMO LA 19: MAWASILIANO SOKONI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kubainisha shughuli tofauti za kibiashara na manufaa yake,
- Kutumia kwa ufasaha msamiati maalum wa mazingira ya sokoni katika majadiliano ya bei,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya I-ZI.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha jengo la soko, michoro ya vibanda na bidhaa sokoni, na wauzaji na wanunuzi, vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo**: Hii ni mbinu ambayo kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri - jozi - changia**: Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi**: Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi

huongoza uwasilishaji huo na kusahihisha ama kurekebisha pale panapohitajika.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo**

***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Mapendekezo ya majibu***

Baadhi ya msamiati unaotumiwa katika biashara ni:

- **Bei**: Kiwango cha pesa kununulia au kuuzia bidhaa au huduma fulani.
- **Faida**: Pato libakialo baada ya kuondoa gharama za kufanya biashara k.v. ununuzi na usafirishaji.
- **Hasara**: Ukosefu wa faida; hali ya kupoteza pato au mali katika biashara.
- **Mteja**: Mtu aendaye kununua bidhaa au huduma.
- **Muuzaji**: Mtu mwenye kuuza vitu kama vile dukani au sokoni.
- **Mnunuzi**: Mtu anayepata kitu kwa kulipa kwa pesa.
- **Bidhaa**: Vitu vinunuliwavyo na kuuzwa.

- **Faranga**: Fedha zinazotumiwa katika nchi k.v. Ufaransa na katika nchi zilizokuwa zikitawaliwa na Ubelgiji na Ufaransa.
- **Kibanda**: Kijumba kidogo kinachotumiwa kwa shughuli za biashara sokoni.

**Kazi ya 1:** ***Katika makundi, mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo kila mwanafunzi anapewa fursa ya kutoa maoni yake. Mapendekezo ya majibu:***

- Kuna soko ambalo hutumiwa kuuzia na kununulia vitu tofauti,
- Kuna vibanda ambapo pametandikwa bidhaa za aina aina,
- Kuna wanunuzi ambao wanajadiliana bei na wauzaji.

**Kusoma na ufahamu: Safari ya Niwemwiza na Kayigi sokoni**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo na kuwaongoza katika majadiliano yao. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

a. Mama yake na Niwemwiza na Kayigi aliwatuma vifaa tofauti vya shule na bidhaa nyingine za kutumia nyumbani.

b. Kayigi na Niwemwiza walinunua madaftari na kalamu kwenye kibanda cha vifaa vya shule.

c. Walishangazwa na kuona watu wengi wa marika tofauti wakijaa sehemu zote za soko.

d. Alikuwa anahofu kupata hasara.

e. Kwa sababu walitumia pesa vizuri na kutokawia sokoni.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya Kamusi za Kiswahili Sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

**a. Faida**: Pato libakialo baada ya kuondoa gharama za kufanya biashara k.v. ununuzi na usafirishaji.

**b. Bei ghali**:-enye bei kubwa, siyo rahisi kwa mnunuzi.

**c. Kununua**: Kutoa fedha ili kupata kitu kinachouzwa.

**d. Kuuza**: Kubadilisha kitu kwa fedha.

e. **Bucha**: Duka la nyama

f. **Hasara**: Ukosefu wa faida; hali ya kupoteza pato au mali katika biashara.

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI**

**Kazi ya 4: *Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo na kuwaongoza katika majadiliano yao kuhusu mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza. Pendekezo la jibu:***

Sentensi zote zilizo katika umoja, upatanisho wa kisarufi kati ya jina na kitenzi unaonyesha kuwa majina haya yanatumia kiambishi nafsi "I" wakati ambapo katika wingi kiambishi nafsi kinageuka "**ZI.**" Majina haya ni ya ngeli ya "**I-ZI**."

**Kazi ya 5: *Mkufunzi aandike ubaoni sentensi za kushughulikiwa, kisha awagawe wanafunzi katika makundi kufuatana na idadi yao na kila kundi lishughulikie sentensi zote. Wanafunzi kutoka kila kundi washirikishwe kwenda ubaoni na kutoa majibu. Mkufunzi awapatie wanafunzi wengine fursa ya kutoa hoja zao kuhusu majibu yaliyotolewa ubaoni pale inapohitajika. Majibu ya kutolewa ni haya yafuatayo:***

1. Barabara hii ni **mpya** lakini imepasuka kwa sababu haikujengwa vizuri.
2. Tafadhali nipe Kamusi ya Kiswahili **Sanifu** kuna msamiati mgumu ninaotaka kuchunguza.
3. Karatasi **chafu** zimetupwa jalalani.
4. Meza **pana** imewekewa bidhaa nyingi sokoni.
5. Pombe **tamu** iliwalevya watoto na kusababisha kutohudhuria masomo.

**Kazi 6: *Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi watano watano. Kila kundi lishughulikie kazi yote iliyotolewa, kisha amotishe kila mwanafunzi kutunga sentensi moja katika kundi lake. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Nyumba **kubwa** zimeanza kujengwa mjini kwetu hivi karibuni kufuatana na maendeleo ya kibiashara yanayojitokeza kwa hali ya juu.

b. Shule **pana** ilijengwa mjini Musanze kwa lengo la kuwapokelea wanafunzi wengi mwaka ujao.

c. Nipe karatasi **safi** nimwandikie mama yangu kuhusu habari za masomo yangu shuleni.

d. Baiskeli **mpya** imetumiwa katika shughuli za kubeba mizigo sokoni.

e. Nyumba **chafu** zilisababisha kuwepo kwa viroboto kabla ya kuzisafisha.

**Matumizi ya lugha: Msamiati maalumu katika uwanja wa kibiashara**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi watano watano kisha awaombe kutaja maneno matano yanayotumiwa katika shughuli za kibiashara. Kila kundi liwasilishe mbele ya darasa matokeo yake. Mkufunzi ashiriki kama mwezeshaji. Mapendekezo ya majibu:***

a. Uuzaji wa rejareja: Uuzaji wa bidhaa moja moja.

b. Uuzaji wa jumla: Uuzaji wa bidhaa nyingi kama maburungutu ya vitu wakati mmoja.

c. Bei rafi: Bei ambayo haipunguzwi.

d. Bei ya kuruka: Bei iliyopanda na isiyokubalika kisheria.

e. Rasilimali: Jumla ya mali inayomilikiwa na mtu, kampuni au nchi.

**Kazi ya 8:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi tofauti na kuwaongoza kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati uliotolewa. Mapendekezo ya majibu:***

**a. Hundi**: Baba amenipatia hundi ya themanini elfu kwa ajili ya kulipa ada ya shule.

**b. Mteja:** Kuna wateja wengi katika duka la dadangu.

**c. Ruzuku:** Wilaya yetu imepewa na serikali ruzuku ya kutosha ili kukarabati barabara zilizokuwa zimeharibika.

**d. Magendo:** Biashara za magendo zimeshapigwa marufuku nchini Rwanda.

**e. Rasilimali:** Rasilimali ya mwenyeduka huyu yapata mia tano milioni.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi ya wanne wanne na kuwapa fursa ya kujadili juu ya safari ya sokoni waliyoifanya, kisha mwakilishi wa kila kundi aitwe mbele ya darasa na kukariri kauli ya wenzake.***

**Kuandika**

**Kazi ya 10:** ***Baada ya kuwagawa wanafunzi katika makundi madogo madogo, mkufunzi awaongoze kutunga kifungu cha habari chenye aya tatu kuhusu safari yao ya sokoni. Mkufunzi awasahihishie makosa yao ya kisarufi na kisintaksia.***

## SOMO LA 20: MAJADILIANO DUKANI

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kutumia kwa ufasaha msamiati maalum wa kibiashara katika majadiliano ya bei,
- Kueleza aina za bidhaa za madukani na masokoni; bidhaa zitokanazo na mazao, zile zitokanazo na mifugo, na zile zitokanazo na viwanda na madini,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha mazungumzo baina ya muuzaji na mnunuzi,
- Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya I-ZI na kupatanisha kisarufi.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha duka, bidhaa zinazouzwa dukani, vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongeza vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa kila mkufunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kufikia jibu sahihi.

- **Mbinu ya fikiri -jozi - changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi hurekebisha ama husahihisha pale inapohitajika.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi***:* Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi watano watano kisha awaombe kutaja mahali fulani panapofanyiwa biashara na huduma zinazotolewa hapo. Kila kundi liwasilishe mbele ya darasa matokeo yake. Mkufunzi ashiriki kama mwezeshaji mahiri wa kuaminika. Mapendekezo ya majibu:***

a. Mkahawa: Pahala panapouzwa kahawa, chai na vyakula vingine.

b. Baa: Mahali panapouzwa na kunywewa pombe.

c. Hoteli: Jengo maalumu lenye vyumba vya kupangishia ambamo agh. vyakula na vinywaji huuzwa.

d. Duka: Mahali panapouzwa na kununuliwa vitu, nyumba ya biashara.

e. Soko: Mahali penye mkusanyiko wa wauzaji wengi wanaouza bidhaa rejareja.

**Kusoma na ufahamu: Muuzaji na mteja**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kulingana na idadi ya wanafunzi waliopo. Mwanzoni, wasome kimya mazungumzo na baadaye wapewe fursa ya kusoma kwa sauti mazungumzo hayo. Mwishowe, wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu yaliyoulizwa. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Bidhaa zinazozungumziwa katika mazungumzo haya ni: Sabuni, chumvi, sukari, vitunguu, mafuta ya kupikia na sufuria.
2. Kalisa alinunua: Sabuni moja, kilo moja ya chumvi, kilo mbili za sukari, nusu ya vitunguu, lita moja ya mafuta ya kupikia na sufuria moja.
3. Mizani hutumiwa kupima uzito wa bidhaa na kusaidia kutonyang'anya wanunuzi wanaponunua bidhaa mbalimbali.
4. Uwera huuza bidhaa zinazotokana na mahitaji ya wateja ili waweze kufaidika na kile wanachokinunua.
5. Uwera alimwahidi Kalisa kumpa nyongeza ya kutosha siku ijayo.

**Kazi ya 3:** ***Katika jozi, wanafunzi watoe maelezo ya bidhaa zilizotolewa. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. **Kekee:** Chombo cha seremala cha kutobolea ubao.

b. **Patasi:** Chombo cha chuma kilicho bapa, agh. chenye mpini wa mti na mbele kina makali, hutumiwa kutobolea mashimo kwenye mbao.

c. **Chungu:** Chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kitumiwacho kwa kupikia.

d. **Jiko la mkaa:** Chombo cha kupikia.

e. **Almasi:** Madini ngumu ya thamani sana, agh. hutumika kukatia kioo.

f. **Dhahabu:** Madini ya thamani yenye rangi ya manjano mbivu ambayo hutumika kufulia vitu vya kujipambia k.v pete au mkufu na hutumika kama kipimo cha thamani ya sarafu na utajiri wan chi.

g. **Maziwa:** Kiwowevu kizito na cheupe kinachotoka kwenye titi la mnyama au binadamu wa kike.

h. **Kuku:** Ndege anayefugwa na anayefanana sana na kware mkubwa.

i. **Maparachichi:** Matunda yenye kokwa ndani na nyama ya kijani.

j. **Tikitimaji:** Tunda la aina ya boga lenye nyama nyekundu au kijani hafifu au manjano likiisha iva, huwa na maji ndani, ambalo huliwa bila ya kupikwa.

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI**

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aandike ubaoni sentensi zenye kivumishi cha a- Unganifu kisha aombe wanafunzi kueleza mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza. Kazi hii ifanyike katika makundi na kila kundi lipewe fursa ya kueleza mbele ya darasa matokeo ya kazi hii. Mkufunzi atoe hitimisho. Pendekezo la jibu:***

Majina yaliyotumiwa katika sehemu A ni majina ya ngeli ya **I-ZI** katika umoja na yametumiwa pamoja na kivumishi cha a-Unganifu. Katika sehemu B, majina hayo yamewekwa katika wingi. Mabadiliko ya kisarufi ambayo yamejitokeza ni kwamba katika umoja kivumishi cha a- Unganifu kimetumia "**ya**" wakati ambapo katika wingi ile "**ya**" imegeuka "**za**" kufuatana na upatanisho wa kisarufi.

**Kazi ya 5**: ***Mkufunzi awaweke wanafunzikatika makundi ya watano watano kisha watunge sentensi sahihi. Mkufunzi achunguze ikiwa kila mwanafunzi anatunga sentensi sahihi katika kila kundi. Mapendekezo ya majibu:***

a. Kazi ya mama inachangia katika kuongeza mapato ya familia yangu.

b. Televisheni ya taifa letu inapeperusha habari za kusitawisha umoja na maridhiano katika jamii ya Wanyarwanda.

c. Nyama ya samaki ni muhimu sana kwa afya ya wanadamu.

d. Ngazi za utawala lazima ziheshimiwe mahali kote.

e. Kengele za shule zinapigwa na wanafunzi wakakimbilia darasani.

**Matumizi ya lugha: Aina za bidhaa zinazopatikana sokoni**

**Kazi ya 6:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi ya watano watano na kuwamotisha kubainisha bidhaa kumi zinazopatikana sokoni. Baadaye wawasilishe matokeo yao mbele ya darasa. Mapendekezo ya majibu:***

a. Matufaha
b. Kibiriti

c. Karatasi

d. Mapapai

e. Mafenesi

f. Samaki

g. Jogoo

h. Shati

i. Sidiria

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Kila mwanafunzi ashirikiane na mwenzake. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Bidhaa zitokanazo na viwanda: Msumari, kompyuta, gari, n. k.
2. Bidhaa zitokanazo na mazao: Mahindi, maharage, viazi vitamu, n.k.
3. Bidhaa zitokanazo na ufugaji: Mayai, kuku, ng'ombe, maziwa, n.k.
4. Bidhaa zitokanazo na madini: Almasi, feruzi, yakuti, n.k.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8:** ***Kazi ya jozi. Mkufunzi aandae somo la mazungumzo kati ya wanafunzi wawili wawili darasani huku akichunguza makosa ya kimatamshi.***

**Kuandika**

**Kazi la 9:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi na ya nyumbani. Wanafunzi waombwe kutunga mazungumzo kuhusu majidiliano ya bei. Mkufunzi asahihishe makosa ya kiothografia.***

## SOMO LA 21: MATUMIZI BORA YA MIZANI

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kutumia kwa ufanisi mizani katika hesabu za biashara,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya I-ZI.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa muhimu katika somo hili ni vifuatavyo:

Michoro au picha zinazoonyesha soko na wauzaji wanaotumia mizani, bidhaa zinazouzwa sokoni, vinasa sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Hali kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anashauriwa kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kufikia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi hurekebisha ama husahihisha pale inapohitajika.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji**: Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo

na kuyaigiza darasani.

- **Mijadala darasani**: Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti**: Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi achore kwenye karatasi kubwa vibanda na kila kibanda kiwe kinaonyesha bidhaa zinazouzwa hapo. Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wajadili wanachokiona kwenye vibanda hivyo na shughuli zinazofanyika hapo. Mapendekezo ya majibu:***

- Kuna soko na bidhaa zinazouzwa hapo,
- Kuna vibanda vyenye bidhaa tofauti,
- Kuna soko la kisasa na sehemu zake.

**Kusoma na ufahamu: Matumizi bola ya mizani**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi awagawe wanafunzi katika makundi ya watano watano na kuwamotisha kusoma kifungu hiki cha habari kimya na baadaye kuandika majibu yao kwenye karatasi. Kila kundi litawasilisha mbele ya hadhira majibu ambayo wamepata. Mkufunzi ashiriki kwa kueleza zaidi pale ambapo wanafunzi wanapata vikwazo. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Ni mfanyabiashara aitwaye Muhire aliyekuwa analalamikiwa kwa matumizi ya mizani yake isiyo sahihi.
2. Adhabu hizo ni kifungo au kutozwa faini.
3. Aliwaonya kuacha tabia mbaya hiyo mara moja kwani wakikamatwa watapata hasara.
4. Lengo la ziara ya viongozi wanaohusika na ushuru ni kuwakagua wafanyabiashara halamu.
5. Jambo jema husifiwa na hushangiliwa ili liweze kufana zaidi. Ni kama kidole kizuri kinapovalishwa pete ili kizidi kupendeza. Kwa ufupi, afanyaye vizuri hutuzwa.

Kutokana na kifungu cha habari hiki, wafanyabiashara ambao hawakuwa na makosa yoyote katika shughuli zao za biashara walipewa na viongozi tuzo ya mizani nne.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kila kundi lipewe Kamusi ya Kiswahili Sanifu ili kuchunguza msamiati unaohusiana na maelezo yaliyotolewa. Baada ya hapo wawasilishe mbele ya darasa matokeo ya kazi yao. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. d
2. g
3. f
4. b
5. a
6. e
7. c

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI na vivumishi vya kurejesha**

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aandike sentensi hizi ubaoni na kuweka wanafunzi katika makundi ya watatu watatu. Mkufunzi ahamasishe wanafunzi kuchunguza mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza katika sentensi hizo na kila kundi liwasilishe maoni yao mbele ya wenzao. Pendekezo la jibu:***

Katika sehemu ya A kuna majina ya ngeli ya I-ZI ambayo yametumiwa katika umoja yakifuatana na kirejeshi "**amba-". Majina** haya ambayo yametumiwa katika sentensi iliyo katika umoja yamechukuwa kirejeshi **"-yo"** na katika wingi kirejeshi **"-yo"** kimegeuka **"-zo."**

**Kazi ya 5**: ***Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia kirejeshi amba- kufuatana na maneno waliyopewa. Sentensi hizi ziwe katika umoja na wingi na kazi hii iwe ya kibinafsi. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Klabu ambayo inajihusisha na kuhifadhi mazingira imeahidiwa na mkurugenzi wa shule kutembelea mbuga ya wanyama ya Akagera.

b. Chupa ambazo zimesafishwa zinatandikwa sokoni.

c. Redio ambazo zinarusha habari za kuhamasiha raia kupenda kazi zinachangia katika ukuzaji wa uchumi wa nchi.

d. Kaptula ambayo imechanika imetupwa jalalani.

e. Suruali ambayo imeibiwa na wezi imerudishwa.

**Matumizi ya lugha: Matumizi ya mizani katika hesabu na aina za pesa**

**Kazi ya 6:** ***Wanafunzi, katika jozi, wajadiliane kuhusu vipimo wanavyovijua. Mkufunzi awaongoze ili kufikia malengo yaliyowekwa. Mapendekezo ya majibu:***

- Vipimo vya umbali.
- Vipimo vya tungamo.
- Vipimo vya ujazo.

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika jozi na kuwaongoza kuwasilisha majibu yao mbele ya darasa. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Kumi na sita: 16

b. Thelathini na moja: 31

c. Sabini na saba: 77

d. Mia tatu hamsini: 350

e. Moja elfu, mia mbili na saba: 1207

f. Laki tano: 500,000

g. Moja elfu mia sita ishirini na sita: 1626

**Kazi ya 8:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi na mkufunzi achunguze ikiwa kila mwanafunzi anashiriki ipasavyo.***

a. Sitini jumlisha kumi ni sawa na sabini : 60+10=70

b. Mia moja na arubaini toa ishirini na saba ni sawa na mia moja kumi na tatu:140-27=113

c. Mia nane na themanini gawanya kwa nane ni sawa na mia moja kumi: 880/8=110

d. Sabini na moja ni kubwa kuliko kumi na nne:71>14

e. Mia moja ni ndogo kuliko laki moja: 100<100,000

f. Tisini mara tatu ni sawa na mia mbili na sabini: 90×3=270

**Kazi ya 9:** ***Wanafunzi wawekwe katika makundi ya watatu watatu na kutumia mbinu ya bunguabongo. Mkufunzi achore michoro inayoonyesha ghorofa inayotumiwa na wafanyabiashara wanaobadilisha pesa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi kutazama na kueleza kinachoendelea. Mapendekezo ya majibu:***

- Kuna ghorofa kubwa ndefu inayovutia,
- Kuna ghorofa kubwa inayotumiwa katika shughuli za kibiashara,
- Ghorofa ile ni ya wafanyabiashara wanaojishughulisha na kubadilisha pesa za kigeni,
- Ni watu wanaobadilishana pesa katika maduka ya kubadilisha pesa.

**Kazi ya 10**: ***Mkufunzi aandike maswali ubaoni na kutumia mbinu ya fikiri-jozi- changia. Hapa wanafunzi wawili wawili watajadiliana kuhusu pesa zinazotumiwa katika nchi na bara tofauti na wapate jibu sahihi. Baadaye, kila jozi iwasilishe matokeo yao mbele ya darasa. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Wanyarwanda wengi hutumia **faranga** katika shughuli nyingi za biashara ya ndani.

b. Mjomba wangu alikwenda kumtembelea rafiki yake anayeishi Uganda. Kabla ya kuvuka mpaka alikwenda kwenye duka la kubadilisha pesa ili wampe **shilingi** za Uganda.

c. Mama aliniahidi kwamba nikishika nafasi ya kwanza katika kidato cha kwanza atanitembeza Marekani. Katika safari yetu tutatumia **dola** mia nne za kimarekani.

d. Shughuli za biashara anazozifanya mama yangu huhusisha uagizaji wa bidhaa kutoka Japani. Kila wiki hulipa **yeni** elfu tano.

e. Je, uliwahi kufika katika duka la kubadilisha pesa? Mimi nilifikapo nikaona faranga za Rwanda, Shilingi za Kenya, Dola za Marekani na Kanada na **pauni** za Uingereza.

**Kazi ya 11:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi na kazi ya nyumbani. Mkufunzi aombe wanafunzi kutafuta aina za pesa zinazotumiwa katika nchi zilizo tofauti na zile ambazo wamesoma. Kila mwanafunzi arudi akiwa na majibu sahihi kipindi kijacho. Mapendekezo ya majibu:***

| NCHI | AINA YA PESA |
|---|---|
| Libya | Dinar |
| Ghana | Cedic |
| Zambia | Kwacha |
| Moroko | Dirham |
| Botwsana | Pula |
| Swaziland | Lilangeni |
| Lesotho | Loti |
| Nijeria | Naira |

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 12**: ***Mkufunzi atumie jozi na kila mwanafunzi asimulie mwenzake sifa za soko fulani alilolitembelea na kueleza bidhaa alizoziona. Baadaye mwanafunzi aliyesimuliwa awasilishe mbele ya darasa aliyoyasikia.***

**Kuandika**

**Kazi ya 13:** ***Katika jozi, wanafunzi wapewe fursa ya kukaa pamoja na kushirikiana katika ubunifu wao. Baadaye wawasilishe matokeo ya kazi yao hadharani.***

## 5.6. Muhtasari wa mada

"Matumizi ya msamiati katika mazingira ya biashara" ni mada ya tano katika kitabu cha mwanafunzi. Imejigawa katika masomo matatu ambayo ni yafuatayo:

1. ***Mawasiliano sokoni***: Somo hili linatilia maanani msamiati maalumu unaotumiwa katika shughuli za kibiashara.
2. ***Majadiliano dukani:*** Somo hili linahusu aina za bidhaa mbalimbali.
3. ***Matumizi bora ya mizani***: Somo hili limesisitizia aina za mizani ama vipimo, hesabu na aina za pesa zinazotumiwa duniani.

Ikumbukwe kuwa kila somo limezingatia sehemu kuu sita ambazo ni:

i. Kusoma na ufahamu

ii. Matumizi ya msamiati maalum

iii. Sarufi

iv. Matumizi ya lugha

v. Kusikiliza na kuzungumza

vi. Kuandika

## 5.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu mahiri tena wa kuaminika, na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao cha ujuzi kwa ajili ya kuimarisha akili yao na kuitumia kwa ufasaha lugha yetu tukufu; yaani, Kiswahili.

## 5.8. Tathmini ya mada ya tano

Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kuchunguza uwezo wa kila mwanafunzi na kumsaidia pale anapoonyesha udhaifu katika masomo yake.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

**1.**

a. Nguo

b. Viatu

c. Viti

d. Ndoo

e. Uma

f. Simu

g. Daftari

h. Meza

i. Viazi

j. Mahindi

k. Mbatata

**2.** Kukamilisha sentensi kwa kuchagua neno linalofaa:

**Majibu yariyopendekezwa :**

a. Mwalimu wetu huvaa suti nzuri sana. Wanafunzi wote hufikiri kwamba suti zake hununuliwa kwa bei **ghali.**

b. Dada yangu amekwenda sokoni **kununua** sare ya shule ili arudi shuleni kesho kuanza masomo ya muhula wa tatu.

c. Uwantege anauza matunda katika soko la Nyagasambu. Kwenye kibanda chake kuna **maembe, ndizi mbivu, machungwa, mananasi** na **tikitimaji**.

d. Mwenyeduka katika duka la vitabu alitoa **nyongeza** ya kitabu kimoja cha hadithi za Kiswahili kwa wateja wote ambao hununua kwake kila wiki.

e. Wakati wa uhaba wa **bidhaa** sokoni, bei hupanda sana.

3. Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno ya ngeli ya I-ZI:

**Majibu yaliyopendekezwa:**

a. Nchi zote za Kiafrika zimeweka mikakati thabiti ya kuondoa umaskini kabla ya mwisho wa mwaka 2050.

b. Tarafa ya Kivugiza katika Wilaya ya Nyarugenge imepiga hatua sana katika usawa wa kijinsia.

c. Serikali ya Rwanda inasifika sana katika uwanja wa kuhifadhi mazingira katika bara la Afrika.

d. Barabara za lami zilirahisisha mawasiliano ya kibiashara kati ya tarafa, wilaya, majimbo na nchi tofauti ulimwenguni.

e. Shule ya Mtakatifu Marko wilayani mwetu imeshika nafasi ya kwanza katika mashindano ya mpira wa wavu mwaka huu.

4. Kukamilisha kifungu cha habari kwa kutumia maneno sahihi:

**Majibu:**

Mamake Mutoni ni mfanyabiashara katika soko la Nyarugenge. Mara nyingi huagiza bidhaa kutoka nchi zinazopakana na Rwanda. Anapoagiza bidhaa kutoka Uganda inambidi abadilishe **faranga** za Rwanda katika **shilingi** za Uganda. Ni sawa na kuagiza bidhaa kutoka Tanzania na Kenya.

Ikiwa Mama anahitaji bidhaa zinazotengenezewa katika nchi za Ulaya kama Vile Uingereza, inambidi kutumia **pauni**. Mwezi uliopita rafiki yake ambaye anaishi Marekani alimwambia kuwa kuna bidhaa nzuri zinazoweza kumletea faida nyingi anapoziuza kwa Wanyarwanda. Mama aliamua kumtumia **dola** elfu tatu za Marekani ili amnunulie bidhaa hizo.

Kazi ya biashara naipenda sana. Kuna wakati ambapo naenda pamoja na mama yangu Zambia na Libya kufanya biashara huko nikaona namna anavyobadilisha faranga zake katika **nairu** za Libya au **kwacha** za Zambia nikawa na motisha ya kufanya biashara ya kubadilisha pesa siku moja. Mimi nafikiri kwamba aina hii ya biashara itachangia kuongeza mapato yetu nyumbani.

5. Hapa, wanafunzi wanaweza kubuni mazungumzo yao wenyewe kwa kuongozwa na mkufunzi. Lengo la swali hili ni kuwezesha wanafunzi kutumia msamiati wa kibiashara wakitilia maanani jinsi ya kujadiliana bei.

## 5.9. Kazi za ziada

### 5.9.1. Kazi za urekebishaji

Weka bidhaa zifuatazo katika kundi linalofaa kati ya haya yafuatayo: Bidhaa zitokanazo na kilimo, ufugaji na viwanda: Mapera, maziwa, sindano, utepe, randa, chaki, samaki, matufaha, jogoo, zabibu, ndimu,bata.

**Majibu:**

| Bidhaa zitokanazo na kilimo | Ufugaji | viwanda |
|---|---|---|
| Mapera | Maziwa | Sindano |
| Matufaha | Samaki | Utepe |
| Zabibu | Jogoo | Randa |
| Ndimu | Bata | Chaki |

### 5.9.2. Kazi jumuishi

Soma kifungu kifuatacho na kujaza mapengo kwa kutumia neno linalofaa.

Binti yangu huishi huko nchini Tanzania. Katika nchi hii wanatumia pesa aina ya ………… katika biashara zao. Dada yake Musafiri anasomea masomo ya lugha katika chuo kikuu cha Rwanda, Koleji ya Ualimu huko Rukara. Musafiri hutumia ………… elfu tatu za Rwanda kutoka Kigali kufika Rukara.

Mwaka ujao mke wangu anatarajia kutembelea Uingereza. Inambidi awe na ………… mia mbili za Uingereza. Baada ya safari hiyo atapitia Moroko. Hapo ataanza kubadilisha pesa zake katika Dirham.

**Majibu:**

a. Shilingi

b. Faranga

c. Pauni

d. Dirham

### 5.9.3. Kazi za nyongeza

Taja na kueleza vitu muhimu angalau vitatu ambavyo mfanyabiashara analazimishwa kutilia maanani ili aweze kutoa huduma nzuri kwa wateja.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

a. **Kujua bidhaa yako:** Katika kumhudumia mteja hakikisha unaijua bidhaa yako vizuri. Isitokee mteja akauliza swali lolote ukamwambia hujui. Hii inamkatisha tamaa na kuanza kuona anaweza kuwa ananunua kisicho sahihi au kitu ambacho hakina ubora.

b. **Lugha/mawasiliano ya mwili:** Wingi wa mawasiliano ambayo sisi tunawasilisha kwa wengine hufanywa kwa lugha ya mwili. Tukiwa na lugha hasi ya mwili wakati tunaingiliana na wengine inaweza kuonyesha ukosefu wa kujali katika upande wetu. Sehemu mbili muhimu za lugha chanya ya mwili ni tabasamu na mawasiliano kijicho. Hakikisha kuwa umewaangalia wateja wako katika macho. Hii inaonyesha kwamba tunawasikiliza kwa makini. Na kisha, bila shaka tabasamu tu linakaribisha zaidi kuliko mtu ambaye ana uso uliozubaa.

c. **Tarajia mahitaji ya mgeni:** Hakikisha unamhudumia mteja zaidi ya matarajio yake. Daima, tafuta njia za kumtumikia mteja wako zaidi ya anavyotarajia. Katika kufanya hivyo inamsaidia kujua kwamba wewe unajali na itamuacha na "kipengele cha kuhisi vizuri" ambacho sisi tunatafuta.

# MADA YA 6:

# UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO

## 6.1. Uwezo mahususi katika mada hii

Kuigiza mazungumzo mbalimbali kwa kutumia Kiswahili sanifu

## 6.2. Ujuzi wa awali

Mada hii inazungumzia "Uigizaji wa mazungumzo." Wanafunzi wa mwaka huu wana ujuzi wa awali wa kutosha kuhusu uigizaji wa mazungumzo. Hii inadhihirishwa na ukweli wa kwamba toka kidato cha kwanza hadi cha nne, wanafunzi walishughulikia sana mazungumzo mbalimbali hivi wakiyakariri na kuyawasilisha darasani. Kwa hiyo, mada hii itakuwa kwa wanafunzi chanzo cha kupanua ujuzi na uwezo walionao wa kuzungumza kwa ufasaha hadharani.

## 6.3. Masuala mtambuka

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile mafunzo kuhusu usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili pamoja na mafunzo kuhusu uzalishaji mali/ujasiriamali. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika.

## 6.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi, wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 6.5. Orodha ya masomo

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| 1. Kuigiza mazungumzo | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza maana ya mazungumzo na aina zake.<br>**Stadi:** Kuigiza mazungumzo mbalimbali.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujiamini katika mawasiliano. | 8 |
| 2. Umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza umuhimu wa maigizo katika maisha ya kila siku.<br>**Stadi:** Kuigiza mazungungumzo kwa madhumuni ya mamlaka mbalimbali.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujivunia faida kutoka maigizo. | 7 |
| 3. Vifaa na sifa katika uigizaji wa mazungumzo | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha vifaa vitumiwavyo katika uigizaji wa mazungumzo pamoja na sifa za mwigizaji bora.<br>**Stadi:** Kuigiza mazungungumzo kwa kutumia vifaa maalum na kuongozwa na sifa bora.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuiheshimu sanaa ya maigizo kwa ajili ya kupata manufaa mbalimbali. | 7 |
| Tathmini ya mada | | 2 |
| Vipindi vya mada yote | | 24 |

## SOMO LA 22: KUIGIZA MAZUNGUMZO

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza maana ya mazungumzo na aina zake,
- Kuigiza mazungumzo husika,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia viulizi mbalimbali.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa halisi kama vile mikrofoni, kipaza sauti, simu ya mkononi, meza, viti, runinga, chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.
- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea karatasi hizo na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo**

***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Mazungumzo ni utaratibu wa kuongea baina ya watu wawili au miongoni mwa watu zaidi ya mmoja au pande mbili tofauti kuhusu mada mbalimbali zinazobadilikabadilika.
2. Kukuza stadi za kukariri, kuburudisha, kuendeleza ujuzi na uwezo wa kuzungumza hadharani, kupata zawadi au mshahara.
3. Mazungumzo hujadili mada kadhaa zenye muktadha wa maisha ya binadamu.
4. Kutoa sauti, kujiamini, kutumia lugha ishara, kuwa na ucheshi, n.k.

5. Mandhari ya mazungumzo hayana mpaka: sokoni, njiani, darasani, nyumbani, harusini, n.k.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao.***

**Mwelekeo:**

Wanafunzi sita kwenye duara mbele ya wenzio wakiigiza mazungumzo, mikrofoni mikononi mwa mwanafunzi mmoja.

**Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya mwalimu mkuu wa shule na mzazi**

**Kazi ya 2:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Mapendekezo ya majibu:***

1. Mazungumzo kati ya mkuu wa shule na mzazi kuhusu utovu wa nidhamu wa mtoto wake shuleni.
2. Shuleni katika ofisi ya mkuu wa shule.
3. Kueleza sababu za utovu wa nidhamu wa mwanawe.
4. Kuchelewa kufika shuleni asubuhi, kukosa vifaa vya ujifunzaji kwa mwanafunzi pamoja na ukosefu wa usafi kwenye mwili wa mwanafunzi.
5. Wazazi wameahidi kutimiza wajibu wao wa kumlea mtoto wao kama ilivyo; shule nayo imeahidi kuwasiliana na wazazi mara kwa mara kwa manufaa ya mtoto.
6. “Harakati za maisha ya leo ni pingamizi kubwa kwa elimu ya watoto katika jamii”. Hii inathibitishwa na jinsi wazazi wa mwanafunzi huyu hawakutimiza wajibu wa kumchunga mtoto na kumpatia mawaidha kwa sababu ya shughuli za kimaisha. Hata hivyo, mtoto huyu alikosa adabu shuleni na kutumwa mzazi wake.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Waweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya kamusi za Kiswahili sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Baada ya kutoa maana, waongoze wanafunzi kutunga sentensi mmoja kwa mmoja na kusahihisha makosa mbalimbali yanayoweza kujitokeza. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:***

a. **Utovu wa nidhamu:** ukosefu wa mwenendo mzuri au adabu.

b. **Kuwasili:** kufika mahali ulipotarajia baada ya safari.

c. **Kukiri:** kuungama au kukubali jambo, hoja au tendo ulilofanya

d. **Kuzorota:** kurudi nyuma kiutendaji, kukosa kupiga hatua kwa haraka.

e. **Chanzo:** jambo lililosababisha kutokea kwa kitu fulani.

f. **Kuahidi:** kutoa ahadi.

g. **Kurekebisha:** kutengeneza kilichoharibika au kwenda mrama kifae tena.

h. **Kuimarisha:** kufanya madhubuti, kufanya kuwa na nguvu, kufanya kuwa imara.

i. **Uamuzi:** ukataji shauri wa kufanya jambo fulani.

j. **Bega kwa bega:** kwa kushirikiana.

**Kazi ya 4:** ***Kazi hii ifanyike kibinafsi. Wanafunzi wa kujitolea washindane kutoa jibu haraka.***

i. **Kukiri** kosa ni njia ya kusamehewa.

ii. Ukosefu wa mwenendo mzuri ni **chanzo** cha kushindwa masomo shuleni.

iii. Ni lazima kuepuka vita kwa sababu bila usalama amani na utulivu **huzorota.**

iv. Tunaombwa **kurekebisha** tabia mbaya ili tujenge jamii nzuri.

v. Tumechukua **uamuzi** huu shuleni kwa ajili ya kugombana dhidi ya uvivu miongoni mwa wanafunzi.

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike kibinafsi. Wanafunzi wa kujitolea washindane kutoa jibu haraka.***

a. **Kumkaribisha mtu:** kumfukuza mtu.

b. **Utovu wa nidhamu:** mwenendo mzuri, adabu.

c. **Kushirikiana bega kwa bega:** Kutengana.

d. **Kuzungumza:** kukaa kimya.

e. **Kuheshimu:** kudharau.

**Sarufi: Matumizi ya "nini," na "lini"**

**Kazi ya 6:** ***Tumia mbinu ya kuuliza maswali ambapo mwanafunzi anayejitolea atoe jibu.***

**Mwelekeo:**

Maneno yaliyopigiwa mstari huitwa viulizi, yaani maneno yanayotumiwa kuuliza swali.

Viulizi huweza kutumiwa mwanzoni mwa sentensi au mwishoni mwake.

**Nani**

Neno hili hutumiwa kuulizia mtu, Mwenyezi Mungu, mnyama, ndege au wadudu.

**Nini**

Hutumiwa kwa kuulizia kitu.

**Lini**

Neno hili hutumiwa kuuliza kipindi cha muda (tarehe au mwaka).

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo.***

a. Shule yetu ilijengwa lini?

b. Ukosefu wa usafi huweza kusababisha nini?

c. Nani ambaye amewasili nyumbani?

**Matumizi ya lugha: Mazungumzo na ugizaji wake**

**Kazi ya 8:** ***Wagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo ambapo watajadiliana na kutoa hoja ambazo zitawasilishwa mbele ya darasa.***

**Mwelekeo:**

Mazungumzo ni utaratibu wa kuongea baina ya watu wawili au miongoni mwa watu zaidi ya mmoja au pande mbili tofauti kuhusu mada mbalimbali zinazobadilikabadilika.

**Aina za mazungumzo:**

- **Malumbano ya utani**: Ni mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani. Watu husimama jukwaani na kushindana kwa maneno. Mazungumzo haya hutumia mzaha na vichekesho pamoja na kejeli ili kuangazia ukweli fulani katika jamii.

- **Ulumbi**: Ni uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi. Walumbi husifika sana kwa kuzungumzia mambo yanayoathiri jamii.
- **Soga**: Ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum. Aghalabu soga huwa na vichekesho vingi, mzaha na kejeli. Nia yake huwa kuburudisha na kupitisha wakati. Soga huwa na vichekesho na mzaha mwingi. Mada hubadilikabadilika kutoka wakati mmoja hadi mwingine. Haihitaji taaluma yoyote ya kisanaa na inaweza kufanyika mahali popote - njiani, sebuleni, katika vyumba vya burudani, n.k.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 9:** ***Tumia redio rekoda, simu ya mkononi au runinga na kuwaomba wanafunzi kuwa na utaratibu wa kusikiliza yaliyomo. Baadaye, yaunde makundi madogomadogo na kujadiliana kuhusu kazi iliyotolewa na kuwasilisha matokeo darasani.***

**Mwelekeo**

Video ya 1

**https://www.youtube.com/watch?v=NK4M_yrYIJI imezungumzia watangazaji wa Redio Maisha wawatembelea wagonjwa katika hospitali ya Kenyatta.**

Video ya 2

https://www.youtube.com/watch?v=G91GtbgdZKA inahusu Mwito wa Mazungumzo.

**Kazi ya 10:** ***Hii ni mbinu ya mchezo wa umithilishaji. Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika katika mazungumzo husika. Kila mwanafunzi apewe jukumu lake la kuiga wakati unaokusudiwa kuwasilisha kazi hii.***

**Kuandika**

**Kazi ya 11:** ***Kazi ya nyumbani na ya kibinafsi. Kila mwanafunzi abuni na kuandika mazungumzo baina yake na mwalimu.***

**Kazi ya 12:** ***Unda makundi matatu ya wanafunzi kulingana na viulizi vitatu husika ambapo kila kundi litatunga sentensi sita na kuzisoma hadharani.***

## SOMO LA 23: UMUHIMU WA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kujadili umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo,
- Kuigiza mazungumzo husika,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia viulizi mbalimbali.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa halisi kama vile mikrofoni, simu ya mkononi, meza, viti, vinasa sauti, runinga na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongezea vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila

msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.

- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.
- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea kataratasi kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia  fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo mijadala.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Mapendekezo ya majibu:***

Wanafunzi wamekaa kwenye viti, msichana na mvulana wanasimama na kushika mikrofoni. Huenda wanafunzi hao wakawa wanaigiza maigizo fulani.

**Kusoma na ufahamu: Tujivunie lugha yetu**

**Kazi ya 2:** ***Majadiliano yafanyike katika jozi. Pendekezo la majibu:***

1. Faida kutoka uigizaji wa mazungumzo.
2. Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Tarubwenge ambao ni Kamana na Zaninka.
3. Mazoezi ya kuigiza mazungumzo.
4. Ndiyo. Kwa sababu wamefikia kiwango cha juu cha kuizungumza kwa ufasaha lugha ya Kiswahili. Ujuzi na uwezo huo uliwawezesha kupata zawadi nyingi kutoka sherehe za burudani.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Waweke wanafunzi katika makundi madogomadogo kutegemea idadi ya kamusi za Kiswahili sanifu zilizopo na kuwagawa msamiati wa kuchunguza. Baada ya kutoa maana, waongoze wanafunzi kutunga sentensi mmoja kwa mmoja na kusahihisha makosa mbalimbali yanayoweza kujitokeza.***

a. **Kujivunia:** kuonea fahari, kufurahia.

b. **Mchakato:** mfululizo wa vitendo ambavyo hufanywa ili kutimiza lengo fulani.

c. **Tele:** -ingi sana; -liojaa kwa wingi.

d. **Mafanikio:** upatikanaji wa kitu au mahitaji yaliyokuwa yamekusudiwa.

e. **Kujiaminia:** kujisikia kuwa na uwezo wa kufanya jambo fulani.

**Kazi ya 4:** ***Kazi ya kibinafsi. Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia msamiati huu: majivuno, pwani, ushahidi, tajiriba, kujinyakulia.***

i. Zaninka na Kamana wametoa **ushahidi** kwamba uigizaji wa mazungumzo ulikuwa chanzo cha mafanikio yao.

ii. Inahakikishwa kuwa asili ya Kiswali ni sehemu za **pwani** au mwambao.

**iii.** **Majivuno** ni tabia ya kujisikia bora kuliko wengine; maringo.

iv. Baada ya kuishambulia timu B, timu A iliweza **kujinyakukulia** ushindi wa mabao mawili kwa sufuri.

**Sarufi: Matumizi ya "nini", "wapi" na "kwa"**

**Kazi ya 5:** ***Tumia mbinu ya kuuliza maswali ambapo mwanafunzi wa kujitolea atatoa hoja zake.***

**Mwelekeo:**

**Wapi**: Hutumiwa kuulizia mahali na huwekwa mwishoni mwa sentensi tu.

**Tanbihi:** Matumizi ya neno 'mahali' huathiri neno 'wapi' na kugeuka "papi"

**Mfano**: Pahali papi panapotembelewa sana nchini humu?

**Kwa nini**: Kiulizi hiki hutumiwa kuulizia sababu na huwekwa mwanzoni mwa sentensi.

**Kazi ya 6:** ***Tumia mpira kwa kuutupia mwanafunzi fulani ili atoe jibu. Hakikisha kuwa wanafunzi tofauti wameshirikishwa.***

i. Sokwe hupatikana wapi?

ii. Taka zote hutupwa wapi?

iii. Kwa nini hali ya hewa ilikuwa nzuri mwaka huu?

iv. Kwa nini mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi yaliwezekana nchini Rwanda?

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo na wanafunzi wawasilishe hoja zao baadaye.***

**Mwelekeo:**

a. Kuigiza mazungumzo ni kuyakariri mazungumzo yaliyosimuliwa na mtu mwingine na kuyarudia kwa kumwiga mtu huyo kimatendo kwa njia au namna ya mchezo; yaani kuvaa uhalisia wa mtu huyo. Ni karibu na maigizo au michezo ya kuigiza.

b. Umuhimu wa kuigiza mazungumzo:

- Huunganisha watu katika jamii,
- Hutumiwa kama chombo cha kuburudisha katika jamii,
- Huelimisha kuhusu mambo fulani,
- Huleta umoja na utangamano,
- Hutumiwa kuonya dhidi ya matendo mabaya,
- Hutumiwa kupitisha wakati,
- Hukuza stadi za kuzungumza lugha kwa ufasaha,
- Huendeleza hisia za kujiamini katika mawasiliano hadharani.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8:** ***Tumia mbinu ya mchezo wa umithilishaji. Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika katika mazungumzo husika. Kila mwanafunzi apewe jukumu lake la kuiga wakati unaokusudiwa kuwasilisha kazi hii.***

**Kuandika**

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii iwe ya nyumbani na ya kibinafsi.***

**Kazi ya 10:** ***Unda makundi mawili ya wanafunzi kulingana na viulizi viwili husika ambapo kila kundi litatunga sentensi sita na kuzisoma hadharani.***

## SOMO LA 24: VIFAA NA SIFA KATIKA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kubainisha vifaa vinavyotumiwa katika uigizaji wa mazungumzo,
- Kujadili sifa za mwigizaji wa mazungumzo bora,
- Kuigiza mazungumzo husika,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia viulizi mbalimbali.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa halisi kama vile mikrofoni, kinasa sauti, simu ya mkononi, meza, kofia, pesa, mavazi ya aina aina, viti, runinga, na vifaa vingine kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum, matini mbalimbali na kitabu cha mwanafunzi.

Kadhalika, mkufunzi ana wajibu wa kuongeza vifaa vingine ambavyo yeye anadhani ni muhimu sana katika kuliboresha somo lake kwa kuwashirikisha wanafunzi wote wa darasa lake bila upendeleo wowote. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa muhimu vya ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.
- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea kataratasi kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo majadiliano.

**Kazi ya 1:** ***Tumia mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wa kujitolea hushirikishwa. Mkufunzi awamotishe wanafunzi wote kutoa mchango wao. Pendekezo la majibu:***

Ninaona mikrofoni, kofia, vuvuzela, simu ya mkononi.

**Kusoma na ufahamu: Majukumu yetu katika uigizaji wa mazungumzo**

**Kazi ya 2:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwanafunzi mmoja asome swali na mwenzake atoe jibu. Mapendekezo ya majibu:***

1. Kifungu cha habari hiki kinazungumzia vifaa vinavyoweza kutumiwa katika uigizaji wa mazungumzo pamoja na sifa za mwigizaji bora.
2. Wahusika wawili ambao ni Egide pamoja na Liliane.
3. Simu ya mkononi, kofia, aina tofauti za pesa, chupa, tarumbeta, vuvuzela, suti, kimono, tarubushi, bombo, barakoa za ucheshi, mkongojo na miwani.

4. Sifa hizo ni kama vile: Kuwa na ucheshi, kutumia lugha ya ishara na kuzungumza kwa ufasaha.
5. Wameelewa wazi vifaa muhimu vitakavyotumiwa, sifa zinazofaa kwa mwigizaji bora na wana shauku ya kuandaa mazoezi kabla ya mashindano.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Tumia mbinu ya bunguabongo. Shirikisha wanafunzi kutoa maoni kuhusu maana ya msamiati na kukubaliana kwenye maana sahihi. Mapendekezo ya majibu:***

a. **Kombe:** chombo kilichotengenezwa kwa madini ya thamani kinachoshindaniwa na kukabidhiwa mshindi.

b. **Kujali:** kuzingatia jambo na kulitekeleza ipasavyo; kutia maanani.

c. **Maandalizi:** matayarisho ya kufanya kazi au shughuli yoyote.

d. **Mkongojo:** fimbo inayotumiwa na wazee wenye matatizo ya kutembea ili iwasaidie kujikongoja.

e. **Ucheshi:** tabia ya kuwa mchangamfu na kufurahisha watu.

f. **Kimono:** Vazi refu kama kanzu la kike linalovaliwa na mkanda ambalo ni mtindo ulioletwa kutoka Japani.

g. **Tarubushi:** kofia yenye shada la nyuzi ndefu.

h. **Bombo:** Suruali fupi iishiayo juu ya magoti au kwenye magoti. Pia huvaliwa na wanawake.

i. **Barakoa:** kinga ivaliwayo usoni kuzuia ama pua, mdomo au macho dhidi ya vumbi, upepo, harufu au vimelea vya maradhi.

**Kazi ya 4:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Oanisha michoro hii na majina yake, kisha eleza umuhimu wa kila aina: tarumbeta, vuvuzela, suti, miwani, barakoa. Mapendekezo ya majibu:***

| Picha | Msamiati |
|---|---|
|  | **Tarumbeta:** Inatumiwa kama ala ya mziki ya kupuliza. |

| | |
|---|---|
|  | **Suti:** Vazi la wanaume kwa kawaida ambalo limeundwa na suruali pamoja na koti vyenye rangi inayofanana. |
|  | **Vuvuzela:** Chombo cha kushajiishia wanamichezo katika mashindano. |
|  | **Barakoa:** Kifaa kitumiwacho katika maigizo au michezo kwa ajili ya kuchekesha. |
|  | **Miwani:** Chombo cha kuvalia machoni kwa ajili ya ugonjwa wa macho, kujilinda jua ama maringo. |

**Sarufi: Matumizi ya "gani" na "ngapi"**

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike katika jozi. Waongoze wanafunzi kueleza matumizi ya "gani" pamoja na "–ngapi." Pendekezo la majibu:***

a. **gani:** Neno hili hutumiwa kuuliza aina ya mtu au vitu.

b. **ngapi:** Hiki ni kiulizi cha kuulizia idadi ya watu au vitu.

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa wanafunzi. Majibu yaliyopendekezwa:***

i. Tumetumia vifaa gani katika maigizo yetu?

ii. Sabuni ngapi zimewekwa nje ya choo kwa ajili ya usafi?

iii. wanafunzi wangapi wamezawadiwa kwa sababu ya kuimarisha amani na umoja darasani mwao?

iv. Mwigizaji bora anapaswa kuwa na sifa gani?

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mapendekezo ya majibu:***

a. Kuigiza mazungumzo ni kuyakariri mazungumzo yaliyosimuliwa na mtu mwingine na kuyarudia kwa kumwiga mtu huyo kimatendo kwa njia au namna ya mchezo; yaani kuvaa uhalisia wa mtu huyo. Ni karibu sawa na maigizo au michezo ya kuigiza.

b. Kwa kawaida wahusika huwa ni binadamu.Wahusika ndio huzungumza katika sehemu zao mbalimbali. Kulingana na aina ya mazungumzo, wahusika wanaweza kuwa wawili au zaidi. Katika uigizaji wa mazungumzo, majukumu ya watu wa rika au viwango mbalimbali huigizwa kama vile wazee, rais, waziri, askari jeshi, mbunge, mwalimu, mfanyabiashara, mfalme, daktari, hakimu, n.k

c. Maigizo ni sanaa katika fasihi simulizi ambayo watendaji huwa ndio wahusika. Maigizo hayasimuliwi kama mbinu nyingine za fasihi. Wahusika ndio huzungumza katika sehemu zao mbalimbali. Ifuatayo ni mifano ya maigizo.

1. **Michezo ya Kuigiza** (Jukwaani) : Maigizo ya jukwaani ambapo watendaji huiga maneno na matendo ya wahusika mbele ya hadhira.
2. **Miviga:** sherehe mbalimbali katika jamii fulani. Watu hujumuika na sherehe hizi kulingana na tamaduni zao.
3. **Ngomezi**: sanaa ya ngoma. Midundo mbalimbali ya ngoma hutumika kuwasilisha ujumbe mbalimbali.
4. **Malumbano ya utani:** mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani
5. **Ulumbi:** uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi.

6. **<u>Soga</u>:** mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum.
7. **<u>Vichekesho</u>:** aina ya sanaa ya fasihi simulizi ambayo watu hutoa vihadithi vifupi au sentensi zenye uwezo wa kuwafanya wasikilizaji wacheke.
8. **<u>Sanaa za maonyesho</u>:** Maonyesho huhusisha watu wa jamii au kundi fulani wanaoonesha taaluma, ujuzi au sanaa yao kwa watazamaji.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 8:** ***Tumia mbinu ya mchezo wa umithilishaji. Wagawe wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya wahusika katika mazungumzo husika. Kila mwanafunzi apewe jukumu lake la kuiga wakati unaokusudiwa kuwasilisha kazi hii.***

**Kuandika**

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii iwe ya nyumbani na ya kibinafsi.***

**Kazi ya 10:** ***Unda makundi mawili ya wanafunzi kulingana na viulizi viwili husika ambapo kila kundi litatunga sentensi kumi na kuzisoma hadharani.***

## 6.6. Muhtasari wa mada

"Uigizaji wa mazungumzo" ni mada ya sita katika kitabu cha mwanafunzi. Imejigawa katika masomo matatu ambayo ni yafuatayo:

1. Kuigiza mazungumzo,
2. Umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo,
3. Vifaa katika uigizaji wa mazungumzo pamoja na sifa za mwigizaji bora.

Ikumbukwe kuwa kila somo limezingatia sehemu kuu sita ambazo ni:

i. Kusoma na ufahamu.

ii. Matumizi ya msamiati maalum.

iii. Sarufi.

iv. Matumizi ya lugha.

v. Kusikiliza na kuzungumza.

vi. Kuandika.

## 6.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana haki au idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao kwa ajili ya kuimarisha shauku yao ya kuitumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

## 6.8.Tathmini ya mada ya sita

Kazi hii iwe ya kibinafsi. Hakikisha kuwa vitabu pamoja na madaftari ya wanafunzi tayari yameweka mbali kwa ajili ya kuepuka tabia ya kuibia tathmini.

1. Aina za mazungumzo na maelezo yake:

**Majibu:**

a. **Malumbano ya utani:** Mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani.

b. **Ulumbi:** Ni uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi.

c. **Soga:** Ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum.

2. Umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo ni huu ufuatao:

**Majibu:**

i. Kuunganisha watu katika jamii,

ii. Kutumiwa kama chombo cha kuburudisha katika jamii,

iii. Kuelimisha kuhusu mambo fulani,

iv. Kuleta umoja na ushirikiano,

v. Kutumiwa kuonya dhidi ya matendo mabaya,

vi. Kutumiwa kupitisha wakati,

vii. Kukuza stadi za kuzungumza lugha kwa ufasaha,

viii. Kuendeleza hisia za kujiamini katika mawasiliano kadhaa.

3. Mwigizaji wa mazunguzo anastahili kuwa na sifa zifuatazo:

**Majibu:**

Kujiamini katika mazungumzo, kuwa na ucheshi, kutumia lugha ya ishara, kuzungumza kwa ufasaha, kutumia lugha ya mkato.

4. Kwa kutegemea mifano mitatu, mazungumzo yanaweza kuigizwa hapa:

**Majibu:**

**Darasani:** Mazungumzo baina ya mwanafunzi na mwenzake.

**Sokoni:** Mazungumzo kati ya mnunuzi na muuzaji.

**Hospitalini:** Mazungumzo kati ya mgonjwa na daktari.

5. Maswali sahihi kwa sentensi zilizotolewa:

**Majibu:**

i. Barabara hii ilijengwa lini?
ii. Kwa nini mtoto wako hakuweza kufika shuleni jana?
iii. Mnakuja shuleni namna gani?
iv. Maswali mangapi yametolewa na washiriki? Nani ambaye ametoa maswali kumi?
v. Ni watu gani ambao ni muhimu katika jitihada za kuimarisha elimu bora?
vi. Nani ambaye amepiga hodi?

## 6.9. Kazi za ziada

### 6.9.1. Kazi za urekebishaji

a. Unajua nini kuhusu tamthilia katika vipindi vya Idhaa ya utangazaji nchini Rwanda?

**Jibu**

Ni shirika la wachezaji wa michezo ya kuigiza amabao huzungumzia mada mbalimbali kuhusu maisha ya Wanyarwanda ya kila siku kwa madhumuni ya kuelimisha, kurekebisha na kuburudisha.

b. Taja majina angalau manne ya wachezaji mashuhuri katika sanaa ya michezo ya kuigiza.

**Mapendekezo ya majibu:**

William Shakespeare

Ebrahim Hussein

M.S. Abdulla

Amandina Lihamba

### 6.9.2. Kazi jumuishi

a. Jaza sentensi zifuatazo kimazungumzo.

i. Watu wenye ulemavu wa kutosikia na kutozungumza huweza kushirikishwa kwenye mazungumzo kwa kutumia.........................

ii. Mazungumzo baina ya watu wawili huitwa mazungumzo ya ana kwa ana au.................................................

iii. Uigizaji wa mazungumzo hukuza stadi za ...................................... .................................................................

b. Jaza sentensi hizi kimaandishi

i. Jina jingine la mazungumzo ni ....................................................... ..........., yaani.....................

ii. Uigizaji wa mazungumzo huwa na faida za aina tatu muhimu: ..... ..........................., .................................., ..........................

iii. Ulumbi ni sawa na hotuba kwa sababu...........................................

**Pendekezo la majibu:**

a. Jaza sentensi zifuatazo kimazungumzo:

i. Watu wenye ulemavu wa kutosikia na kutozungumza huweza kushirikishwa kwenye mazungumzo kwa kutumia **ishara maalum.**

ii. Mazungumzo baina ya watu wawili huitwa mazungumzo ya ana kwa ana au **malumbano ya utani**.

iii. Uigizaji wa mazungumzo hukuza stadi za **kukariri, kuzungumza kwa ufasaha, kusikiliza kwa makini na kubuni**.

b. Kujaza sentensi hizi kimaandishi:

i. Jina jingine la mazungumzo ni **dayalojia,** yaani **utaratibu wa kuongea baina ya watu wawili au miongoni mwa watu zaidi ya mmoja au pande mbili tofauti kuhusu mada mbalimbali zinazobadilikabadilika**.

ii. Uigizaji wa mazungumzo huwa na faida za aina tatu muhimu: **faida za kielimu, kijamii na kiuchumi.**

iii. Ulumbi ni sawa na hotuba kwa sababu **mtu mmoja huzungumza mbele ya hadhira.**

### 6.9.3. Kazi za nyongeza

Tumia viulizi viwakilishi katika sentensi zifuatazo :

i. Vifaa vitano vimetumiwa.

ii. Pahali pale panatembelewa mno.

iii. Simu ya mkononi ile itatumiwa katika maigizo.

iv. Mwigizaji huyu ni mashuhuri kuliko wengine

**Majibu:**

**i.** **Vingapi** vimetumiwa?

**ii.** **Papi** panatembelewa mno?

**iii.** **Ipi** itatumiwa katika maigizo?

**iv.** **Yupi** ni mashuhuri kuliko wengine?

# MADA YA 7:

# UTUNGAJI WA INSHA

## 7.1. Uwezo mahususi wa mada

Kutunga insha fupifupi kwa kuzingatia kanuni za utungaji na masimulizi.

## 7.2. Ujuzi wa awali

Katika kidato cha pili mada ya pili, wanafunzi walisoma utungaji wa barua za aina aina (za mialiko, za kikazi au rasmi, za magazetini, za kindugu, n.k.), matangazo na ilani. Katika kidato cha tatu, walisoma utungaji wa insha kwenye mada ya nne ambamo walisoma sehemu za insha, mambo yakuzingatia katika uandishi au utungaji wa insha na aina mbalimbali za insha. Mojawapo ya stadi zilizotarajiwa kwa wanafunzi kulikuwa na stadi ya kutunga insha fulani kulingana na kichwa au mada iliyotolewa.

Wanafunzi hawa walifundishwa sifa za aya na namna ya kuandika aya nzuri. Pia, walifundishwa kufanya uchambuzi wa insha iliyotungwa huku wakibainisha mambo makuu yanayojitokeza katika insha hiyo na kisha kutoa maoni yao kuhusu mada au suala linalojadiliwa katika insha.

## 7.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile mafunzo kuhusu usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, mazingira na maendeleo endelevu pamoja na mafunzo kuhusu uzalishajimali. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika

## 7.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi, wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

**Kwa mfano mkufunzi anaweza kuwauliza:**

1. Nini maana ya insha?
2. Taja aina za insha, n.k.

## 7.5. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha mada | Malengo ya kujifunza (maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Dhana ya insha | **Maarifa na ufahamu:** Kutoa maana ya insha.<br>**Stadi:** Kuchunguza sifa za sehemu kuu za insha.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuthamini shughuli za kimaendeleo katika jamii. | 5 |
| 2 | Aina za insha | **Maarifa na ufahamu:** Kutoa aina mbalimbali za insha.<br>**Stadi**: Kutumia kwa usahihi alama za vituo katika uandishi wa insha za masimulizi na za maelezo.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuonyesha mwenendo wa kuimarisha amani na uzalendo. | 5 |
| 3 | Insha ya masimulizi | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza insha ya masimulizi.<br>**Stadi**: Kutofautisha insha ya masimulizi na ya maelezo.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kudumisha mshikamano, ushirikiano na mwingiliano bora katika jamii kupitia utunzi wa insha za masimulizi na maelezo. | 5 |
| 4 | Mwongozo wa kutunga insha | **Maarifa na ufahamu:** Kuonyesha sifa za aya<br>**Stadi :** Kutunga insha za masimulizi na za maelezo kulingana na mada husika<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kudumisha mshikamano na ushirikiano katika jamii kupitia utunzi wa insha za masimulizi na maelezo | 5 |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya saba** | | | **22** |

## SOMO LA 25: DHANA YA INSHA

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kueleza maana ya insha,
- Kutaja sehemu kuu za insha ,
- Kutumia herufi kubwa katika sentensi.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Magazeti na majarida mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya vifaa tofauti, n. k.

Mukufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.
- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea kataratasi kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo:**

***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo. Wanafunzi waeleze maana ya insha na kutaja aina zake. Pendekezo la jibu:***

Insha ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani. Utungo huu huwa na urefu wa wastani. Kisa hicho au suala hilo ndilo mada ya utungo huo. Kuna aina tofauti za insha k.v. insha za wasifu, insha ya mjadala, insha fafanuzi, insha ya methali, insha ya mdokezo, n.k.

**Kusomana kufahamu: Mchuano wa fainali**

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi apange kazi hii katika makundi ya wanafunzi kufuatana na idadi ya vitabu vya kusoma vilivyopo na kuwasaidia kuelewa maswali. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Timu hizi mbili ni shule ya wasichana ya Elimu Bora na Tusonge Mbele.
2. Timu hizo mbili zinagombania kombe la Agaciro.
3. Hapana. Timu hizi mbili ni wapinzani sugu tangu jadi na jadi.
4. Elimu Bora inajivunia historia nzuri kwa kushinda kombe hili mara

kumi. Wao ndio bingwa tetezi. Tusonge Mbele imeshinda kombe hili mara tatu. Mwaka jana walitimuliwa katika nusu fainali. Katika awamu hii, wana rekodi ya kutoshindwa katika mechi zote hadi kufikia fainali.

5. Mchezo haukumalizika kwa amani, kwasababu Elimu Bora walipopata goli la kwanza wachezaji wa Tusonge Mbele walipandwa na mori. Walimzingira refa mkuu. Walidai kuwa Uwamwiza alikuwa ameotea. Nahodha wao, Mutoni alimiminia refa maneno makali. Mutoni alionyeshwa kadi nyekundu kwa kukosa adabu.
6. Wazazi walitaka kusikiliza matokeo ya mchezo huo kwa sababu mmoja kati ya wachezaji ni dada yangu, jina lake Uwamwiza.
7. Msichana yule alipewa kadi nyekundu kwa sababu alimiminia refa maneno makali.
8. Kwa maoni yangu:

- michezo huimarisha afya yetu,
- michezo huleta umoja miongoni mwa wanajamii,
- michezo huleta fahari,
- michezo huleta pato.

9. Ndiyo kabisa. Ni vizuri kwa wasichana kucheza mchezo wa kandanda kama kaka zao. Wao pia wana uwezo sawa na kaka zao.

**Matumizi ya msamiati kuhusu kifungu cha habari**

**Kazi ya 2:** ***Katika jozi, wanafunzi watumie Kamusi ya Kiswahili Sanifu na kueleza maneno waliyopewa. Yafuatayo ni majibu:***

**Kabumbu**: Mchezo wa mpira wa mguu ( kandanda/ kipute/ gozi/ soka).

**Mchuano**: Mashindano baina ya timu mbili.

**Fainali**: Shindano la mwisho kabisa la kutafuta mshindi/ mshindaji na mshinde.

**Kuwania kombe**: Kushindania kombe/ tuzo katika mchezo.

**Wapinzani:** Kikundi cha watu wanaoshindana na wengine.

**Bingwa tetezi**: Timu ambayo iliibuka mshindi/ kuchukua kombe katika awamu iliyopita ya shindano fulani.

**Nusu fainali**: Mchezo unaotangulia fainali ambapo washindi hucheza katika fainali.

**Safu ya ulinzi**: Wachezaji ambao huzuia wapinzani kufunga mabao.

**Kiungo cha kati**: Wachezaji ambao hucheza sana katikati ya uwanja.

**Washambulizi**: Wachezaji ambao hucheza karibu na lango la wapinzani ili wafunge mabao.

**Kazi ya 3:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi akamilishe sentensi kwa kutumia maneno yaliyotolewa ambayo ni:*** kabumbu, mchuano, fainali, kuwania kombe, washambulizi, kuinua kijibendera, bingwa tetezi, refa, mashabiki, penalti.

1. Elimu Bora ndiyo **bingwa tetezi** kwa sababu walishinda mara nyingi.
2. **Refa** anachomoa kadi nyekundu na kumuonyesha Mutoni.
3. Kulikuwepo mashabiki wengi katika mchezo wa **kuwania kombe** la Agaciro nchini Rwanda.
4. **Washambulizi ndio** wanaofungia timu yao magoli mengi.
5. Mara nyingi **penalti** husababisha goli.
6. Wasaidizi wa refa wanamsaidia katika mchezo kwa **kuinua kijibendera.**
7. Timu ya Arsenal ina **mashabiki** wengi nchini Rwanda.
8. Siku hizi wachezaji wa **kabumbu** hulipwa hela nyingi.
9. Nchini Rwanda, **mchuano** wa APR FC na Rayon Sport FC unatazamwa na watu wengi sana.
10. Katika mchezo wa **fainali** kila timu inatakiwa kuwa bingwa.

**Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa**

**kazi ya 4:** ***Katika jozi, wanafunzi wajadiliane na kueleza sababu ya kutumia herufi kubwa katika sentensi zilizotolewa.***

a. Mjini Kigali panajulikana kuwa na usalama pamoja na usafi.

b. Shule ya Mtakatifu Yohana inawapokea wasichana na wavulana.

c. Jina lako ni nani? Ninaitwa Peter. Jina jingine ?

***Pendekezo la majibu:***

Herufi kubwa imetumiwa kwa kuanza sentensi na kwa majina ya pekee

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi na kila mwanafunzi achunguze makosa ya kisarufi katika sentensi na kuyasahihisha. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. **M**usanze ni mji mkubwa.

2. **K**alisa na Uwineza ni wanafunzi wenye bidii.
3. **M**iti hutupatia kivuli cha kupumzikia.
4. **M**walimu anafundisha.
5. **B**erwa anacheza mpira.

**Matumizi ya lugha: Dhana ya insha na utungaji wake**

**Kazi ya 6:** ***Katika makundi ya wanafunzi, mkufunzi awaongoze kujadiliana kuhusa mada walizopewa na kuwasilisha kazi hiyo mbele ya darasa. Kila kundi lipewe mada moja.***

a. Insha ni nini?

b. Eleza umuhimu wa kujifunza insha.

c. Insha nzuri inastahili kuwa na sifa gani?

d. Kifungu hiki cha habari ni aina gani ya insha ?

Mifano ifuatayo inaonyesha mapendekezo ya majibu ya mada ya kwanza na mada ya pili:

- **Insha** ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani. Utungo huu huwa na urefu wa wastani. Kisa hicho au suala hilo ndilo mada ya utungo huo. Insha hutumiwa kuelezea maoni ya mwandishi kuhusu masuala au mambo tofauti.
- **Umuhimu wa kujifunza utungaji wa insha:**

- Utungaji wa insha huwezesha watu kutoa maelezo, mawazo au maoni kwa njia ya maandishi au mazungumzo.
- Utungaji wa insha huwezesha utumiaji wa lugha fasaha, sanifu na uwezo wa kujieleza kwa njia ya maandishi au mazungumzo.
- Utungaji wa insha huwezesha kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu maisha yetu ya kila siku. Kupitia njia ya utungaji, watu hupata taarifa kuhusu vitu mbalimbali vinavyozunguka maisha yao ya kila siku.
- Utungaji wa insha hutumika kuelimisha, kukosoa na hata kuonya. Maandishi au mazungumzo (masimulizi) yanayotokana na utungaji huweza kuakisi hali halisi ya maisha ya jamii, na hivyo ikawa ni kama kioo cha kujitazamia na kujirekebishia.
- Utungaji wa insha, hususan unaotokana na kazi za fasihi hutumika kuburudisha jamii. Hadithi na tanzu nyingine za fasihi zinazotokana na utungaji huburudisha, huliwaza na kufurahisha jamii.

- Utungaji wa insha hutumika kukuza lugha kwa njia ya mazungumzo au maandishi. Mzungumzaji na msikilizaji hupata ufundi wa kujieleza zaidi kupitia utungaji, hali kadhalika, mwandishi na msomaji hupata ufundi wa kujieleza pia.

**Kusikiliza na Kuzungumza**

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kufikiria insha moja waliyoisikiliza au kuisoma na kuisimulia mbele ya darasa. Kazi hii iwe ya kibinafsi.***

**Mifano**: Mkutano wa viongozi wa shule, ziara uliyoifanya kwenye mbuga za wanyama, n.k.

**Kuandika**: **Utungaji wa Insha**

**Kazi ya 8:** ***Wanafunzi katika makundi ya watano watano, andikeni insha yenye mada "Umoja wa Waafrika ni msingi muhimu kwa maendeleo ya Afrika." Mambo yafuatayo yazingatiwe katika utungaji:***

- Kukuza maendeleo,
- Kukuza demokrasia barani Afrika,
- Kudumisha amani na usalama barani Afrika,
- Kuzuia ueneaji wa silaha barani Afrika,
- Kukuza haki za binadamu,
- Kuimarisha ushirikiano baina ya Waafrika wote.

## SOMO LA 26: AINA ZA INSHA

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza aina za insha,
- Kutumia nukta na mkato / koma katika sentensi sahihi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyomsaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,

- Magazeti na majarida mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya vifaa tofauti.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

iii. **Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au

kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea karatasi iliyobandikwa kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo mijadala.

**Kazi ya 1. *Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi na kuwaongoza kutazama michoro na kujadili inachoeleza. Kila kundi liwasilishe majibu yake mbele ya darasa. Majibu yaliyopendekezwa:***

Kuna michoro mitatu. Mchoro wa kwanza unaonyesha mzee akikaa mbele ya watoto. Huenda akawa anawasimulia hadithi fulani. Mchoro wa pili pia unaonyesha watoto wawili ambao wanaonekana kama mmoja anasimulia mwenzake hadithi fulani. Mchoro wa tatu unaonyesha msichana ambaye anaonekana kama anajigamba.

**Kusoma na ufahamu: Usafiwa mavazi yetu**

**Kazi ya 2: *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu wakiongozwa na mkufunzi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Vazi ni nguo ya aina yoyote inayovaliwa mwilini.
2. Kwa sababu vazi husaidia binadamu kujikinga dhidi ya hali ya hewa.
3. Mavazi ya kike, mavazi ya kiume na mavazi mahususi.
4. Mtu akivaa nguo ya mtindo fulani mara nyingi utamaduni wake au uraia wake hutambulika waziwazi.

   **Mifano:** Kuna mavazi na mitindo ya kinyarwanda, mavazi ya kimasai, ya kichina. Vitenge huonyesha utamaduni wa kiafrika. Kanga huonyesha utamaduni wa kitanzania.
5. Nguo za kijeshi, sare za wanafunzi na sare za wachezaji.
6. Ni vazi mahususi kwa sababu huvaliwa kwa wakati maalum tu.
7. Nguo hutegemeana sana na utamaduni wa jamii husika kwa sababu mtu anaweza kuvaa vazi fulani likiwa zuri kulingana na

utamaduni wake lakini likaonekana kuwa baya kwa watu wenye utamaduni tofauti na wake.

**Mifano:** kuvaa bikini, chupi, nguo fupi na kutembea barabarani, kwa Wazungu ni jambo la kawaida lakini kwa Wanyarwanda huonekana kuwa ni jambo lisilo la kawaida.

8. Chawa na viroboto.
9. Ni lazima kwa sababu jambo hili hufanyika kwa kuaangamiza bakteria walioepukana na mionzi ya jua.
10. Ni vizuri kuwa na usafi wa nguo zetu pamoja na wa miili yetu.

**Msamiati kuhusu kifungu cha habari**

**Kazi ya 3:** ***Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mkufunzi awaongoze kutafuta majina ya mavazi kwenye mraba***.

| A | ~~C~~ | V | ~~K~~ | I | T | E | N | ~~G~~ | E |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ~~H~~ | I | ~~I~~ | ~~A~~ | Z | A | P | ~~A~~ | L |
| K | ~~U~~ | R | ~~K~~ | F | ~~N~~ | M | I | ~~U~~ | U |
| T | ~~P~~ | A | ~~O~~ | F | U | ~~I~~ | E | ~~N~~ | B |
| ~~S~~ | ~~I~~ | D | ~~I~~ | R | I | A | ~~K~~ | ~~I~~ | E |
| ~~O~~ | S | H | A | T | I | K | A | ~~I~~ | G |
| ~~K~~ | A | B | U | ~~T~~ | I | U | S | N | A |
| ~~S~~ | U | R | U | ~~A~~ | L | I | I | U | N |
| ~~I~~ | S | U | K | ~~I~~ | L | O | K | B | N |
| V | E | L | I | S | U | T | I | Y | P |

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi ya watatu watatu na kuwaomba kuunganisha msamiati kutoka sehemu A na maana yake katika sehemu B. Wapewe fursa ya kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu pale inapohitajika. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. f, 2. h, 3. g, 4. i, 5. a, 6. b, 7. j, 8. e, 9. c, 10. d.

**Sarufi: Matumizi ya alama za vituo**

**Kazi ya 5:** ***Weka wanafunzi katika jozi watazame sentensi walizopewa na kuzungumzia matumizi ya alama yanayojitokeza.***

i. Usafi ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.
ii. Kalisa alienda sokoni. Alikutana na rafiki yake sokoni.
iii. Tunasoma ili tupate elimu.

- Alama inayotumiwa ni ni **nukta (.)** ambayo hutumiwa mwishoni mwa sentensi sahili.

**Kazi ya 6:** ***Kazi kwa kila mwanafunzi. Chunguza sentensi hizi na kusahihisha makosa ya kisarufi yaliyojitokeza. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Mwalimu anaandika ubaoni.
2. Mifano ya ndege ni k.v. kuku, mwewe na bata.
3. Tulianza mitihani yetu tarehe 12.12.2017.
4. Bi. Mutoni anaendesha gari.
5. Wanafunzi wanasoma darasani.

**Kazi ya 7:** ***Katika jozi, mkufunzi aongoze wanafunzi kutazama sentensi walizopewa na kuzungumzia matumizi ya alama yanayojitokeza.***

1. Nimemkuta mzee, nikamwuliza shida zake, nikamsaidia kupata gari la kumpeleka nyumbani.
2. Tumekuja kwa ajili ya akili, si kwa ajili ya pesa.
3. Baadhi ya maadili ambayo Mnyarwanda anatakiwa kuwa nayo ni kama vile utu, unyarwanda, ushirikiano na ushujaa.

***Mapendekezo ya majibu:***

Ni matumizi ya alama ya **mkato/ koma ( ,).** Alama hii imetumiwa kutenga maneno yaliyo katika orodha. Pia, alama hii imetumiwa kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume (katika sentensi ya pili).

**Kazi ya 8:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika jozi na kila jozi lisahihishe makosa ya kisarufi katika sentensi husika. Majibu yaliyopendekezwa*** :

1. Baba alinunua daftari, kalamu, rula na kifutio.
2. Mama alipofika sokoni alinunua nanasi, mkate, chungwa na parachichi.
3. Familia yetu ina watoto wafuatao: Kabanda, Kabalisa na Mukandoli.
4. Mwalimu wetu anatufundisha masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Historia.
5. Katika lugha ya Kiswhili kuna alama za uandishi kama vile: nukta, nukta-mkato, alama ya kuuliza,….

**Matumizi ya lugha: Aina za insha**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi ya watano watano na kujadili kuhusu mada walizopewa. Majibu yaliyopendekezwa:***

**9.1.** Kifungu "Usafi wa mavazi"ni insha ya wasifu kwa sababu insha hii huwasilisha sifa za vitu, watu, hali, matendo, mahali au hata sherehe uliyoihudhuria. Inalenga kutoa picha ya kitu katika akili zetu jinsi kinavyomdhihirikia anayekiona. Ili kuandika insha ya maelezo, mwandishi wake anahitaji kwanza kabisa kukusanya habari za kina kuhusu jambo analoliandika. Hategemei tu yale ambayo yanaonekana kwa macho bali pia aina nyingine za hisi kama vile kugusa, kuonja, kunusa, kusikia na kadhalika. Hali hii humwezesha msomaji kupata taswira kamilifu kuhusu jambo linaloelezwa kupitia viungo vya kuona, kuonja, kugusa na kusikia.

**9.2.** Kifungu "Mchuano wa fainali" ni insha ya masimulizi kwa sababu ni insha yenye kuhadhiria tukio au hali fulani. Ni utungo ambao husimulia au kueleza kisa. Dhima yake ni kuburudisha au kuteka umakini wa msomaji. Kwa kuwa inalenga hadhira ni muhimu kufahamu na kuitambua hadhira yako kabla ya kuandika utungo wako.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 10:** ***Wanafunzi wawekwe katika makundi ya watano watano na kuongozwa na mkufunzi namna ya kujadili mada iliyotolewa. Kazi hii ni kama mdahalo lazima kuwe na kundi linalotetea maoni fulani na kundi jingine lipinge maoni ya wenzao. Mwishowe, mkufunzi atoe hitimisho. Mambo ya kuzingatiwa ni:***

- Mavazi ya Wanyarwanda,
- Mavazi ya kigeni,
- Mtazamo wa Wanyarwanda kuhusu mavazi tofauti,
- Mavazi kufuatana na marika.

**Kuandika**

**Kazi ya 11:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi na kila mwanafunzi atunge insha ya wasifu yenye ukurasa mmoja (insha anayoitaka). Mambo ya kuzingatiwa ni:***

- Sehemu kuu za insha,
- Maana ya insha ya wasifu.

## SOMO LA 27: INSHA YA MASIMULIZI

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kueleza insha ya masimulizi,
- Kutumia alama ya kuuliza na mshangao.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyomsaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Magazeti na majarida mbalimbali,
- Ubao, chaki, kifutio (dasta/ kifuto),
- Michoro ya vifaa tofauti, n.k.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.
- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea karatasi iliyobandikiwa kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo mijadala.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi awaweke wanafunzi katika makundi ya watatu watatu, watazame mchoro na kuzungumzia wanachokiona kwenye mchoro huu. Mapendekezo ya majibu:***

- Msichana anayesimama mbele ya watoto akiwasimulia kisa fulani,
- Watoto wanaokaa chini ya mti na kumtega sikio.

**Kusoma na ufahamu: Mafanikio ya kudumu**

**Kazi ya 2:** ***Maswali haya yafanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mkufunzi awaombe wanafunzi kusoma kifungu cha habari na baadaye wajibu maswali.***

1. Kabatesi alipokuwa mtoto mdogo hakubahatika kulelewa na wazazi wake kwani walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake.
2. Kabatesi alipewa zawadi nyingi baada ya kumaliza masomo yake ya shule za Sekondari kwa kuwa alipata cheti kilichokuwa na alama

nzuri. Jambo hili liliwafurahisha watu wengi: walimu na majirani zake. Wengi waliompongeza siku hiyo walimletea zawadi nono tena nyingi.

3. Masomo ya muda mfupi aliyoyafuata yalihusu kuandaa miradi midogo midogo ya kujiendeleza na jinsi ya kuifanikisha. Aliomba mkopo ili aweze kutekeleza mengi aliyokuwa amejifunza katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo.
4. Kabatesi aliweza kufaidika kutokana na masomo ya muda mfupi akapewa cheti katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo.
5. Alipomaliza masomo yake katika shule za sekondari, Kabatesi alipata stashahada iliyokuwa na alama nzuri. Alipewa kazi ya ukalimani. Kazi hiyo ilikuwa fursa nzuri ya kuonyesha uwezo wake na kutekeleza mengi aliyokuwa amejifunza katika shule za sekondari.
6. Alikuwa msichana asiyekata tamaa na kila aliposhikilia jambo alilifuatilia mpaka lilipokamilika.

   **Mfano:** Kabatesi alikuwa na fikira nyingi kuhusu jinsi ya kutumia shamba lake kubwa ambalo alikuwa ameachiwa na wazazi wake. Kwa kutimiza mpango wake baada ya kumaliza shule zake za sekondari alisoma masomo ya muda mfupi kuhusu kuwawezesha kuandaa miradi midogo midogo ya kujiendeleza na jinsi ya kuifanikisha. Alipata kazi ya ukalimani, akafungua akaunti, akaomba mkopo kutoka benki na akatumia fedha hizo kwa kuandaa mradi wa kilimo na ufugaji.
7. Kabatesi aliweza kuboresha maisha ya watu wengine kwa kuajiri baadhi ya vijana waliokuwa pamoja katika mafunzo ya muda ule mfupi, kila mmoja akapewa jukumu lake.
8. Kabatesi alipewa tuzo kwa kubadilisha maisha ya watu wengi. Alikuwa amewapatia ajira watu wengi.
9. Alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule za chekechea hadi kiwango alichofikia. Alikuwa msichana aliye na mawazo na mtazamo imara wa maisha kiasi kwamba watu walishangaa kutokana na tabia na mienendo yake. Alifanya kazi yake kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake. Na utulivu na upendo ni baadhi ya sifa zinazomtambulisha kijana huyu ambaye amewashangaza wengi wanaomjua.
10. Kabatesi anachukuliwa kuwa mfano kwa vijana wengine kwa kuwa alijulikana kote nchini kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu. Alipewa tuzo la mtu aliyechangia kubadilisha maisha ya watu wengine.

11. Ndiyo. Ninapata funzo kwa kifungu hiki kama vile:
    - Kuwa mwanafunzi au mfanyakazi mahiri tena mwenye bidii.
    - Kutokata tamaa.
    - Kuwa na malengo/ shabaha au mipango maishani mwa mtu.
    - Kuwa mtu mwenye mawazo na mitazamo imara maishani.
    - Somo la kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu.
12. a) Mvumilivu hula mbivu: Kabatesi, wazazi wake walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake. Kabatesi baada ya kifo cha mama yake alivumilia maisha ya kuwa yatima kwa wazazi wote baadaye akawa tajiri maarufu ambaye alichangia **pakubwa** kuyaboresha maisha ya majirani zake kwa kuwapatia kazi.

    b) Mchumia juani hulia kuvulini: Kabatesi alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule za chekechea hadi kiwango alichofikia. Kabatesi alikuwa anatumia nguvu zake zote. Alifanya kazi ya ukalimani kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake. Alikuwa msichana asiyekata tamaa na kila aliposhikilia jambo alilifuatalia mpaka lilipokamilika. Aliandaa vizuri mradi wa kilimo na ufugaji, akajenga vibanda vya mifugo wake. Baadaye, alipata mali nyingi na kuanza kujulikana kote nchini kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu. Serikali ilimpatia tuzo kwa watu waliochangia kubadilisha maisha ya watu wengine. Kabatesi alikuwa miongoni mwa matajiri maarufu. Kwa machache, kabatesi alikula matunda kutoka kazi aliyoifanya kwa muda mrefu.

**Matumizi ya msamiati kuhusu kifungu**

**Kazi ya 3**: ***Mkufunzi awasaidie wanafunzi wafanye makundi ya wanafunzi wawili wawili na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa.***

1. **Kuandaa**: Mwanafunzi anatakiwa kuandaa masomo yake kabla ya kuanza wiki.
2. **Karo:** Mwanzoni mwa mwaka wa masomo, wazazi wanalipia watoto wao karo.
3. **Tafrija:** Watu walikuwa wengi katika tafrija ya ndoa ya kaka yangu.
4. **Ajira:** Waziri Mkuu anahamasisha watu kujitafutia ajira kutokana na uhaba wa kutoa kazi kwa serikali.
5. **Hodari:** Katika mbio za baiskeli, mnyarwanda hodari alishika ushindi dhidi ya wananchi wageni.

6. **Kukata tamaa**: Kijana yule alifaidika katika maisha yake kwa sababu hakukata tamaa baada ya kupambana na matatizo mengi.
7. **Akaunti:** Jirani yangu alifungua akaunti katika benki "Songa mbele" ili apate mkopo wa kumsaidia kufanya biashara.
8. **Tuzo:** wazazi wamempatia tuzo mtoto wao kwa kuwa amepata alama nzuri katika mtihani.
9. **Mradi:** Rurangwa ni tajiri siku hizi kutokana na mradi wake wa ufugaji.

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika jozi awaombe kuhusisha maneno kutoka sehemu A na maana yake katika sehemu B. Majibu:***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mkalimani | f. Mtu afasiriye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. |
| 2. Utalii | j. Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari. |
| 3. Shahada | h. Cheti au karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo. |
| 4. Mshahara | a. Malipo ya mwezi anayopewa mwajiriwa kwa kazi aliyofanya; janguo. |
| 5. Yatima | i. Mtoto ambaye mzazi wake au wazazi wote wamekufa. |
| 6. Stashahada | b. Cheti maalumu chenye hadhi ya chini kuliko shahada. |
| 7. Mtaji | c. Mali inayotumika kuanzishia au kupanulia biashara au shughuli yoyote ya kuzalisha mali. |
| 8. Mwaliko | e. Mwito wa kumtaka mtu au watu kuhudhuria mahali. |
| 9. Tabia | d. Matendo ambayo mtu amezoea kuyafanya mara kwa mara; mwenendo; mazoea; desturi. |
| 10. Kudumu | g. Kuendelea kuishi au kuwepo kwa muda wote. |

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi akamilishe sentensi kwa kutumia maneno yaliyotolewa ambayo ni: Bidii, suluhisho, inawapongeza, utulivu, jukumu, vibanda, shule za chekechea, ukalimani. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Nchini Rwanda watoto wengi wanaanzia masomo yao katika **shule za chekechea.**
2. Wanafunzi wanalazimishwa kusoma kwa **bidii** ili waweze kufaulu mtihani wa taifa.
3. Wanakijiji wengi wanaomba mkopo kutoka benki kama **suluhisho** la ukosefu wa mitaji ya kifedha.
4. Kuna uhusiano wa karibu wa kazi ya **ukalimani** na tafsiri.
5. Wanafunzi wenye tabia ya **utulivu** wanapata alama nzuri katika masomo yao.
6. Serikali ya Rwanda **inawapongeza** wasichana wanaosoma masomo ya sayansi na teknolojia.
7. Wazazi wana **jukumu** la kuwalisha na kulipa karo za watoto wao.
8. Mjomba wangu alijenga **vibanda** vitatu vya kuku wake.

**Sarufi: Matumizi ya alama za vituo**

**Kazi ya 6:** ***Katika jozi, wanafunzi watazame sentensi zilizotolewa na kuzungumzia matumizi ya alama inayojitokeza.***

i. Unasema nini ?

ii. Mnafanya nini hapa ?

iii. Je, jina lako nani ?

iv. Kwa sababu gani wototo wanaheshimu wazazi wao ?

**Jibu:** Ni matumizi ya alama ya kuuliza ( ? ) ambayo hutumiwa mwishoni mwa sentensi kuonyesha kwamba sentensi hiyo ni swali.

**Kazi ya 7**: ***Kazi hii iwe ya kibinafsi na kila mwanafunzi asahahishe sentensi zilizotolewa. Yafuatayo ni majibu:***

1. Unasoma kitabu kipi?
2. Mwalimu wako wa Kiswahili anaitwa nani?
3. Je, unakunywa chai?
4. Kwa nini unapiga kelele darasani?
5. Unachora nini?

**Kazi ya 8:** ***Katika jozi, tazameni sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama inayojitokeza.***

i. O lalala! Baba yako amekufa!

ii. Gooooo !Amefunga goli!

**Jibu:** Ni matumizi ya alama ya **mshangao ( ! ).** Alama hii hutumiwa ili kuonyesha mahangaiko au mshangao.

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi achunguze sentensi na kuzisahihisha. Yafuatayo ni majibu:***

1. Ala! Umebeba mzigo huo pekee yako!
2. Hoyee! Wanariadha wametunzwa medali!
3. Pesa yangu imeibiwa!
4. Nimepita mtihani wangu wa kitaifa!
5. Lo! Akimana ameanguka chini!

**Matumizi ya lugha: Sifa za insha ya masimulizi**

**Kazi ya 10:** ***Katika kundi la wanafunzi watano watano, mkufunzi awaongoze kueleza aina ya insha ya kifungu chenye kichwa "Mafanikio ya kudumu."***

Kifungu***"Mafanikio ya kudumu***"ni insha ya masimulizi kwa kuwa insha ya masimulizi ni insha yenye kuhadhiria tukio au hali fulani. Ni utungo ambao husimulia au kuelezea kisa. Dhima yake ni kuburudisha au kuteka umakini wa msomaji. Kwa kuwa inalenga hadhira ni muhimu kufahamu na kuitambua hadhira yako kabla ya kuandika utungo wako.

**Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano**

**Kazi ya 11**: ***Kwenye kundi la wanafunzi watano, jadilini kuhusu mada ifuatayo: Serikali ya Rwanda inawahimiza wananchi kujitafutia ajira kutokana na uhaba wa kazi. Jadili kuhusu namna ya kujitafutia kazi. Kazi hii ni kama mdahalo, mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi ya watetezi na wapinzani kisha atoe hitimisho. Mambo ya kuzingatiwa:***

- Maana ya kazi,
- Njia za kujitafutia ajira,
- Uwezo wa kibinafsi kwa mtu,
- Mwenendo wa kufanya kazi vizuri,
- n.k

**Kuandika: Utungaji wa insha ya masimulizi**

**Kazi ya 12** : ***Baada ya kusoma kifungu kuhusu insha za masimulizi "Mafanikio ya kudumu," katika kundi la watatu watatu, wanafunzi watunge insha ya masimulizi kuhusu tukio fulani, kisa au tukio la kweli au la kubuni kwa kuheshimu vipengele muhimu vya insha ya masimulizi na taratibu zake. Mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga insha ya masimulizi:***

- Insha yenye sehemu tatu: utangulizi, kiini na hitimisho,
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki,
- Kutumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada,
- Maelezo yote yatolewe kwa undani,
- Maelezo yatolewe kwa njia ya kuvutia,
- Kutumia vizuri sarufi na alama za uakifishaji, n.k.

## SOMO LA 28: MWONGOZO WA KUTUNGA INSHA

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kueleza kanuni za kutunga insha,
- Kutumia alama ya nuktambili, na nukta na mkato.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya vifaa vinavyotumiwa darasani.

Mukufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalumu. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.
- **Kazi za mzunguko darasani:** Mkufunzi hubandika kwenye kuta karatasi zenye maswali tofauti na kuwaongoza wanafunzi kuzunguka wakielekea karatasi zilizobandikwa kwenye kuta na kutoa jibu haraka ili kuwapatia fursa wenzao walio nyuma yao.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo mijadala.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo ambapo wanafunzi wanaeleza wanachokiona kwenye mchoro. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Kuna watu watatu wanaokaa wakiandikia kwenye meza
- Kuna karatasi inayoonyesha maandishi ya "mwongozo wa kutunga insha"

**Kusomana kufahamu: Siku yangu ya kwanza katika shule za mabweni**

**Kazi ya 2:** ***Maswali haya yafanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Mkufunzi awaombe wanafunzi kusoma kifungu cha habari na baadaye wajibu maswali. Mkufunzi awaongoze na asahihishe majibu watakayoyatoa. Majibu yanayopendekezwa:***

1. Wazazi wanapokaribia mwanzo wa masomo ya watoto wao huanza kujiandaa kwa kutimiza wajibu wao kwa kuandaa mahitaji yote muhimu kwa ajili ya watoto wao watakapoenda shuleni. Wakati huu wazazi huwanunulia watoto vifaa na vitu vingine vya kutumia shuleni na kuwalipia karo za shule.
2. Mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki alikuwa anakwenda kujifunza katika aina ya shule za mabweni.
3. Babake ndiye alimsindikiza mwanafunzi hadi shuleni.
4. Baba yake alimshauri kusoma kwa bidii na kutumia muda wake wa kusoma ipasavyo, kujiepusha na tabia mbaya za vijana, kutojiingiza katika makundi ya wanafunzi wabaya ambao hawazingatii maonyo na mawaidha ya wazazi wao na walimu.
5. Mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki ni mtiifu na mchangamfu.
6. Kinachoonyesha kwamba mwanafunzi huyu alipokewa vizuri mara tu alipofika shuleni ni wakati alipopiga hodi ofisini na akapokelewa kwa mikono miwili kisha akasajiliwa na akapewa kitanda cha kulala.
7. Mwanafunzi alipofika bwenini alishangaa sana kuona vitanda vingi katika ukumbi mkubwa ambapo kila kitanda kilikuwa na sehemu mbili za kulala, moja chini nyingine juu yake.
8. Wanafunzi, wakati wa jioni, walipewa chakula kizuri ambacho ni wali, maharage, mboga na matunda.
9. Walipoingia darasani mwanafunzi huyu alichukua daftari lake la somo la Kiswahili akaanza kupitia masomo yote waliyojifunza katika kidato cha tatu alipokuwa akisomea.
10. Wanafunzi walitakiwa kulala saa tatu za usiku.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3:** ***Katika kundi la wanafunzi wanne wanne, tungeni sentensi fupifupi kwa kutumia maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu hapo juu. Tumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu inapohitajika. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Kabla ya kila muhula kuanza, wanafunzi na wazazi wao wanapaswa **kujiandaa** vya kutosha ili wasije wakapata usumbufu baadaye.
2. Hawezi kuvumiliwa askari **kusaliti** nchi yake.
3. Kijana huyu hana akili: amekubali **kuuza** shamba alilorithi kutoka kwa wazazi wake.
4. Wanafunzi wasiotaka kusoma kwa **bidii** hawafaulu mitihani.
5. Wale ambao wane **tabia** za kutowaheshimu wengine hupoteza marafiki.
6. Mwanafunzi huyu ana **maadili;** kila mtu shuleni anampenda.
7. Tulipokutana alinitakia **heri na fanaka** ya mwaka mpya.
8. "Tulikutania kwenye **ukumbi** wa shule," Mwalimu Mkuu aliwambia wazazi.
9. Uwamahoro anafanya kazi ya kusajili wanafunzi wapya katika shule ya Ikirezi.
10. Wingu lilitanda kuashiria mvua kubwa.

**Kazi ya 4:** ***Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wanafunzi watumie mshale kwa kuunganisha maneno na maana zake. Mkufunzi awasaidie na atathmini majibu ya wanafunzi wote.***

1. c
2. j
3. g
4. k
5. i
6. a
7. h
8. e
9. b
10. f
11. d

**Sarufi: Matumizi ya alama za vituo**

**Kazi ya 5:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya fikiri- jozi –changia kisha ahamasishe wanafunzi kutazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama ya nuktambili.***

i. Tunaenda sokoni kununua vitu vifuatavyo : nyanya, mahindi,…

ii. Katika familia yetu kuna watoto kama : Karangwa, Mukamurenzi…

iii. Jimbo la kusini kuna wilaya kama : Ruhango, Kamonyi, Huye ….

**Jibu: Nuktambili (:)** hutanguliza maneno yaliyo katika orodha.

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Yafuatayo ni majibu:***

1. Mifano ya ndege wanaofugwa ni : kuku, bata na njiwa.
2. Baba yangu hutengeneza: meza, kiti, kitanda na kabati.
3. Familia huwa na: baba, mama na watoto.
4. Mimi huamka saa 2:00 asubuhi kila siku.
5. Mchezo wa kandanda ulianza saa10:00 jioni.

**Kazi ya 7:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya fikiri-jozi–changia.***

**Jibu: Nukta na mkato ( ; )** imetumiwa kuunganisha vishazi viwili bila kutumia viunganishi.

**Kazi ya 8:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi asahihishe sentensi alizopewa. Yafuatayo ni majibu:***

1. Kabla ya kupata chakula; ni lazima kunawa mikono; hii ni tabia nzuri.
2. Akili ni mali; kila mtu ana zake.

**Matumizi ya lugha: Taratibu za kutunga insha**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne, baadaye wasome maelezo muhimu kuhusu insha katika kitabu cha mwanafunzi na kisha wajibu maswali yaliyoulizwa. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Utangulizi ndio sehemu muhimu katika mtungo wowote wa insha kwa sababu:

- Ndiyo sehemu ambayo inampa mtu habari kamili ya mada inayozungumziwa,
- Utangulizi mzuri hufafanua malengo ya insha na jinsi malengo hayo yatakavyofikiwa,

- Utangulizi mzuri pia humfanya msomaji avutiwe na yale yatakayojadiliwa katika insha nzima.

2. Sehemu kuu za insha ni tatu, ambazo ni utangulizi, kiini na kimalizio.

Utangulizi hupaswi kuwa mrefu sana au wa kuchosha. Aya moja fupi inatosha. Iwapo sehemu hii haikuandikwa kwa ufasaha ufaao, inaweza kumfanya msomaji akose hamu ya kuendelea kuisoma insha hata ingawa insha inaweza kuanza kuvutia hapo baadaye.

Sehemu ya kiini hutoa ufafanuzi na maelezo kuhusu kichwa au hoja. Aghalabu sehemu hii huwa ndefu na yenye aya nyingi za urefu tofauti.

Katika sehemu ya kimalizio, mwandishi hujaribu kusisitiza hoja zote muhimu ambazo zimejadiliwa na kutoa msimamo wa insha yenyewe kuhusu jambo lililojadiliwa. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua.

3. Yapo mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha. Mambo hayo ni pamoja na:

- Kutambua ni mada gani ya kuandikia insha na kuielewa vyema,
- Kupanga mawazo katika mtiririko wa fikra zilizopangwa ili kujenga insha zenye kukubalika,
- Kutumia lugha yenye usahihi wa maneno na inayoeleweka,
- Kufuata taratibu za kuendesha uandishi. Kwa mfano, matumizi ya alama za uandishi, aya, herufi kubwa na herufi ndogo,
- Kupanga insha katika muundo wake, yaani kichwa, utangulizi, kiini na hitimisho.

i. Kichwa cha habari cha insha ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha.

ii. Utangulizi wa insha ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

iii. Kiini cha insha: Hii ni sehemu tunayoweza kusema ndiyo insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua.

iv. Hitimisho la insha: Hii ni sehemu ya mwisho ya insha ambayo nayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejea kwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake, anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 10**: ***Kazi hii ifanyiwe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, wanafunzi wachague mada ya kuzungumzia mbele ya darasa wakifuata muundo wa insha. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi katika kundi ametoa maoni yake kuhusu mada.***

1. **Harusi**

   Maneno haya ni muhimu kutumika: waalikwa, vyakula na vinywaji, mazingira na hali ya hewa.

2. **Mchezo uliouhudhuria**

   Mambo haya yaingizwe katika mazungumzo: Rejesta za mpira, dhana ya michezo katika kujenga afya.

**Kuandika: Utungaji wa insha**

**Kazi ya 11:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi atunge insha yenye ukurasa mmoja kuhusu mada:*** *"Siku yangu ya kwanza shuleni"* ***kwa kuzingatia sehemu kuu za insha.***

## 7.6. Muhtasari wa mada

Mada hii **"Utungaji wa insha "** ina masomo makuu manne yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, maelezo muhimu, kusikiliza na kuzungumza na utungaji. **Somo la kwanza,** linaeleza dhana ya insha na matumizi ya herufi kubwa, **Somo la pili** linaeleza aina za insha na matumizi ya alama ya nukta, na alama ya mkato, **Somo la tatu** linaeleza insha ya masimulizi na matumizi ya alama ya kuuliza na mshangao. **Somo la nne** linaeleza taratibu au mwongozo wa kutunga insha na matumizi ya alama ya nukta mbili na alama ya nukta na mkato.

## 7.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mkufunzi. Sehemu hii inamsaidia mkufunzi kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

**Sehemu kuu za insha ni:**

1. **Mada au kichwa cha insha:** Mada ya insha hutambulisha jambo linalozungumziwa katika insha. Mada ya insha haifai kuzidi maneno manane. Mara nyingi mada ya insha huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Lazima mada iwe na mvuto kwa msomaji.
2. **Utangulizi au mwanzo wa insha:** Utangulizi wa insha mara nyingi huwa ni aya moja tu. Unafaa kuvutia kwa kiwango cha juu ili kumpa msomaji hamu ya kutaka kusoma insha nzima.
3. **Mwili wa insha:** Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu inabeba ujumbe kamili wa insha nzima. Aya nyingi huandikwa hapa na ni bora aya hizi ziandikwe kwa namna ya kutiririsha matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha.
4. **Hitimisho na mwisho wa insha:** Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyoandikwa katika mwili wa insha kwa namna ya kuvutia msomaji.

## 7.8. Tathmini ya mada

**A. Masahihisho ya makosa ya kimaandishi katika mazungumzo hapa chini**

**Mgonjwa:** Hujambo daktari?

**Daktari:** Sijambo! Karibu uketi.

**Mgonjwa:** Asante daktari.

**Daktari:** Nikusaidie vipi?

**Mgonjwa:** Jina langu ni Kayitesi. Ninaumwa na tumbo sana.

**Daktari:** Pole sana Kayitesi. Tumbo lilianza kukuuma lini?

**Mgonjwa:** Tangu jana usiku. Hata sijalala. Ninaendesha na kutapika sana.

**Daktari:** Pole sana. Ulikula nini jana usiku?

**Mgonjwa:** Nilikula wali kwa kitoweo cha samaki.

**Daktari:** Mmmmhh! Wewe hunywa maji yaliyochemshwa?

**Mgonjwa:** Si kila siku daktari. Mimi hunywa maji yoyote bora yanayoonekana kuwa safi.

**B. Andika insha ya masimulizi kuhusu mada zifuatazo.**

i. Siku ya kuadhimisha mwaka mpya.

ii. Safari yangu mjini Kigali.

iii. Utoto wangu.

iv. Likizo iliyopita.

v. Siku ya kuadhimisha mwaka mpya.

**Mwelekeo wa kujibu maswali haya:**

**i. Siku ya kuadhimisha mwaka mpya**

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Umuhimu wa siku hiyo,
- Mahali na tarehe tukio lilitukia,
- Walioalikwa,
- Burudani,
- Chakula, n.k.

**ii. Safari yangu mjini Kigali.**

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Umuhimu wa kusafiri,
- Lengo la safari yangu,
- Muda wa safari,
- Mambo niliyoyaona,
- Funzo kutokana na safari, n.k.

**iii. Utoto wangu.**

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Umuhimu wa kusimulia jambo hili,
- Tabia za utotoni,
- Malezi ya wazazi wangu,
- Funzo au maadili, n.k.

iv. **Likizo iliyopita.**

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Kazi nilizozifanya,
- Mahali nilipotembelea,
- Funzo au maadili, n.k

## 7.9. Kazi za ziada

### 7.9.1. Kazi za urekebishaji

**Sahihisha makosa ya matumizi ya alama za uandishi.**

**Gasore** shikamoo daktari

**daktari** marahaba gasore karibu

**gasore** asante

**daktari** habari ya leo

**gasore** njema, lakini mimi naugua.

**Daktari** unaugua wapi gasore

**Gasore** midomo yangu imevimba.nashindwa hata kula. nahisi uchungu sana.

**daktari:** pole sana gasore

**gasore:** nishapoa

**daktari:** nitakupima kisha nitakupa dawa ya kupunguza uchungu huo.

**gasore:** asante sana daktari.

**daktari:** karibu.

**Masahihisho:**

**Gasore:** Shikamoo daktari!

**Daktari:** Marahaba Gasore. Karibu.

**Gasore:** Asante.

**Daktari:** Habari ya leo?

**Gasore:** Njema, lakini mimi naugua.

**Daktari:** Unaugua wapi Gasore?

**Gasore:** Midomo yangu imevimba. Nashindwa hata kula. Nahisi uchungu sana.

**Daktari:** Pole sana Gasore.

**Gasore:** Nishapoa.

**Daktari:** Nitakupima kisha nitakupa dawa ya kupunguza uchungu huo.

**Gasore:** Asante sana daktari.

**Daktari:** Karibu.

### 7.9.2. Kazi jumuishi

Tunga sentensi moja kwa kila alama za vituo vifuatavyo: nukta, nukta mbili, mkato, nukta na mkato, kiulizi, na mshangao.

**Mwelekeo:** Mkufunzi aeleze tena matumizi ya alama hizi kisha awamotishe kutunga sentensi hizo.

### 7.9.3. Kazi za nyongeza

Tunga insha kuhusu mkutano wa mkuu wa shule na wanafunzi wiki iliyopita.

**Mwelekeo:** Mkufunzi akumbushe wanafunzi sehemu kuu za insha na sifa zinazoambatana nazo. Kila mwanafunzi atunge insha yake.

# MADA YA 8:

# DHIMA YA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA JAMII

## 8.1. Uwezo mahususi wa mada

Kuonyesha dhima ya lugha ya Kiswahili kwa jamii ya nchi zinazozungumza lugha hii.

## 8.2. Ujuzi wa awali

Hii ni mada ya nane katika mwaka wa kwanza, mchepuo wa elimu lugha. Mada hii inazungumzia umuhimu wa lugha. Wanafunzi wa mwaka wa kwanza wana ujuzi wa awali kuhusu mada hii. Katika shule za awamu ya kwanza (kidato cha 2) wanafunzi walisoma katika mada kuu ya tatu "Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali."Mada hii iliwawezesha kujua umuhimu wa lugha katika jamii. Kwa hiyo, mada hii itakuwa rahisi kwao kufuatana na ujuzi wa awali walionao kuhusu matumizi ya lugha.

## 8.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Kupitia mada hii, wanafunzi wanapata fursa ya kujishughulisha na kazi tofauti za ujifunzaji ambazo zinasisitizia masuala mtambuka mbalimbali kama vile mafunzo kuhusu usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili pamoja na mafunzo kuhusu uzalishaji mali/ujasiriamali. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika majadiliano yao au kutoa hoja zao kwa madhumuni ya kujadili kwa undani masuala mtambuka husika.

## 8.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kidokezo cha mada ni kama kielelezo cha yaliyomo yatakayozingatiwa katika mada nzima. Kwa hiyo, jukumu la mkufunzi ni kutathmini ujuzi wanafunzi walionao kuhusu mada husika kwa kuwauliza maswali juu ya muktadha kwa ujumla. Kwa mwelekeo wa mkufunzi, wanafunzi hufaidika kugusia kiini cha mada na kujitayarisha kushiriki kikamilifu.

## 8.5.Orodha ya masomo:

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza<br><br>(Maarifa na ufahamu, stadi maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | TUONGEE KISWAHILI SANIFU | **Maarifa na ufahamu:**<br>• Kufafanua maana ya lugha kama chombo cha mawasiliano.<br>• Kuonyesha matumizi ya hali ya kuamrisha.<br>**Stadi:** Kuonyesha kimazungumzo na kimaandishi maana ya lugha.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujivunia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. | 7 |
| 2 | **MAWASILIANO YETU** | **Maarifa na ufahamu:**<br>• Kufafanua maana ya lugha kama chombo cha mawasiliano.<br>• Kuonyesha matumizi ya hali ya kuamrisha.<br>**Stadi**: Kulinganisha umuhimu wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine katika mawasiliano ya kila siku katika jamii ya Wanyarwanda.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuheshimu lugha kama chombo cha kuimarisha umoja na ushirikiano katika jamii. | 7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | UMUHIMU WA LUGHA | **Maarifa na ufahamu:**<br>• Kueleza umuhimu wa lugha katika jamii.<br>• Kuonyesha matumizi ya hali ya kuamrisha.<br>**Stadi**: Kulinganisha umuhimu wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine katika mawasiliano ya kila siku katika jamii ya Wanyarwanda.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kujivunia lugha kama chombo cha kuiendeleza jamii. | 6 |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya pili** | | | **22** |

## SOMO LA 29: TUONGEE KISWAHILI SANIFU

i. **Malengo ya ujifunzaji**

- Kutoa maana na umuhimu wa lugha,
- Kusoma na kuelewa kifungu kuhusu lugha kama chombo cha mawasiliano,
- Kusikiliza kwa makini na kusimulia kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kujadili namna ya kuitunza lugha na mwenendo unaofaa.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya watu wanaowasiliana.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humwacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv. Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo vidokezo.

**Kidokezo:**

***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kuwaongoza kujadili kidokezo walichopewa. Mbinu ya bunguabongo itumiwe ili kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mapendekezo ya majibu:***

a. **Lugha hizo ni**: Kinyarwanda, Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa.

b. Dhima nne za lugha ya Kiswahili ni: Kurahisisha mawasiliano, hutumiwa katika biashara, hutumiwa katika kupata habari, hutusaidia kujipatia marafiki.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo na kuomba wanafunzi kuchunguza mchoro na kujadili kinachofanyika kwenye mchoro huo. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Kuna watu wanaofanya kazi ya useremala, ushonaji na uuzaji. Katika mchoro huu, inaonekana kwamba wahusika hawa wanaongea.

**Kusoma na ufahamu: Kiswahili nchini Rwanda**

**Kazi ya 2:** ***Kazi hii ifanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wasome kifungu cha habari na kuhakikisha kuwa wanakielewa. Majibu ya maswali ya ufahamu:***

1. Kinyarwanda, Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili.
2. Kutokana na ushirikiano wa Rwanda pamoja na nchi jirani zake ambayo ni Kenya, Tanzania, Uganda, Jumhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi zinazotumia lugha ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali. Sababu nyingine ni ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi; hivyo kinafundishwa shuleni, kinatangazwa katika vyombo vya habari tofauti, n.k.
3. Kiswahili ni lugha ya mawasiliano kati ya watu, kinatumiwa katika kufanya biashara, na kinasaidia katika kuleta amani. Lugha ya Kiswahili pia hufundishwa shuleni.
4. Shule za sekondari zote hasa hasa za awamu ya kwanza, na nyingine nyingi zenye mikondo ya lugha (LKK) na vyuo vikuu mbalimbali vikiwemo Chuo Kikuu cha Rwanda Koleji ya Elimu, n.k.
5. Ndiyo. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya mawasiliano kwa sababu hutumiwa katika maisha ya kila siku, shuleni, sokoni na katika vyombo vya habari mbalimbali.

**Matumizi ya samiati kuhusu dhima za lugha ya Kiswahili**

**Kazi ya 3**: ***Omba wanafunzi watoe maana za maneno yaliyoko kwenye ukurasa husika katika makundi ya wanne wanne. Watumie mbinu ya utafiti na ya fikiri -jozi –changia kisha mkufunzi awaongoze katika kutafuta maana za msamiati huu huku wakichangiana mawazo katika kutoa jibu sahihi. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. **Dhima**: wajibu mkubwa, pamoja na uwezo wa kufanya jambo (jukumu, kazi, umuhimu).

   **Mfano: Dhima** kuu ya lugha ni mawasiliano.

2. **Ushirikiano**: Hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli, uelewano, changamano.

   **Mfano**: Nchi za Afrika zinapaswa kuwa na **ushirikiano** ili ziwe na soko moja.

3. **Kupashana**: Peana taarifa au habari kati ya mtu na mtu au chombo kimoja na chombo kingine.

   **Mfano**: Kupashana habari katika shirika lolote huonyesha msimamo mzuri wa uongozi wake.

4. **Maarifa**: mbinu ya kufanya jambo, elimu au ujuzi aupatao mtu kwa kusoma au kutenda.

   **Mfano**: Mtu anayesoma vitabu sana hupata **maarifa** na kuerevuka.

5. **Utamaduni**: Mila, desturi, asili, jadi, imani na itikadi za kundi la watu au jamii fulani.

   **Mfano**: Mimi ninaupenda **utamaduni** wa Wanyarwanda kwa sababu ya ukarimu wao.

6. **Jamii**: Mkusanyiko wa watu au vitu.

   **Mfano**: Jamii ya Wanyarwanda inahimizwa kufanya kazi yoyote kwa bidii ili iweze kuepukana na umaskini.

7. **Mzawa**: Mtu aliyezaliwa mahali fulani, mtu mwenye asili ya mahali fulani.

   **Mfano:** Mwalimu Julius Nyerere ni mzawa wa nchi ya Tanzania.

**Sarufi: Matumizi ya hali ya kuamuru**

**Kazi ya 4**: ***Ambia wanafunzi kutazama michoro na kueleza kinachofanyika pale. Mkufunzi atumie mbinu ya makundi, kisha wanafunzi wajibu walichoona kwenye mchoro. Majibu yanayopendekezwa:***

1. Kwenye mchoro wa 1: Tumeona afande ambaye anasimama mbele ya jeshi lake. Anaweza kuwa anatoa amri.
2. Kwenye mchoro wa 2: Tumeona vijana wawili ambao wanasukuma gari linaloonekana kuwa limekwama matopeni.

**Kazi ya 5**: ***Ambia wanafunzi watunge sentensi tano kwa kutumia hali ya kuamuru. Hii ifanyike katika jozi. Mmoja asimame mbele ya darasa kisha aamrishe mwenzake wafanye hivyo mpaka mkufunzi ahakikishe ikiwa wameelewa kutumia hali ya kuamuru katika umoja na wingi.***

a. Nyamazeni! Watoto wangali kitandani wanahitaji kusinzia.

b. Fanya kazi yako haraka! Tunachelewa.

c. Kuleni chakula hiki kabla hakijapoa!

d. Someni kitabu cha fasihi ya Kiswahili na kutusimulia maudhui yake!

e. Lete pesa zangu nataka kununua viatu!

**Kazi ya 6:** ***Omba wanafunzi wakamilishe sentensi kwa kutumia hali ya kushurutisha kwa vitenzi ambavyo vimo katika mabano. (Hapa mbinu ya fikiri-jozi-changia itumiwe).***

1. ***"Fanya*** kazi yako ya shule kuhusu dhima ya kiswahili!" Mama alimuamrisha mtoto wake.
2. Mwalimu alimuomba mwanafunzi akisema: "…***futa*** ubao tufanye mazoezi!"
3. Baada ya kujiunga na nchi nyingine za Afrika Mashariki viongozi wa Rwanda walituambia: "***zungumzeni*** Kiswahili!"
4. Kwa kuwa wewe ni mkazi wa nchi ya Rwanda ***ongea*** vizuri lugha ya Kinyarwanda!
5. Mwalimu ameniambia kuwa "mtafanya jaribio la Kiswahili kesho; kwa hiyo ***rudieni*** masomo yenu!"
6. Mwalimu aliwaambia wanafunzi: "***tazameni*** runinga kuna mchezo wa kuigiza uhusuo uhifadhi wa mazingira!"
7. Katibu aliombwa na mwenyekiti: "***andika*** mawazo yote yatakayotolewa mkutanoni!"
8. Kama unataka kukuza stadi zako za kuzungumza na kusikiliza lugha ya kiswahili, ***sikiliza*** matangazo ya redioni na utazame runinga!

**Matumizi ya Lugha: Maana na umuhimu wa lugha katika jamii**

**Kazi ya 7:** ***Omba wanafunzi wapange kwa utaratibu unaofaa maneno waliyopewa katika kitabu cha mwanafunzi ili yaweze kuleta maana kamili. Kazi hii itafanyika kwa jozi. Na mkufunzi atumie pia mbinu ya bunguabongo, fikiri-jozi-changia na nyingine ile inayoweza kumsaidia kufikia lengo la somo lake.***

1. Kiswahili ni lugha muhimu sana katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.
2. Hapo mwanzoni lugha ya Kiswahili ilikuwa ikitumiwa kama lugha ya biashara.
3. Wanyarwanda walifurahi sana kusikia kwamba lugha ya Kiswahili ni moja wapo ya lugha rasmi nchini Rwanda.

**Kazi ya 8:** ***Ambia wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia maneno yanayopatikana katika kitabu chao. Kazi hii ifanyike katika makundi ya watu watatu. Mapendekezo ya majibu:***

1. Nchi zote zilikubaliana kujenga **jumuiya** bora.
2. **Utamaduni** wetu ni mzuri tunapaswa kuutunza.
3. Baadhi ya **matangazo** ya Redio yanahusu usawa wa kijinsia
4. Jamii ya Wanyarwanda inahimizwa kuendelea kutunza utamaduni wao.

**Kusikiliza na Kuzungumza: Umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii**

**Kazi ya 9:** ***Omba wanafunzi wajadili kuhusu dhima za lugha ya kiswahili au umuhimu wake kwa jamii ya Wanyarwanda. Kazi hii ifanyike katika makundi na kuwasilishwa mbele ya darasa.***

**Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari**

**Kazi ya 10:** ***Ambia wanafunzi watunge kifungu kifupi (mistari kumi) wakionyesha faida ya Rwanda kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii itakuwa kazi ya kibinafsi.***

## SOMO LA 30: MAWASILIANO YETU

### i. Malengo ya ujifunzaji

- Kufafanua maana ya lugha kama chombo cha mawasiliano.
- Kutumia kwa ufasaha hali ya kuamuru katika sentensi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya watu wanaowasiliana.

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa, kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

**iv.** **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo mijadala.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo na kuomba wanafunzi kujadiliana katika makundi wanachoona kwenye picha husika. Pendekezo la jibu:***

- Kuna vijana wawili wanaosikiliza redio,
- Mvulana na msichana wanaozungumza kwenye simu,
- Kijana na msichana wanaotazama runinga.

**Kusoma na ufahamu: Ziara ya mjini**

**Kazi ya 2:** ***Kazi hii ifanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu. Mkufunzi achunguze ikiwa wanafunzi wote wanasoma na kuelewa kifungu cha habari. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1. Mugisha, Ange, Lidia, Masengesho, Rukundo na Ruhara.
2. Alishangazwa na watu waliokuwa wanazungumza lugha ngeni kwake kuisikia.
3. Hakuwa na uwezo wa kuzungumza lugha iliyotumiwa pale. Alisaidiwa na Ange na wenzake ambao walielewa lugha ya Mugisha.
4. Walikuwa wanazungumza Kiswahili lakini walipotambua kuwa Mugisha hakijui Kiswahili wakaamua kuzungumza lugha ya Kinyarwanda. Inawezekana walimtambua kuwa ni Mnyarwanda.

5. Aliogopa kuibwa au kusumbuliwa.
6. Wasichana walimnunulia chakula na chai akala na kushiba. Pia, walimfundisha maneno machache ya kiswahili.
7. Ningerejea nyumbani na kuanza kujifunza lugha zaidi ya moja na ningeanzia kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ndiyo iliyoniletea shida katika ziara yangu.

**Matumizi ya msamiati**

**Kazi ya 3**: ***Omba wanafunzi watoe vinyume vya maneno yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Kazi hii ifanyike katika jozi.***

1. Mzee ≠ kijana
2. Mji ≠ kitongoji
3. Haraka ≠ pole
4. Lugha nzuri ≠ lugha mbaya/mbovu
5. Karibu ≠ mbali

**Kazi ya 4:** ***Ambia wanafunzi wajaze sentensi walizopewa kwa kutumia msamiati unaofaa kama ulivyotumiwa katika kifungu walichokisoma. Hii ni kazi ya kufanya kwa mbinu ya fikiri-jozi-changia.***

1. Bwana Mugisha alisaidiwa na ***mabinti*** wawili waliomnunulia ***chakula*** akala akashiba.
2. Miaka miwili iliyopita ***Ruhara*** alikwenda mjini ***Arusha*** katika ***mkutano*** wa waumini.
3. Ange na ***Lidia/Masengesho*** waliongea lugha ya ***Kiswahili*** na lugha ya ***Kinyarwanda***.
4. Mugisha alidhani wasichana walikuwa ***wezi*** na kukimbia.

**Kazi ya 5:** ***Ambia wanafunzi waeleze maneno yanayopatikana katika kitabu chao. Mwanafunzi mmoja ashirikiane na mwenzake katika jozi.***

a. **Mkoba**: Mfuko uliosukwa au kutengenezwa kwa ngozi wa kuwekea vitu kwa mfano nguo, vitabu, mafaili, n.k.

b. **Jamaa**: Ndugu uliozaliwa nao au unaohusiana nao kwa karibu sana,watu unaofahamiana nao au kufanya kazi nao, mtu asiyefahamika jina au atokako.

c. **Mkutano:** Kongamano la watu wanaojadiliana juu ya jambo au wanaosikiliza hotuba.

**d. Kutoka:** Nahau inayomaanisha kuvaa vizuri sana.

**e. Fikra**:Ni mambo aliyonayo mtu katika ubongo wake kuhusu jambo analoliwaza au kutafakari, mawazo.

**f. Binti**: Mzaliwa wa kike wa wazazi, mtoto wa kike wa….

**g. Mbio**: Mwendo wa kasi au upesi.

**h. Kuaga**: Kuambia mtu kwaheri, kusema buriani.

**Kazi ya 6:** ***Ambia wanafunzi wakamilishe sentensi walizopewa ili zilete maana kamili kwa kutumia msamiati waliopewa: lugha, mawasiliano, televisheni, simu na ishara.***

1. Kiswahili ni ***lugha*** ambayo inatumiwa katika ***Jumuia*** ya Afrika Mashariki.
2. Jamila hufuata vipindi vya ***televisheni*** kila siku.
3. Wasichana watapigiwa ***simu*** na mzee Karinda.
4. Mtu asiye na ujuzi wa lugha lazima atumie ***ishara***.

**Sarufi: Hali ya kuamuru**

**Kazi ya 7:** ***Omba wanafunzi wasome mazungumzo waliyopewa na kubainisha vitenzi vilivyotumiwa katika hali ya kuamuru. Kazi hii wataifanya katika makundi ya wanafunzi watatu watatu.***

**Jibu:**Vitenzi vilivyotumiwa katika hali ya kuamuru ni: nenda, Jitayarishe, uchukue, uende, niandalie, usisahau, fanya, mwekee.

**Kazi ya 8**: ***Ambia wanafunzi watunge sentensi tatu kwa kutumia hali ya kuamuru tungo yakinishi. kazi hii ifanywe wakitumia mbinu ya fikiri-jozi-changia.***

**Mifano:**

- Lima shamba lako kabla mvua haijanyesha!
- Acha kudanganya useme ukweli!
- Nenda sokoni ukanunue chumvi na mafuta ya kupikia!

**Kazi ya 9:** ***Omba wanafunzi watunge sentensi tatu zenye vitenzi vilivyoko katika hali ya kuamuru, tungo kanushi. Kazi hii ifanywe kwa kutumia mbinu ya fikiri-jozi-changia.***

**Mifano:**

- Usikate miti kwani serikali yetu imekataza hilo!

- Msifanye uzinifu ndipo mtaeupukana na maradhi ya zinaa!
- Usichelewe shuleni ndipo utashinda masomo yako!

**Kazi ya 10:** ***Ambia wanafunzi wabadilishe sentensi ziwe katika hali ya kuamuru katika wingi. Kazi hii ifanyike katika jozi ya wanafunzi.***

a. Njooni hapa mtusalimuni!

b. Kimbieni ili msichelewe shuleni!

**Matumizi ya lugha: Mawasiliano yetu**

**Kazi ya 11:** ***Omba wanafunzi wajadili maswali waliyopewa kisha wafanye hayo katika makundi kulingana na idadi ya wanafunzi. Majibu yaliyopendekezwa:***

1. **Mawasiliano** ni upashanaji wa habari kwa kutumia mdomo, barua, simu au vyombo vya habari k.m. redio, televisheni, n.k.
2. Huwasiliana kwa njia ya sauti au ishara.
3. Mawasiliano yanawawezesha watu kupata habari ama uelewano.

**Kazi ya 12**: ***Ambia wanafunzi wajibu maswali kutoka katika kitabu chao na kuyajibu kwa jozi.***

1. Huwasiliana kwa njia ya ishara.
2. Watu hutumia lugha lakini viumbe wengine hutumia ishara na sauti.
3. Kiswahili kinaweza kutumiwa katika matangazo ya redio na televisheni, kinaweza kutumiwa shuleni, kinaweza kutumiwa katika utawala, kinaweza kutumiwa katika biashara, n.k.

**Kazi ya 13:** ***Ambia wanafunzi waseme ikiwa kuna mawasiliano ya lugha, ya ishara au ya sauti kulingana na picha wanazoziona kitabuni na kujaza jedwali walilopewa.***

| Mawasiliano ya lugha | Mawasiliano ya ishara au sauti |
|---|---|
| **Baba na watoto** | **Chui** |
| Msichana | **Njiwa** |
| | Panzi |
| | Chatu |

**Kusikiliza na Kuzungumza**

**Kazi ya 14**: ***Ambia wanafunzi kujadili kauli hii: "Mawasiliano ya lugha ni bora kuliko mawasiliano ya ishara na sauti." Kazi hii inaweza kufanywa kwa mazungumzo darasani ama kwa njia ya mdahalo ambapo upande mmoja huweza kutetea mada na upande mwingine huweza kuipinga.***

**Kuandika: Utangazaji wa insha**

**kazi ya 15.** ***Omba wanafunzi watunge insha fupifupi wakionyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda. Kazi hii iwe ya nyumbani na wanafunzi wamkabidhi matokeo yao kipindi kijacho. Mkufunzi asahihishe kazi hii akitilia maanani makosa ya kisarufi, kiothografia na kisintaksia.***

**Kazi ya 16:** ***Ambia wanafunzi waandike aya mbili kuhusu "Umuhimu wa mawasiliano." Kazi hii iwe ya mwanafunzi binafsi.***

## SOMO LA 31: UMUHIMU WA LUGHA

**i. Malengo ya ujifunzaji**

- Kueleza umuhimu wa lugha katika jamii,
- Kutumia hali ya kuamrisha katika sentensi.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya watu wanaowasiliana

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hapa, mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika harakati za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi anastahili kutumia mbinu tofauti kama vile:

- **Mbinu ya bunguabongo:** Hapa kila mwanafunzi hupewa fursa ya kutoa hoja zake hadharani juu ya swali, kauli au msimamo fulani. Mkufunzi hutega sikio hoja hizo na kuwaongoza wanafunzi kugusia jibu sahihi.
- **Mbinu ya fikiri – jozi – changia:** Mbinu hii huwashirikisha wanafunzi wawili wawili katika majadiliano yao na kisha kuwasilisha matokeo ya majadiliano hayo hadharani.
- **Kazi katika makundi:** Mkufunzi huwagawa wanafunzi katika makundi madogomadogo na kulipatia kila kundi kazi ya kushughulikia. Jukumu la mkufunzi hapa ni kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao kwa kusisitizia adabu na maadili mema katika majadiliano yao. Baada ya muda uliokuwa umetolewa kuwadia, kila kundi huwasilisha kazi yake mbele ya darasa ambapo mkufunzi huchukua jukumu kama la refa uwanjani.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Mbinu hii humuacha mwanafunzi kujitegemea, kutumia na kukuza stadi zake za kujiamini bila msaada mwingine. Anaweza kupatiwa kazi za nyumbani, za utafiti na hata za shuleni kama vile kujibu maswali ya ufahamu, kutunga na kujaza sentensi, n.k.
- **Michezo ya umithilishaji:** Mbinu hii imetiliwa maanani katika uigizaji wa mazungumzo ambapo wanafunzi hukariri mazungumzo na kuyaigiza darasani.
- **Mijadala darasani:** Hii ni mbinu ambayo wanafunzi hupewa jambo la kuzungumzia wakalitolea hoja.
- **Kazi za utafiti:** Wanafunzi hupatiwa kazi ambayo itahitaji ziara au matembezi kwenye mazingira mbalimbali, katika maktaba au kwenye kompyuta kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani.

iv. **Majibu:** Sehemu hii inaonyesha majibu yaliyopendekezwa kwenye maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi. Ingawa majibu haya yalipendekezwa, kuna majibu mengine ambayo yanaweza kutolewa na wanafunzi yakiwa sahihi kulingana na jinsi swali lilivyoulizwa hasa hasa kwenye maswali yahusuyo mijadala.

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi atumie mbinu ya bunguabongo na kuomba wanafunzi kueleza wanachokiona kwenye mchoro. Majibu yaliyopendekezwa:***

- Kuna duka kuu lenye aina tofauti za bidhaa,
- Kuna muuzaji na mnunuzi wanaojadiliana bei,
- Mhasibu anayefanya hesabu zake.

**Kusoma na ufahamu: Umuhimu wa lugha**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu acunguze kama wanasoma na kukielewa. Yafuatayo ni majibu:***

1. Watu wanaozungumziwa katika kifungu hiki ni mzee Yakobo, Petero, Maria, Bi. Hassani na Musoni.
2. Mzee Yakobo alikuwa anawahimiza watoto wake kujifunza lugha mbalimbali kwa madhumuni ya maisha yao ya usoni.
3. Maria amepewa kazi katika kitengo cha utalii katika Taasisi inayoshughulikia masuala ya utalii na mazingira.
4. Yakobo alikuwa na lengo la kwenda kumtembelea dada yake aliyeishi katika nchi jirani.
5. Petero alilipa shilingi zaidi kwa mkate mmoja na hata hivyo akapewa mkate uliopitisha tarehe ya kuula.
6. Bi. Hassani ameonyesha tabia mbaya dhidi ya mteja wake kwa kumtoza shilingi nyingi kwenye mkate mmoja na kuuza kimakusudi chakula kibovu.
7. Petero angekula chakula hicho kingeweza kuharibu afya yake.
8. Petero alijuta akisema "Nisingepuuza mawaidha ya baba yangu, nisingekumbana na matatizo haya." Alijuta kwa sababu hakuweza kuwasiliana na mfanyabiashara kwa hiyo akapoteza shilingi zake bure.
9. Aliporudi nchini Rwanda alianza kujifunza Kiswahili kwa bidii.
10. Kutokana na kifungu hiki cha habari nimejifunza kuwa ujuzi wa lugha zaidi ya moja ni muhimu sana kwa kila mtu; hivyo ni lazima tujifunze lugha mbalimbali.

**Msamiati kuhusu umuhimu wa lugha**

**Kazi ya 3:** ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo huku wakizingatia matumizi yake katika kifungu cha habari walichokisoma. Hapa mkufunzi atumie mbinu ya fikiri-jozi-changia au makundi.***

Mkufunzi ahakikishe kwamba wanafunzi wanaandika sentensi sahihi wakitumia maneno waliyopewa na awaelekeze panapohitajika. Hii ni mifano ya sentensi ya maneno husika:

1. Mwalimu **huwahimiza** wanafunzi kujifunza kwa bidii masomo yote.
2. Alianzisha shule kwa **madhumuni** ya kusaidia watoto wenye ulemavu.
3. Ni vizuri kusikiliza **mawaidha** tunayopewa na viongozi wetu.
4. **Mtazamo** wangu kuhusu jambo hilo ni tofauti na mitazamo yenu.
5. Mtoto huyu ni **mtukutu**, hasikii mawaidha ya babake.
6. **Utalii** unaleta wageni wengi nchini Rwanda.
7. Mwanafunzi ameomba mwalimu ruhusa ya **kwenda haja.**
8. Amepokea habari hiyo **kwa shingo upande.**
9. Alishinda mtihani wa taifa baada ya kusoma masomo yote kwa **bidii**.
10. Alipigwa na **bumbuazi** aliposikia habari hiyo na akakosa la kufanya.

**Kazi ya 4:** ***Mkufunzi aombe wanafunzi kuoanisha maneno katika sehemu A na maana zake zilizopo katika sehemu B. Maneno haya yaandikwe kwenye flip chati na kubandikwa kwenye ukuta darasani. Kila mwanafunzi aandike kwenye karatasi maana ya kila neno na kuihusisha na maneno yaliyoandikwa kwenye flip chati.***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Inayoshughulikia | l) Iliyo na harakati za kutekeleza jambo fulani |
| 2. Mtazamo | i) Namna ya kuangalia au kutazama kitu au mtu |
| 3. Madhumuni | g) Sababu ya kufanya jambo; kusudi; nia; lengo |
| 4. Alijitihadi | m) Alifanya jambo kwa bidii |
| 5. Aliyazingatia | j) Aliyatia moyoni na kuyafikiria |
| 6. Wasafiri | b) Watu wanaokwenda au walio katika safari |
| 7. Bumbuazi | h) Hali ya kuwa kimya na kutojua la kufanya au kutosikia lisemwalo |
| 8. Bidii | f) Hamu ya kufanya jambo, juhudi |

| | |
|---|---|
| 9. Mazingira | k) Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anapoishi au maisha yake |
| 10. Mawaidha | c) Maneno ya maonyo au ya mafunzo yenye mwongozo na mashauri |
| 11. Kupuuza | e) Kuacha kutia maanani, kudharau |
| 12. Shingo upande | n) Hali ya kutoridhika, kutopenda, kuchukizwa |
| 13. Kwenda haja | d) Kwenda chooni kwa ajili ya kujisaidia haja ndogo au kubwa |
| 14. Maarufu | a) Enye kujulikana kila mahali, mashuhuri. |

**Kazi ya 5:** ***Ongoza wanafunzi katika kujaza nafasi kwa kutumia maneno mwafaka yafuatayo: bidii, madhumuni, kupuuza, maarufu, mawaidha, mtazamo, bumbuazi, ratiba, kwenda haja, shingo upande. Hapa mkufunzi atumie mbinu ya fikiri-jozi-changia au ya makundi. Majibu yanayopendekezwa:***

1. Madhumuni
2. Ratiba
3. Bidii
4. Bumbuazi
5. Mawaidha
6. Kwenda haja
7. Mtazamo
8. Shingo upande
9. Maarufu
10. Kupuuza

**Sarufi: Matumizi ya hali ya kuamuru**

**Kazi ya 6:** ***Onyesha wanafunzi kifungu cha habari cha kusoma kwa jozi na kubainisha vitenzi vilivyotumiwa katika haliya kuamrisha. Majibu yaliyopendekezwa:***

Ona, uelewe, uache, jaribu, soma, usiendelee, soma, kimbia.

**Kazi ya 7:** ***Ambia wanafunzi watunge sentensi tano zenye vitenzi mbalimbali katika hali ya kuamuru kwa makundi ya watatu watatu. Mapendekezo ya majibu:***

a. Nyamaza wewe! Baba na mama wanasali chumbani.

b. Simama hapo ueleze uliyoyafanya!

c. Fanyeni kazi hii twende kulala!

d. Tazameni mchoro unaohusu uhusiano wa kifamilia!

e. Kimbieni msije mkachelewa shuleni!

**Kazi ya 8**: ***Hakikisha kuwa wanafunzi wanatazama picha hizi kisha wanatunga sentensi katika hali ya kuamuru kulingana na vitendo vinavyoendelea kwenye picha. Kazi hii ifanyiwe katika jozi.***

**Mifano:**

- Andika haraka mkurugenzi wa shule anakutaka!
- Rukeni fisi yule mkali asiwaue nyote!
- Kula haraka imetimia saa nne asubuhi!
- Acha wewe chui! Usimwue mnyama ye yote!
- Mpige simba amemwua nyoka huyu!
- Amka wewe simba nyani anataka kukupiga fimbo mgongoni!
- Toka mbele zangu wewe chui usimle paa huyu!
- Nisaidie sokwe! Chui anataka kunila.
- Rudi hapa, unaenda wapi!

**Kazi ya 9:** ***Chunguza kazi za wanafunzi wakiandika katika makundi ya watu watatu vitenzi vilivyopigiwa kistari katika hali ya kuamuru tungo yakinishi au kanushi:***

Hutembelea: Tembelea/Usitembelee

Husafisha: Safisha/Usisafishe

Kuhifadhi: Hifadhi/Usihifadhi

Huwazuru: Wazuru/Usiwazuru

Akiwashawishi: Washawishi/Usiwashawishi

Aliamua: Amua/Usiamue

Kufanya: Fanya/Usifanye

Akiwajengea: Wajengee/Usiwajengee

**Kazi ya 10:** ***Waongoze wanafunzi kuweka sentensi zifuatazo katika hali ya kuamuru katika umoja na kuwakumbusha kufanya mabadiliko ya kisintakisia katika sentensi panapohitajika. Majibu yaliyopendekezwa:***

a. Sauti ya pili, ingia uimbie Bwana!

b. Tetea maendeleo ya lugha ya kiswahili!

c. Kula nyama yote pia osha vyombo!

d. Lia kwa sauti ndogo jambazi lisituvamie!

**Matumizi ya lugha: Umuhimu wa lugha**

**Kazi ya 11:** ***Hakikisha kuwa wanafunzi wanasoma maelezo kitabuni na kujibu maswali ya kazi husika. Kazi hii ifanyike katika jozi au katika makundi. Majibu:***

1. Ni kwa sababu chombo hiki hutumiwa kuwasilisha amali, mila na desturi zote za jamii.
2. Kuwafanya watu wawasiliane kwa kupashana habari.
3. a) Faida za kutumia lugha moja:

- Maendeleo huwezekana haraka kwa sababu watu huelewana bila shida na hata nchi ikitoa tangazo au habari fulani kwa wananchi huwa na uhakika kuwa ujumbe umeeleweka.

b) Hasara za kujua lugha moja:

- Huweza kukosa habari zilizo katika lugha nyingine.
- Huwa na marafiki wachache ukilinganisha na yule anayejua lugha nyingi, n.k

**Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano**

**Kazi ya 12:** ***Wape wanafunzi fursa ya kujadili katika makundi kazi waliyopewa wakishirikiana na kutoa majibu sahihi.***

1. Kukosa habari, kukosa uelewano au mfarakano, kutofanya lo lote, kutopendana, kukasirika, n.k.
2. Kupata habari, uelewano, amani, urafiki, n.k.
3. ujuzi mdogo wa lugha, ujuzi wa lugha moja, n.k.

**Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha habari**

**Kazi ya 13:** ***Kwa kutoa hoja zenye mifano, hakikisha kuwa wanafunzi wanatunga kifungu cha habari kwa kutumia mada isemayo:***

"Lugha inapotumiwa vizuri hujenga jamii na ikitumiwa vibaya huangamiza jamii." Kazi hii iwe ya nyumbani na ya kibinafsi.

**Kazi ya 14**: ***Mkufunzi awaongoze wanafunzi katika kuchagua mada moja kati ya hizi kisha wabuni insha yao. Hapa kazi ifanywe katika makundi au iwe kazi ya kibinafsi na ifanyiwe nyumbani.***

Mkufunzi achunguze kama: hoja zilizotolewa ni nzuri, mwanafunzi hakuenda nje ya mada, mwanafunzi amefuata mbinu bora za kuandika insha. Mkufunzi asahihishe makosa yanayojitokeza hasa hasa ya kiothografia na kisintaksia.

**Mada za kuchagua:**

- Lugha ni kitambulisho cha jamii,
- Lugha hurahisisha mawasiliano katika jamii,
- Lugha hukuza utamaduni,
- Lugha huburudisha.

## 8.6. Mhutasari wa mada

Mada hii ya nane **"Dhima ya lugha ya kiswahili katika jamii"** ina masomo matatu yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: Kusoma na ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza na kuandika.

Soma la kwanza linaitwa **"Tuongee Kiswahili Sanifu"** ambalo linazungumzia lugha ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano." Somo la pili ni **"Mawasiliano yetu"** ambapo kumeelezwa njia tofauti zinazotumiwa katika mawasiliano. Somo la tatu ambalo ni la mwisho linahusu "**Umuhimu wa lugha**" ambapo maelezo mapana kuhusu umuhimu wa kujua lugha nyingi yametolewa.

Katika kila somo kuna kipengele cha sarufi ambacho kinagusia matumizi ya hali ya kuamuru.

## 8.7. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kwamba mkufunzi halazimishwi kuwa mtumwa wa kifungu cha habari au mifano iliyotolewa katika kitabu fulani. Ana haki au idhini ya kufanya utafiti mahali mbalimbali na kuchagua matini au vifungu vya habari mbalimbali ambavyo anaona kuwa ni muhimu kwa wanafunzi wake kulingana na kiwango chao kwa ajili ya kuimarisha shauku yao ya kuitumia kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

## 8.8. Tathmini kuhusu mada ya nane

Patia wanafunzi maswali ya tathmini ya mada ya nane. Kila mwanafunzi ajibu maswali mwenyewe katika daftari lake.

**Majibu ya tathmini:**

1. Ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda.
2. Lugha nne: Kinyarwanda, Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili.
3. Ni vituo vya redio na televisheni,
4. - malighafi: ni vitu vinavyotumika kutengenezea vitu vingine
   - chatu: aina ya nyoka mkubwa anayeweza kumeza mtu
   - mawaidha: maneno yenye mafunzo kuhusu mambo mema ya kutenda
5. Kujaza sentensi kwa kutumia neno lililoko mabanoni:

i. rekebisha

ii. andika

iii. jifunzeni

7. Kuonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii:

- Lugha hutuwezesha kuwasiliana,
- Lugha hutumiwa katika utafiti,
- Lugha hutumiwa shuleni (kufundisha na kujifunza),
- Lugha huburudisha.

## 8.9. Kazi za ziada

### 8.9.1. Kazi za urekebishaji

Jaza jedwali lifuatalo ukizingatia hali ya kuamuru, tungo ya kinishi na tungo kanushi.

| Kitenzi | Hali ya kuamuru / tungo ya kinishi | | Hali ya kuamuru / tungo kanushi | |
|---|---|---|---|---|
| | Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
| Jifunza | jifunze | (1) | (2) | Msijifunze |
| Jipodoa | (3) | Jipodoeni | Usijipodoe | (4) |
| Leta | (5) | Leteni | (6) | msilete |
| Jadili | Jadili | (7) | Usijadali | (8) |
| Kula | (9) | Kuleni | (10) | Msile |
| Kuja | njoo | (11) | usije | (12) |

**Majibu:** (1) jifunzeni, (2) usijifunze, (3) jipodoe, (4) msijipodoe, (5) lete, (6) usilete, (7) jadilini, (8) msijadili, (9) kula, (10) usile, (11) njooni, (12) msije

### 8.9.2. Kazi jumuishi

a. Eleza umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwa jamii ya Wanyarwanda.

b. Tunga insha isiyopungua maneno 100 kuhusu mada ifuatayo " Faida ya Wanyarwanda kuingia katika Jumuia ya Afrika Mashariki."

**Kielelezo:**

Kazi hizi ziwe za kibinafsi na mkufunzi aongoze wanafunzi kushughulikia maswali haya kwa kutumia vitabu mbalimbali au mtandao ili kupata maoni faafu na yenye mpangilio mzuri.

### 8.9.3. Kazi za nyongeza

**a. Amrisha sentensi zifuatazo:**

i. ………………………maziwa yote myamalize ! (kunywa katika hali yakinishi/ wingi)

ii. ……………Ubaoni majibu ya maswali haya yote ! (andika katika hali yakinishi/umoja)

iii. ……………………kelele darasani wakati wa masomo! (piga katika hali kanushi wingi)

iv. …………………..jina la Bwana Yesu! ( sifu katika hali yakinishi wingi)

v. …………………..karatasi mfanye jaribio la Kiswahili! ( chukua hali yakinishi/wingi)

**Majibu:**

i. Kunyweni maziwa yote myamalize !

ii. Andika Ubaoni majibu ya maswali haya yote !

iii. Msipige kelele darasani wakati wa masomo!

iv. Sifuni jina la Bwana Yesu!

v. Chukueni karatasi mfanye jaribio la Kiswahili!

**b. Zungumzia kuhusu "Nafasi ya vyombo vya habari katika kuendeleza lugha ya Kiswahili." Usiandike chini ya maneno 250 na usizidi 300.**

**Kielelezo**

Kazi hii iwe ya kibinafsi na mkufunzi aombe kila mwanafunzi kutunga insha yake mwenyewe kwa kuzingatia sehemu muhimu za insha.

# MAREJEO


1. **Ntawiyanga, S. na Wenzake** (2016). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha kwanza.* Longhorn Publishers (K) Ltd.
2. **Ndalu, A. E. (2016).** *Masomo ya Kiswahili Sanifu, Kidato cha 2.* Moran (E.A.) Publishers Ltd.
3. **Rwanda Education Board (2019).** *Kiswahili kwa shule za Rwanda, Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 4.* Rwanda Education Board.
4. **Rwanda Education Board (2019).** *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Michepuo Mingine, Kidato cha 6.* Rwanda Education Board.
5. **TUKI (2004).** *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Pili.* Oxford University Press.
6. **NKWERA,** F.M.V. (1979). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo.* Tanzania Publishing House, Dar-es-salaam, Tanzania.
7. *https://sw.wikipedia.org/wiki/Kito_(madini)*
8. *https://www.youtube.com/watch?v=NK4M_yrYIJI*
9. *https://www.youtube.com/watch?v=G91GtbgdZKA*
10. *http://swa.gafkosoft.com/maigizo*
11. *https://www.facebook.com/1416762588414463/posts/hali-ya-kuamuru-hali-hii-ilichambuliwa-kwenye-tawi-la-mutanga-jumapili-hii-kidat/1823486384408746/*